

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 8 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Moja leo ni Kikao cha Ishirini na Nne. Katibu.

#### NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

#### MASWALI NA MAJIBU

Na. 197

**Hitaji la Watumishi na Vifaa Tiba – Hospitali ya Wilaya ya Newala**

**MHE. JAMES F. MBATIA (K.n.y MHE. RASHID A. AKBAR)**  
aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia Hospitali ya Wilaya ya Newala watumishi pamoja na vifaa tiba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar, Mbunge wa Newala Vijijiini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi kwa kuhakikisha vituo vinakuwa na vifaa tiba vinavyohitajika. Hospitali zinapatiwa rasilimali watu na fedha kwa ajili ya kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendenishi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi 198,671,475mpaka sasa shilingi 120,510,860 zimepokelewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na dawa. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Serikali imetenga shilingi 244,066,959.92 kwa ajili ya vifaa tiba na dawa katika Hospitali ya Wilaya ya Newala.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa watumishi ni changamoto inayovikabili vituo vingi vya kutolea huduma za afya nchini. Hata hivyo Serikali inaendelea kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya kadri vibali vya ajira vinavyopatikana. Mwezi Novemba, 2017 Halmashauri ya Mji wa Newala ilipata watumishi 12 wa kada mbalimbali za afya na katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri imeombwa kibali cha kuajiri watumishi 60 wa kada mbalimbali za afya. Serikali itaendelea kupeleka watumishi wa afya, vifaa tiba na vitendenishi ili kuboresha huduma za afya katika Wilaya ya Newala.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia nilikuona, swali la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Vifaa tiba ni tatizo kubwa kwenye hospitali nyingi nchini na utajiri mkubwa tulionao kuliko wote ni afya za mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, swali, Wizara hii ina upungufu wa zaidi ya sekta ya afya zaidi ya asilimia 50 ya watumishi. Serikali inaji-*commit* nini kuhusu kuhakikisha watumishi wa kutosha wa Hospitali ya Newala wanapatikana kwa wakati ili wawzeze kutoa huduma zinazostahiki?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Hospitali ya Kilema iliyoko Vunjo au ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ina tatizo la vifaa tiba na watumishi wake kwa wakati huu nesi mmoja anahudumia zaidi ya watu 30 wodini. Serikali inatoa kauli gani hapa ili hospitali hii nayo ipate watumishi wa kutosha pamoja na vifaa tiba kwa ajili ya afya za binadamu?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Josephat Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na *commitment* ya Serikali ili kuhakikisha kwamba watumishi wa afya wanapelekwa wa kutosha Newala ni kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi. Maombi yao ni kupatiwa watumishi 60 na hii naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbatia kwa niaba ya Mheshimiwa Ajali Akbar kwamba ni *commitment* ya Serikali kuhakikisha pindi fursa za ajira zitakapokuwa zimetolewa hatutaisahau Newala.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Hospitali yake ya Kilema ambayo anasema wastani Nesi mmoja anahudumu wagonjwa 30 ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaweka vifaa vya kutosha lakini pia na watumishi wa kutosha. Ndio maana wakati Mheshimiwa Waziri wa dhamana ya ajira alivyokuwa anahitimisha alisema ndani ya Bunge hili tunategemea kuajiri watumishi wa kutosha. Katika watumishi 59,000 watakaoajiriwa sehemu kubwa ni upande wa elimu na afya, naomba nimhakikishie ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunapunguza mzigo mkubwa kwa wahudumu kwa maana ya manesi ili na wao wawe na fursa ya kuweza kuhudumia wagonjwa kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie na Hospitali ya Kilema tutaikumbuka.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Nape Nnauye, swalii la nyongeza tafadhali.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Katika sekta iliyoathirika sana wakati wa zoezi la uhakiki wa vyeti, suala zima la vyeti *fake* ni sekta ya afya. Jimboni Mtama baadhi ya zahanati tumelazimika kuzifunga kabisa kwa sababu watu wameondolewa.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini Serikali isichukue hatua za dharura kwenye haya maeneo ambayo zahanati zimefungwa badala ya kusubiri *process* hii ya kuajiri watumishi wapya wa afya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo nilifanikiwa kupita na kuona kazi nzuri ambayo imefanyika katika suala zima la ujenzi wa vituo vya afya ni pamoja na Jimbo lake la Mtama, kwanza naomba nimpongeze.

Mheshimiwa Spika, tukiwa hapa ndani bungeni Mheshimiwa Mkuchika alitoa taarifa kwamba kama yuko Mbunge yeoyote, wa eneo lolote ambalo tumelazimika kufunga zahanati au kituo cha afya kwa sababu ya ukosefu wa watoa huduma aandike barua ampelekee ili tatizo hili lisiweze kutokea.

Mheshimiwa Spika, naomba kama Mheshimiwa Mbunge hakuwepo siku hiyo atumie fursa na bahati nzuri yeye yuko jirani sana na Mheshimiwa Mkuchika ili hicho anachokisema kisiweze kutokea.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na swali linaulizwa na Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara. Mheshimiwa Gashaza tafadhali.

Na.198

### **Hali ya Usalama katika Jimbo la Ngara**

**MHE. ALEX R. GASHAZA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwepo na tatizo kubwa la hali ya usalama katika Jimbo la Ngara tangu mwaka 1993 kutokana na kuwa mpakani mwa nchi za Rwanda na Burundi ambapo kuna mwingiliano mkubwa wa wageni/wahamiaji haramu kutoka nchi hizo.

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha Kanda Maalum ya Kipolisi katika Wilaya ya Ngara ili kudhibiti hali ya usalama?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya polisi katika Kata ya Mabawe, Muganza, Kirushya, Mtobeye, Mbuba na Nyakisasa?

(c) Kwa kuwa Jeshi la Polisi Wilayani Ngara lina gari moja tu zima na lingine bovu bovu, je, ni lini Serikali itatupatia angalau magari mawili, moja kwa ajili ya Tarafa ya Rulenge na la pili kwa ajili ya Tarafa ya Murusagamba?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alex Gashaza, Mbunge wa Ngara lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama katika Jimbo la Ngara kwa sasa imeimarika ikilinganishwa na miaka iliyopita. Wilaya ya Ngara imepakana na nchi jirani za Rwanda na Burundi. Serikali imeweka mikataba ya ujirani mwema na nchi za Rwanda ambapo Jeshi la Polisi hufanya doria za pamoja mipakani.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto katika mipaka yetu na nchi ya Burundi inayotokana na kukosekana kwa

amani katika nchi hiyo na kupelekea watu kuvuka mipaka. Aidha, Jeshi la Polisi nchini limeanzisha vituo vya ulinzi shirikishi ili kujenga uhusiano wa pamoja na wananchi ili kuimarisha hali ya usalama katika eneo hilo. Kwa sasa hali ya usalama katika eneo hilo imeimarika na hakuna haja ya Serikali kuanzisha Kanda Maalum ya Kipolisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la uhaba wa vituo vya Polisi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Ngara na katika Kata za Mabawe, Muganza, Kirushya, Mtobeye, Mbuba na Nyakisasa. Aidha, katika Kata ya Muganza kitajengwa Kituo cha Polisi eneo la Mkalinzi kwa nguvu za wananchi ambapo katika Kata za Mabawe, Mtobeye, Mbuba na Nyakisasa Polisi hutoa huduma kupitia Vituo Maalum vya Operesheni vya maeneo ya Murugyagira, Rulenge, Kabanga na Bugaramo. Hata hivyo, Serikali itajenga vituo vya polisi katika maeneo hayo kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, hii ni sauti ya zege, kwa hiyo msiwe na wasiwasi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Gashaza swalii la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nitaomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Ngara kimejengwa tangu enzi za ukoloni na majengo yake yamechakaa pamoja na nyumba za watumishi kwa maana nyumba za askari wetu. Sasa ni lini Serikali itaweza kukarabati kituo hiki cha polisi na nyumba za askari wetu?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, wananchi wa Jimbo la Ngara wameathirika kwa kiasi kikubwa sana na operesheni zinazoendelea hususani za Uhamiaji. Maeneo mengi Dar es Salaam, Kahama, Arusha, Ngara kwenyewe wananchi hawa wanapokamatwa kwa kuhisiwa na kueleza kwamba wanatokea Ngara moja kwa moja wanachukuliwa kwamba

ni wahamiaji haramu. Wamekuwa wakipigwa na kuumizwa na baadaye baada ya kujiridhisha inaonekana kwamba ni Watanzania halisi. (*Makof*)

Sasa je, Serikali iko tayari pale inapobainika kwamba wananchi hawa wamehisiwa, wakadhalilishwa, wakapigwa wako tayari kulipa fidia kwa hawa wananchi wanaokuwa wamedhalilishwa na kupigwa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa *Engineer Masauni tafadhali.*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza alitaka kujua kuhusiana na uwezekano wa kukarabati Kituo cha Polisi Ngara pamoja na nyumba za polisi. Kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi kwamba dhamira hiyo kwa Serikali ipo na pale tu ambapo hali ya kifedha itaruhusu tutakarabati kituo hicho cha Ngara na nyumba za polisi pamoja na maeneo mengine nchini ambako kuna changamoto kubwa za uchakavu wa vituo na nyumba za polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na wananchi ambao wamepigwa na kuonekana kwamba wamedhaniwa kwamba si Watanzania. Kwanza si utaratibu wa Jeshi la Polisi kupiga raia ama hata wageni. Kuna utaratibu wa kisheria ambao ikiwa mgeni ama raia amevunja sheria unatakiwa uchukuliwe kwa mujibu wa sheria. Nadhani suala hili labda Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili tukae tuone jinsi gani tunaweza kulichunguza ili tujue hatua za kuchukuliwa baada ya hapo kama kutakuwa kuna ukiukwaji wa sheria, sheria iweze kufuata mkondo wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga nilikuona, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Matatizo yaliyopo Ngara ni sawa kabisa tena yanapita ya Jimbo la Mlimba. Jimbo lenye kata 16 halina kituo cha polisi

wala gari la polisi na kupelekea Mahabusu kukaa muda mrefu sana ili kuwapeleka katika Mahakama au Magereza yaliyoko kilometra 265. Je, ni lini sasa Serikali itaboresha miundombinu ya Jeshi la Polisi ndani ya Jimbo la Mlimba angalau uwapatie gari basi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi la nyongeza. Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa *Engineer* Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni sahihi katika Jimbo la Mlimba kuna upungufu ama ukosefu wa Kituo cha Polisi, lakini kama sehemu ya mkakati wa Serikali wa kujenga vituo 65 vya polisi nchi nzima tunaamini Mlimba ni moja ya katika maeneo hayo. Kwa hiyo, tu nimuombe Mheshimiwa Mbunge avute subira pale ambapo mpango huo utakapokuwa umekamilika kituo cha polisi kitapatikana Mlimba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwanko, swali la mwisho la nyongeza tafadhali.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali la kwanza la Mheshimiwa Gashaza lilikuwa ni Ngara kuanzishiwa Kanda Maalum ya Kipolisi na Wilaya ya Ngara, Kakonko, Kibondo, Kasulu na Kigoma ni maeneo ambayo yanapakana na nchi nne yaani Burundi, Rwanda, Congo na Zambia kwa upande wa majini Kusini. Ni kwanini Serikali isione umuhimu wa kuanzisha kanda maalum kwa sababu *zone* ile ndiyo *zone* inayopitisha silaha ambazo hatimaye zinakuja kutushambulia katikati ya nchi yetu. Ni kwa nini Serikali isione umuhimu wa wilaya hizo tano kuanzishiwa Kanda Maalum ya Kipolisi ili kudhibiti uingizaji wa silaha katika nchi yetu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Kanda Maalum.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika swali

langu la msingi kwamba kuna jitihada kadhaa ambazo tumezichukua za kuimarisha hali ya usalama katika maeneo ya Mkoa wa Kigoma kwa ujumla wake ikiwemo hasa maeneo ya Wilaya ya Ngara. Kutokana na jitihada hizo imepelekea kwamba eneo hilo kwa sasa hivi kukosa vigezo vya kuweza kuanzisha ama umuhimu wa kuanzisha Kanda Maalum. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge aridhike kwamba kwa sasa hivi akubaliane na sisi kwamba eneo la Ngara bado halijakidhi vigezo hivyo kutokana na kuimarika kwa hali ya usalama katika maeneo hayo.

Na. 199

**Malipo ya Fidia kwa Askari Aliyejeruhiwa/Kufa  
akiwa Kazini**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta mabadiliko katika sheria inayosimamia malipo ya fidia kwa askari anayejeruhiwa au kupoteza maisha akiwa anatekeleza majukumu ya kulinda usalama ndani au nje ya nchi kwenye vyombo vya *UN* au *SADC Mission* ili kuendana na mabadiliko ya kupanda kwa gharama za maisha?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, malipo ya fidia kwa askari aliyejeruhiwa au kufariki akiwa anatekeleza majukumu ya ulinzi wa amani katika Umoja wa Mataifa hupangwa na kusimamiwa na Umoja wa Mataifa. Kwa kawaida, Umoja wa Mataifa hukaa vikao vya maamuzi na kutoa waraka ambao kwa ujumla hutekelezwa na nchi zote zilizopeleka majeshi katika Misheni za Umoja wa Mataifa unaofafanua stahiki mbalimbali za malipo kwa wanajeshi wanaoumia au kufariki wakati wa kutekeleza majukumu ya ulinzi wa amani.

Waraka huo huzijulisha nchi wanachama zinazochangia vikosi, Maafisa wanadhimu na waangalizi wa amani stahiki ya malipo. Hivyo, siyo jukumu la nchi husika kuamua ilipwe fedha kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Misheni za *SADC*, hadi sasa hakuna Misheni inayomilikiwa na *SADC* pekee, bali iliyopo inaitwa *Force International Brigade* ambayo imeunganishwa na Misheni ya Umoja wa Mataifa nchini DRC ambayo taratibu za kulipa askari aliyeumia au kufariki bado inasimamiwa na Umoja wa Mataifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa afisa au askari aliyeumia, utaratibu huo hufanyika kwa kuwasilisha nyaraka muhimu ambazo hutoa mwelekeo wa kiwango alichoumia ili alipwe kulingana na stahili.

Mheshimiwa Spika, kwa afisa au askari aliyefariki, Umoja wa Mataifa kwa sasa inalipa fidia ya dola za Kimarekani 70,000 kwa askari wa nchi yoyote aliyefariki akiwa anatekeleza majukumu ya ulinzi wa amani katika Misheni za Umoja wa Mataifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chumi swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inajiridhisha vipi kwamba ile fidia ya dola 70,000 inayotolewa inawafikia walengwa hasa watoto au mke wa marehemu ambaye anakuwa amepoteza maisha anapokuwa katika vikosi vyetu vya kulinda amani nchi mbalimbali huko duniani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni muda mrefu sasa tunaendesha mambo yetu ya ulinzi bila kuwa na sera ya ulinzi, je, ni lini Serikali itakamilisha sera hii ili kusudi pamoja na masuala haya ya ulinzi wa amani sehemu mbalimbali duniani. Sera hiyo iweze kubainisha maeneo mbalimbali

ambayo kwa namna moja au nyingine yatafanya vikosi vyetu vinavyoenda kulinda amani huko duniani viweze sio tu kunufaika kwa mujibu wa taratibu za *UN*, lakini pia kwa mujibu wa taratibu za nchi yetu? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tafadhali.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, fedha zinazotolewa kama fidia zinawafikia wahusika kwa sababu Tanzania tumeshakuwa na uzoefu wa jambo hili, tumeshapoteza askari wetu na kuna walioumia, fedha zilizotolewa familia zinaitwa Makao Makuu ya Jeshi na wanakabidhiwa bila ya tatizo lolote na inapobidi basi msimamizi wa mirathi ndiye ambaye anakabidhiwa akiwa pale Makao Makuu ya Jeshi. Mpaka sasa hivi kwa matukio yote yallyotukuta hakuna tatizo la mtu kudhulumiwa na hivyo tunaamini kwamba fedha hizo huwa zinawafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili ya Sera ya Ulinzi, kama tulivyowahi kusema mara kadhaa hapa Bungeni, sera hii rasimu yake ipo tayari, imeshajadiliwa na ngazi zote na kinachosubiriwa ni maoni kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama mdau ili wakishatoa maoni yao basi hatua zilizobaki za kuikamilisha sera hii ziweze kuchukuliwa.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, upande wa CUF sasa.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupana nafasi, Mheshimiwa Waziri amesema kama askari au afisa amefariki analipwa dola 70,000. Sasa ningependa kujua dola 70,000 hizi wanalipwa warithi wake *cash* au kuna mgao wa Serikali unakatwa kutoka hizi kama ambavyo wanakatwa wale askari wanaoenda katika misheni zile, sijui umenielewa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Spika, fedha hizi hazikatwi, wanapewa dola 70,000 zote lakini sio mwisho, hii ni fidia kutoka Umoja wa Mataifa lakini askari ye yeyote anayepoteza maisha ana fidia vilevile kutoka hapa nyumbani. Kwa hiyo, kuna fedha zinazotolewa na Wizara kwa ajili ya kulipa fidia familia ya wale ambao wamepoteza maisha wakiwa kazini.

**SPIKA:** Tunaendelea sasa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali linaulizwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Nyina Mtemi.

Na. 200

**Kuboresha Miundombinu ya Barabara Zinazoelekea  
Mamba Miamba Kiwandani**

**MHE. ANNE K. MALECEL A** aliuliza:-

Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (*LAPF*) umemuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuamua kukiboresha Kiwanda cha Tangawizi cha Mamba Miamba kilichoko Wilaya ya Same katika Jimbo la Same Mashariki.

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu sasa kuboresha barabara zinazoelekea Mamba Miamba Kiwandani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Kuteuliwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwembe – Miamba – Ndugu yenye urefu wa kilometra 90.19 inayopita eneo la Mamba Miamba Kiwandani ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na *TANROADS* Mkoa wa Kilimanjaro. Katika

mwaka wa fedha 2017/2018, barabara hii imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1.487 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo ya muda maalum kwenye eneo lenye urefu wa kilometa 22.5 katika Vijiji vya Mtunguja, Mhezi, Kwizu, Marindi, Mshewa, Mwembe, Mbaga, Gohe, Kambeni na Manka pamoja na matengenezo ya kawaida yanayofanyika katika Vijiji vya Dindimo, Kanza na Miamba. Vilevile kufanyika matengenezo ya madaraja yatakayohusisha ujenzi wa madaraja (*drifts*) mapya mawili katika Kijiji cha Mbaga na ukarabati mkubwa wa Daraja la Mwerera liliopo katika Kijiji cha Mwerera.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 barabara hii pia imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1.250 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo mbalimbali yakiwemo ya ukarabati na matengenezo ya kawaida na muda maalum.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo muhimu barabara hii ili iendelee kuitika bila matatizo muda wote.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Spika, swali langu kubwa hapa lilikuwa ni barabara zinazoelekeea Mamba Miamba Kiwandani, basi naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri swali moja kubwa kidogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara zinazoelekeea Mamba Miamba Kiwandani zipo za aina mbili, ya kwanza ni barabara inayounganisha Kiwanda cha Tangawizi na masoko ya ndani na nje ya nchi na barabara hii inatokea Mkomazi Kisiwani kwenda Same na barabara ya pili ni barabara zinazounganisha walima tangawizi (wakulima) na kiwanda chao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne mwaka 2009 alikuja Mamba Miamba ye ye mwenyewe akaona jitihada za wananchi, akatoa bilioni 2 za kujenga barabara za kuwaunganisha wakulima na kiwanda chao. Je, Mheshimiwa Waziri huoni kwamba ili uelewe tatizo kubwa la miundombinu ya kiwanda kile ni vyema wewe mwenyewe

ukawaahidi wananchi wa Mamba Miamba utakwenda lini kule ili uweze kujibu haya maswali vizuri, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, unaenda lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nipo tayari kwenda, lakini uniruhusu nimpongeze tu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu najua kupatikana kwa kiwanda hiki ni pamoja na juhudzi zake, lakini niwashukuru na kuwapongeza Mkuu wa Wilaya kwa sababu Mkuu wa Wilaya pia amekuja akiwa na ombi la kutembelea maeneo haya. Natambua kwamba lazima tuboreshe barabara ambazo zinawahudumia wananchi kupeleka malighafi kwenye kiwanda hiki, lakini pia kutoa mazao yanayotokana na kiwanda hiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia barabara hii ambayo nimeizungumza ni muhimu sana kwa sababu inapokwenda kuunganisha Mkomazi pia inatoa huduma kwa ajili ya utalii. kwa hiyo, nipo tayari Mheshimiwa Mbunge nitakuja Same tutembelee maeneo hayo. (*Makof*)

**SPIKA:** Jamani swali hili linahusu Same sasa..., Mheshimiwa Damas Ndumbaro nilikuona, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya Likuyufusi – Mkenda mpaka Msumbiji ambayo inaunganisha Jimbo la Mheshimiwa Jenista Mhagama na nchi ya Msumbiji ambayo katikati hapa kuna wawekezaji wengi sana wamefungua na viwanda lakini barabara hiyo bado ni ya vumbi.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha Iami ili kunufaisha Jimbo la Songea Mjini, Jimbo la Peramiho pamoja na wawekezaji waliopo ikiwa kuleta masoko nchini Msumbiji? (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu la Wangoni wote, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimponegeze sana Mheshimiwa Ndumbaro kwa sababu ukikutana naye yaani ni barabara ya mchepuo, barabara ya Likuyufusi – Mkenda, kwa hiyo, nimponegeze pia Mheshimiwa Jenista kwa sababu mara nydingi sana amefuatilia barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii ya Likuyufusi – Mkenda lakini pia tumetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja kule Mkenda, najua hii ndio changamoto ilikuwa kubwa sana ya eneo hili kwa maana hiyo kwamba tumetenga fedha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nitaendelea tu kukupa mrejesho na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa Jenista usiwe na wasiwasi eneo hili tumelitengea fedha.

Mheshimiwa Spika, pia daraja hili la Mkenda ni muhimu sana pia kwa wananchi ambao wanakwenda Mbamba Bay kwa sababu ukitoka Mkenda kwenda kule Tingi hii ni muhimu sana wanaitegemea barabara hii ili waweze pia kutembea na kuvuka kuja upande huu wa Peramiho. Kwa hiyo, tumejipanga vizuri. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana na bado tupo Wizara hii hii, swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini na hili ndio swali la siku la Kibunge, lisomeni ninyi wenyewe mtaona lilivyokaa.

Na. 201

### **Ukarabati Uwanja wa Ndege – Mtwara**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali haitaki kukarabati Uwanja wa Ndege Mtwara?

## **NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za manunuzi kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara. Hadi sasa mkandarasi kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa kiwanja hiki amepatikana ambaye ni *Beijing Construction Engineer Group Co. Ltd.* ya China kwa gharama ya shilingi bilioni 50.366. Hatua iliyobaki ni mkandarasi kukamilisha taratibu za kupata udhamini (*bank guarantee*) ili aweze kulipwa malipo ya awali (*advance payment*) na kukabidhiwa eneo la mradi. Hivyo, mradi huu utaanza kutekelezwa mara tu baada ya taratibu za manunuzi kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kumsimamia mkandarasi akamilishe jukumu lake ili kazi ya ukarabati wa uwanja uweze kuanza mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maftah Serikali sio kwamba haitaki, swali la nyongeza

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, asante. Nashukuru kwa majibu mafupi na *precise* ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu wa manunuzi ni mchakato na majibu yake hayajaeleza kwamba *exactly timeframe* ni lini Serikali imempa huyu mkandarasi kukamilisha mchakato wake ili ujenzi na ukarabati uanze mara moja.

Sasa nilikuwa naomba kupata majibu kwamba ni lini hasa, ni baada ya miezi mingapi huyu mkandarasi atakuwa amemaliza?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na utaratibu huko miaka ya nyuma kwamba baadhi ya vitu vinahamishwa mikoa ya Kusini na baada ya uhuru tu mapema ilihamishwa reli lakini pia na taa za Uwanja wa Ndege wa Mtwara. Sasa nilikuwa naomba kujua kwamba ukarabati ambao unatarajiwa kufanyika katika uwanja huu utahusisha pamoja na uwekaji wa taa za kuongozea ndege ambazo zilizoondolewa miaka ya nyuma? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mafupi Mheshimiwa Naibu Waziri Elias John Kwandikwa tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme ujenzi umeshaanza kwa sababu ujenzi una hatua mbalimbali, kwenye hatua hii mpaka mkataba umesainilwa na tumepata fedha nyingi. Kwa taarifa tu Mheshimiwa Nachuma awali tulikuwa tunakadiria tufanye matengenezo kwa shilingi zipatazo bilioni 39 lakini kwa kuzingatia maboresho na kufanya uwanja uwe na uwezo wa kupokea hata ndege *Airbus* aina ya A340-200 kwa hiyo, tumezingatia, huwezi kupokea ndege hii bila kuwa na taa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutakuwa na barabara na kutua na kurukia zenyet urefu wa mita 3,000, kutakuwa na maegesho ya ndege, kutakuwa na barabara za kuingilia katika uwanja na jengo la abiria lakini kuweza kutua ndege kubwa kama nilivyosema lakini pia taa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Nachuma usiwe na wasiwasi kwamba ule uwanja nafikiri miezi 20 ijayo utaona huduma zimeongezeka na utaendelea ku-*enjoy* huduma za ndege.

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa sababu ya muda, swali la Mheshimiwa Anna Joram Gidarya, Mbunge wa Viti Maalum Manyara tafadhali.

Na. 202

### **Migogoro ya Ardhi – Manyara**

**MHE. ANNA J. GIDARYA** aliuliza:-

Mkoa wa Manyara ni moja kati ya maeneo yanayokubaliwa na changamoto ya migogoro ya ardhi katika wananchi wa Babati Vijiji hasa katika Vijiji vya Amayango, Gedamara na Hifadhi ya Tarangire kwa takribani miaka 11 sasa bila ufumbuzi wowote, migogoro hiyo imesababisha wananchi kukosa elimu, afya na uchumi kushuka ambapo majengo ya jamii yaliyopo ni madarasa manne, bweni moja, matundu 13 ya vyoo vya shule na jengo la zahanati na majengo haya yote yamejengwa kwa nguvu za wananchi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza migogoro hiyo iliyodumu kwa muda mrefu na kurudisha maeneo ya wananchi yaliyochukuliwa na hifadhi?

(b) Endapo itabainika mipaka kati ya vijiji na hifadhi iliyooneshwa kwenye ramani ni batili. Je, Serikali husika iko tayari kuwalipa fidia wananchi wote walioathirika na migogoro hiyo kwa muda wa miaka 11?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Joram Gidarya, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhakiki wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa Tarangire na Vijiji vya Gedamar na Ayamango ulifanywa na wataalam wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi mwaka 2004 kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 160 la mwaka 1970 lililoanzisha Hifadhi ya Taifa Tarangire. Baada ya uhakiki huo eneo hilo lilitimikwa vizingi

(beacons) vya kuainisha mpaka wa hifadhi na vijiji husika ambao unafahamika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika uhakiki huo ilibainika kuwa kaya 245 za vijiji viliviyotajwa hapo juu zilikuwa ndani ya eneo la Hifadhi ya Taifa Tarangire kimakosa. Ili kuwaondoa wananchi wa vijiji hivyo kutoka kwenye eneo la hifadhi, Serikali iliama kuwalipa wananchi waliokuwa ndani ya eneo la hifadhi kifuta jasho kilichohusisha fidia ya mali, posho ya usumbufo, posho ya makazi na gharama za usafiri.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Vijiji vya Gedamar na Ayamango walilipwa jumla ya shilingi 137,845,592 tarehe 2 Februari, 2011 kuitia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati. Baada ya malipo ya kifuta jasho wananchi wengi waliondoka isipokuwa kaya 42 ambazo ziliomba kupewa eneo mbadala la kuhamia. Halmashauri ya Wilaya ya Babati ilikubali kuwapatia wananchi hao eneo maeneo ya kuhamia kwenye shamba la Ufyomi liliopo Gallapo ambapo wananchi hao wameshapatiwa maeneo katika shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hakuna mgogoro wa mpaka uliopo kati ya Vijiji vya Gedamar na Ayamango na Hifadhi ya Tarangire na mpaka uliopo kati ya hifadhi na vijiji hivyo ni sahihi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anna, Serikali inasema hakuna mgogoro wa mpaka, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Spika, asante, nasikitika majibu ya Serikali kwa asilimia 90 ni uongo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa walikaa kwenye hilo eneo miaka 20 iliyopita, fidia wanayosema ya kifuta jasho katika yale mabanda au tuseme zile nyumba waliwathaminishia TANAPA bila kuwashirikisha, kila mmoja fidia haikuzidi shilingi 300,000.

Mheshimiwa Spika, muda wote huo bila kuangalia riba wananchi walikaa mitaani na watoto wao waliathirika

walikosa na masomo kwa sababu walifukuzwa watoto wakawa wanakaa kwenye nyumba za watu baki. Leo hii Serikali inasema imelipa, siamini katika hili. Mheshimiwa Waziri upo tayari kwenda Babati kwa ajili ya kuhakikisha kama mgogoro upo au haupo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, *TANAPA* imelazimisha kuweka mipaka ya kudumu bila kuwashirikisha wahusika wenyewe wa mgogoro. Mkurugenzi anayezungumziwa kwamba amelipa, walienda kutoa amri yeye na Mkuu wa Wilaya mipaka ikawekwa, wananchi hawakushirikishwa, mgogoro huo haukuisha mpaka sasa. Lakini ni kwa nini sasa Serikali katika maeneo yenye migogoro ya hifadhi wamekuwa wakatili kuitilitiza, wananchi hawa ni Watanzania au sio Watanzania?

Mheshimiwa Spika, tunaomba majibu ya Serikali ili tusiumane umane hapa kila siku tunarudia suala la Ayamango na Gedamar, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo lililoulizwa kwa uchungu sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia kuhusu haya maeneo na mgogoro huu, amekuwepo mstari wa mbele sana, hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema, mgogoro huu umekuwepo kwa muda mrefu, lakini kilichokuwepo mwanzoni, hata hifadhi yenye ilikuwa bado haijajua mipaka yake na ndiyo maana mwaka 2004 walipoenda kuhakiki mipaka ilibainika kwamba hata baadhi ya maeneo ya hifadhi yalikuwa yako nje kwa sababu hata hifadhi yenye ilikuwa haijui. Lakini waliofanya uhakiki ilikuwa ni Wizara ya Ardhi ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kuhakiki mipaka, ndio waliofanya. Sisi hatuhakiki, Wizara ndiyo wanatuonesha mipaka kwa ramani hii kuwa mipaka ni hapa

na hapa, kwa hiyo, naamini kabisa kwamba walifanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwenda kuongozana naye, naomba nimhakikishie niko tayari baada ya Kikao cha Bunge tuongozane twende tukaangalie hali halisi iliyopo ili tuone kama bado mgogoro upo tuweze kuutatua kwa pamoja na wananchi waweze kushirikishwa katika utatuzi wa huu mgogoro. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, jibu la nyongeza tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Napenda tu kulihakikishia Bunge lako kwamba migogoro ya mipaka hasa katika maeneo ya hifadhi tayari Wizara kwa kushirikiana na *TANAPA*, tunavyo vijiji vipatavyo 427 katika hifadhi nane ambavyo hatua za uhamasishaji kwa ngazi ya mkoa na wilaya zimeanza, baadaye zitashuka kwenye ngazi ya vijiji na kote huko kutapimwa ili kuweza kupanga pia matumizi bora ya ardhi katika maeneo hayo na tayari pesa, shilingi bilioni nne, zimeshatolewa katika Kitengo chetu kile cha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, kwa hiyo, tuna imani na Tarangire ipo, itakwenda kufanyiwa kazi ili kuondoa utata wa mipaka. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Nassari, nimekuona.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni-*declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge hili ya Ardhi, Maliasili na Utalii na unakumbuka ulikuja Meru wewe, siku mimi nimeoa wewe ulikuja Meru ukimwakilisha Mama Makinda, na kwenye harusi ulizungumza ukasema mionganoni mwa vilio ambavyo Mbunge wenu Nassari amekuwa akipigia kelele kwenye Bunge ni suala la ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Ngarenanyuki ambayo inapakan na Hifadhi ya Taifa ya Arusha, hususan Kitongoji cha Momela, wamekuwa na mgogoro wa muda mrefu sana na Serikali na Wizara kwa sababu ya shamba namba 40 na shamba namba 41 yaliyoachwa na walowezi, walowezi ambao watu wa Meru hawa walichomewa nyumba miaka ya 1950, mwaka 1952 wakamtuma mtu *UN*, leo 2018 tumezungumza kwenye Bunge, aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa *Engineer Ramo Makani* akakubali kuondoka hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa masomoni Uingereza Mheshimiwa Mzee Mbatia huyu wakazungumza na wakakubaliana kwenda Meru Kuniwakilisha kunisaidia kumaliza mgogoro. Amefika Wilayani Arumeru kasimamishwa na Mkuu wa Wilaya kutokwenda kwenye mgogoro, Mheshimiwa Mzee Mbatia akarudishwa kutoka kijiji kule ameshatoka Moshi. Huyo Mkuu wa Wilaya ndio aliyekwenda kuweka vizingi bila kushirikisha wananchi na *imagine* Wizara ya Ardhi hii imetoa hati mwaka huu mwezi wa pili, mwezi wa tatu maaskari wamekwenda kupiga risasi ng'ombe wa wananchi kwenye shamba namba 40 na shamba namba 41. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati mimi nimetaka kulia, mwanaume nikajiuia, sasa swali langu, Naibu Waziri wewe uko tayari baada ya kikao hiki kuongozana na mimi twende ili tukaangalie mgogoro huu na ili tuweze kujenga mahusiano mema kati ya hifadhi na watu wa Momela? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri Hasunga.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mgogoro huu umedumu kwa muda mrefu na viongozi waliotangulia walishafika katika yale maeneo na wakaona hali halisi na mimi niko tayari kuongozana naye ili twende tukaangalie njionee mwenyewe ili tuweze kufanya uamuzi unaostahili.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuongeza tu ni kwamba, kama tulivyosema, Serikali iliunda Kamati ya Kitaifa ya kubaini aina yoyote ya migogoro nchini na Kamati hiyo imeshamaliza kazi yake na imeleta mapendeleko Serikalini ambayo Wizara zinazohusika zinayafanyia kazi na kufikia uamuzi, tukishafikia uamuzi nina imani kabisa tatizo hili la Meru litakuwa nalo ni mojawapo ambalo litaisha kabisa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga, swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, mgogoro uliopo Manyara unafanana na mgogoro uliopo Ulanga kati ya *Selous Game Reserve* na wananchi wa Kata za Ketaketa, Ilonga na Mbuga, Mheshimiwa Waziri analifahamu vizuri. Sasa wananchi wameendelea kukamatwa na kupigwa, huku siyo tu kuwachokoza wananchi, ni kunichokoza hata na mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri, lini yuko tayari kwenda kwa ajili ya kumaliza huu mgogoro kati ya *Selous Game Reserve* na wananchi wa hizi kata?

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kuongozana naye kwa sababu tulishakubaliana kwamba baada ya wiki hii Jumamosi inayofuata twende tukaangalie hali halisi katika eneo lile ambako kuna mgogoro. Kwa hiyo, tutakwenda, tutabainisha na tutakaa na wananchi ili tuone kwamba tatizo ni nini na tulipatie ufumbuzi.

**SPIKA:** Ahsante sana, tuendelee na maswali yanayofuata. Mheshimiwa Naibu Waziri, migogoro ya wahifadhi, ushauri wa jumla tu, wahifadhi nao hebu wasiwe na tamaa kubwa mno ya ardhi. Kila mahali wao wanaatamia ni migogoro tu. (*Makofii*)

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, tafadhali.

Na. 203

**Mgodi wa GGM Kuwasilisha Bajeti Yake Baraza la Madiwani Geita**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Mgodi wa *GGM* utawasilisha bajeti yake ya kuhudumia jamii katika Baraza la Madiwani la Geita ili tuweze kuangalia kipaumbele chao na kuwapa vipaumbele yya Halmashauri ya Geita?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Madini, Mheshimiwa Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, napenda sasa nijibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 105(1)(2) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na mabadiliko yake ya mwaka 2017 kinamtaka mmiliki wa leseni chini ya kifungu cha 7 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kuandaa Mpango wa Mwaka wa Uwajibikaji kwa Jamii (*CSR*). Mpango huo lazima ukubalike kwa pamoja na Mamlaka ya Serikali za Mtaa husika kwa kushauriana na Waziri anayehusika na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Waziri anayehusika na Fedha.

Mheshimiwa Spika, mpango huo unapaswa kuzingatia masuala ya mazingira kijamii, kiuchumi na shughuli za tamaduni zilizopewa kipaumbele katika Mamlaka ya Serikali za Mtaa ya jamii inayozunguka mgodi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 105(3), mmiliki wa leseni anapaswa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Serikali za Mtaa husika mpango huo aliouandaa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini na kupata idhini kutoka kwa Baraza la Madiwani wa Halmashauri. Aidha, kila halmashauri uliopo mgodi inapaswa kuandaa mwongozo wa utoaji wa huduma kwa jamii kwenye Halmashauri yao, kusimamia utekelezaji wake na kutoa elimu kwa wananchi wa wilaya husika juu ya huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Mgodi wa *GGM*, kwa kushirikiana na halmashauri mbili za Geita Mji na Wilaya ya Geita, umeweza kutekeleza mchakato wa kuandaa mpango wake wa kusaidia jamii (*CSR*) kwa mwaka 2018 kama sheria inavyotaka. Mchakato huo umehusisha wataalam kutoka halmashauri zote mbili na wataalam wa Sekretarieti ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa miradi iliyotambuliwa na halmashauri hizo kama vipaumbele umeshawasilishwa kwenye Mgodi wa *GGM* na umesharidhiwa na mgodi. Mgodi wa *GGM* unatarajia kutumia takribani shilingi bilioni 9.124 katika kutekeleza miradi ilio chini ya mpango wa *CSR*. Kiasi cha shilingi bilioni moja kitatumika kutekeleza miradi katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, takribani shilingi bilioni 6.824 zitatumika kutekeleza miradi katika Halmashauri ya Mji wa Geita na takribani shilingi bilioni 1.3 zitatumika kutekeleza miradi katika Halmashauri za Bukombe, Chato na Mbogwe.

Baada ya taratibu zote kukamilika, mpango huo utawasilishwa katika Baraza la Madiwani ili uweze kuidhinishwa. Miradi iliyokubaliwa na wadau wote kwa mwaka 2018 itaanza kutekelezwa kabla ya mwezi Juni, 2018.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita Vijijini swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nimpongeze Waziri kwa majibu mazuri, lakini naona majibu yake hayajitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, kwa kifungu cha 105(3) kama alivyoainisha Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kwamba mgodi utapokea maelekezo kutoka kwenye mabaraza mawili maana yake Geita Mjini na Vijiini, na mgodi utatulipa kama shilingi bilioni 9.1. Lakini kwa mchanganuo wa Halmashauri zetu, Halmashauri ya Geita Vijiini inapata asilimia 46, asilimia 54 zinabaki Geita Mjini. Sasa kwa maelezo na mchanganuo aliyoutoa Waziri *CSR* ya Halmashauri ya Geita inaingiaje kwenye Chato, Bukombe na Mbogwe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Geita Vijiini na Mjini tuna mgogoro na Mgodi wa *GGM*, tunawadai dola bilioni 12 wewe mwenyewe unafahamu na mlisauri watulipe kwanza dola laki nane mwezi wa kwanza, leo ni mwezi wa tano hatuoni majibu na hawatusikilizi, tumeshapeleka *demand*, sasa tunataka kupelekana mahakamani na Mgodi wa Geita unazidi kusafirisha dhahabu Jumanne na Ijumaa, na ili kibali cha kusafirisha dhahabu kitoke lazima walipe kodi za Serikali ninyi Wizara ndio mtoe kibali cha kusafirisha.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Wizara isichukue *action* ya kutusaidia kuwanyima kibali ili waweze kutulipa hata kesho hizo dola laki nane? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Wabunge wa Mbogwe na kwingine... Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Spika, katika swali la kwanza, ni kwamba mgawanyo wa fedha katika Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Geita Vijiini, haya ni makubaliano ambayo wao wenyewe walifikia na Baraza la Madiwani na Mheshimiwa Mbunge naye ni Mjumbe, kwa hiyo, walifikia maamuzi haya na huu ndiyo msimamo wa Halmashauri na hivyo ndivyo mgawanyo utakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shilingi hizo bilioni alizotitaja ambazo ni sawasawa na dola laki nane ambazo walisema kwamba wanatakiwa wapewe na Mgodi wa *GGM*, ni kwamba mpaka sasa hivi *GGM* wako tayari kutoa

hizo fedha. Mgogoro uliokuwepo ilikuwa ni Halmashauri ipi au akaunti ya Halmashauri ipi ipewe fedha hizo, na mpaka hapa ninapozungumza ni kwamba tayari Mkuu wa Mkoa kesho kutwa, siku ya tarehe 10 Mei, anakaa na hizi Halmashauri mbili, anakaa na hiyo *GGM* waelewane kwa pamoja ni Halmashauri ipi akaunti yake iweze kupewa fedha hizo na wao waweze kutafuta utaratibu wa kuweza kugawana fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa kuongezea, suala la Halmashauri ya Mbogwe na halmashauri nyingine, Chato na maeneo mengine, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba waendelee kushiriki vile vikao vya Halmashauri ili waweze kuelewana vizuri kuitia Sekretarieti ya Mkoa waangalie ni namna gani ya kugawanya hizo fedha, sisi kama Wizara tutasimamia tu kuhakikisha *GGM* wameweza kutoa fedha za *CSR*. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mbunge wa Mbogwe sijamuona hapa leo, swali la nyongeza Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Wilaya yetu ya Mbogwe kuna madini ya dhahabu na kumekuwa na mgogoro kati ya wananchi wa Nyakafuru pamoja na wawekezaji ambao wamekuja hapo. Sasa ninataka kujua msimamo wa Wizara uko vipi katika kuhakikisha kwamba leseni inatolewa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo wa Wilaya ya Mbogwe?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la nyongeza, nilitegemea utatetea kupata mgao wa *GGM*, sasa... (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wanaochimba Nyakafuru wanachimba chini ya leseni ya mtu mwингine, wanachimba bila kuwa na leseni, ni kama vile wachimbaji waliovamia leseni ya mtu mwингine. Sisi kama

Wizara hatuchochei wachimbaji wadogo kwenda kuvamia leseni ya mtu mwingine, huo siyo utaratibu. Lakini sisi kama Wizara ya Madini tuna mpango na mkakati wa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, tuna maeneo zaidi ya 44, tuna heka zaidi ya 238,000 kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tunaomba ushirikiane na wananchi wako kwa kuwapa elimu ya kutosha kwamba tunakwenda kuwagawia maeneo ambayo ni halali, wachimbaji wadogo wachimbe kwa uhalali ili waweze kujipatia kipato chao, lakini wasiendelee kuvamia leseni za watu wengine. Ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum Manyara, Mheshimiwa Cecilia Pareoso.

Na. 204

#### **Kuanzisha Viwanda vya Kusindika Wilayani Mbulu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. MARTHA J. UMBULLA)** aliuliza:-

Mazao ya pareto na vitunguu saumu yanalinwa Wilaya ya Mbulu na yana thamani na faida kubwa kwa wananchi.

Je, Serikali itakubaliana na mimi kuwa kuna haja ya kuanzisha viwanda vya kusindika mazao haya Wilayani Mbulu ili kuhamasisha kilimo cha mazao hayo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Charles Mwijage.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**  
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mazao ya pareto na vitunguu saumu yanayolimwa katika Wilaya ya Mbulu yana thamani na faida kubwa kwa wananchi. Hivyo, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Umbulla kuwa kuna haja ya kuendelea kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vyta kusindika mazao hayo Wilayani Mbulu ili kuchochaea zaidi kilimo cha pareto na vitunguu saumu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua faida zitokanazo na zao la pareto, Serikali iliamua kuanzisha Bodi ya Pareto kwa lengo la kudhibiti uzalishaji, usindikaji na biashara ya pareto nchini. Hivyo, kupitia Bodi ya Pareto na Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Serikali itaendeleza juhudhi za kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda vyta kuengua na kuchuja pareto ili kuongeza thamani ya zao hilo na kuwanufaisha zaidi wananchi katika maeneo yanayolimwa pareto ikiwemo Mbulu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa zao la vitunguu saumu, Wizara yangu kwa kupitia karakana za *SIDO* katika Mikoa ya Arusha na Kimlimanjaro zinatengeneza blenda ambayo inatumika kusaga zao hilo kuwa katika mfumo laini (*garlic paste*); teknolojia hii inapatikana kwa shilingi 1,800,000. Aidha, *SIDO* hutoa mafunzo kwa vikundi na watu binafsi juu ya usindikaji wa zao la vitunguu saumu katika mikoa inayolima zao hili.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nashauri Mheshimiwa Mbunge afike ofisi za *SIDO*, Mikoa wa Manyara zilizoko Babati kwa ufanuzi zaidi na hatimaye tuweze kushirikiana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia, swalı la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mazao haya ya pareto na vitunguu saumu na hata vitunguu maji ambavyo vinalimwa katika maeneo ya Mbulu na Karatu, wakulima wamekuwa wakiuza kwa vipimo vya debe badala ya kilo, na sheria ya vipimo inataka mazao haya yauzwe kwa kilo. Je, kwa nini Serikali isihakikishe kwamba mazao haya yanauzwa kwa kilo badala ya madebe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kumekuwa pia kuna changamoto ya wafanyabiashara kufuata mazao haya shambani jambo ambalo linamfanya mkulima ananyonywa na asipate faida ya kile anachokilima, hasa mazao ya vitunguu maji ambayo yanalimwa sana kwenye Tarafa ya Eyasi, Wilayani Karatu, lakini pia maeneo ya Mbulu.

Je, Serikali sasa mna mkakati gani wa kuhakikisha kunakuwa na *centeres* za uuzaji wa mazao haya ili mkulima aweze kufaidika na mazao anayoyalima? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia ujazo na uzito katika kupima mazao, marekebisho ya Sheria ya Vipimo Namba. 340 iko mezani kwangu na nimekataa kuisaini ilivyoletwa nikitaka twende kwa uzito, tupime kwa uzito. Nakubaliana na wewe na sitasaini mpaka wataalam wangu wakubaliane twende kwa uzito. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu vituo vya kuuzia mazao, napenda nimueleze Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote, wakulima wetu tuwahimize warudi kwenye ushirika, washikamane kuwadhibiti wale wanaokuja kunyemelea mazao. *Local Government* (TAMISEMI), wameshaanza zoezi la kuwa na *centers* ambako tutaweka mizani, lakini tukiwa na ushirika hao wanaonyemelea ambao wakulima tutaweza kuwadhibiti. Kwa hiyo, ni jukumu letu muisaidie Serikali sisi ndio Serikali twende pamoja tutaweza kuwasaidia wakulima wetu.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda bado tuko Wizara hiyohiyo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Baraza wa Wawakilishi, Mheshimiwa Jaku tafadhali.

Na. 205

**Uhaba wa Sukari - Tanzania Bara**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Pamoja na kuwepo viwanda vingi nya sukari hapa nchini bado kumekuwa na uhaba mkubwa wa bidhaa hiyo hususan kwa upande wa Tanzania Bara; mfano bei ya mfuko wa kilo 50 ni shilingi 65,000 kwa upande wa Zanzibar ambako kuna kiwanda kimoja tu cha sukari, lakini kwa Tanzania Bara mfuko huu wa kilo 50 huuzwa shillingi 120,000.

(a) Je, kuna tatizo gani linalofanya sukari iuzwe bei ya juu kiasi hicho kwa upande wa Tanzania Bara?

(b) Je, Serikali itachukua hatua gani ili kuweza kuwapatia wananchi unafuu katika upatikanaji wa bidhaa hiyo?

(c) Kwa upande wa Zanzibar katika kipindi ambacho matumizi ya sukari kwa wananchi yanaongezeka mfano, mwezi wa Ramadhan, Serikali inashusha ushuru wa kuingia sukari nchini. Je, kwa nini Serikali ya Muungano isizingatie utaratibu huu mzuri ili kuleta unafuu kwa Tanzania Bara?

**SPIKA:** Majibu ya swali Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**  
aliibju:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Buyuni, Zanzibar lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kuwa kwa vigezo vyovyote nya kupima uwepo wa bidhaa sokoni Tanzania Bara hakuna uhaba wa sukari. Kuhusu tofauti ya bei kat i ya pande mbili za Muungano ni kuwa zaidi ya asilimia 53 ya sukari itumikayo Zanzibar huagizwa kutoka nje kwenye vyanzo ambavyo gharama zake ni nafuu ukilinganisha na asilimia 29 zinazoagiwa upande wa Bara kujaza mapungufu ya uzalishaji. Lakini upande wa Bara na nchi nyingine za Afrika Mashariki bidhaa ya sukari kutoka nje hutozwa ushuru wa asilimia 100 ili kulinda viwanda nya ndani. Kutokana na sababu hizo bei huweza kutofautiana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua uamuzi wa kuhamasisha kusimamia kampuni kubwa nne zinazozalisha sukari ili zipanue uwezo wa mashamba na viwanda vyao. Zoezi linakwenda vizuri ambapo *Kilombero Sugar* tayari inaongeza uwezo wa uzalishaji maradufu kwa kuwekeza dola milioni 200 za Kimarekani. *Mtibwa Sugarkwa* kuwekeza shilingi bilioni 75 za Kitanzania wataongeza uzalishaji katika kipindi cha miaka mitano na kufikia tani 100,000 kwa mwaka toka tani 30,000 za sasa. *Kagera Sugar* wanawekeza shilingi bilioni 360 za Kitanzania ili kwa kipindi hicho hicho cha miaka mitano waongeze uzalishaji mpaka tani 170,000 kwa mwaka kutoka 75,000 za sasa. Wakati huohuo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inawekeza katika mradi kapambe wa Mkulazi Namba Moja na Namba Mbili wakilenga kuzalisha tani 250,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwekezaji huo na kwa kuzingatia kiteknolojia ya kisasa inayotumika bada ya miaka mitatu mpaka minne ijayo tutajitosheleza kwa sukari yenye bei nafuu na kuuza ziada nje ya nchi. Pamoja na faida hiyo sekta ya sukari itatuwezesha kutengeneza ajira zaidi ya 50,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikishusha ushuru au kuruhusu kuingiza sukari bila ushuru ili kutoa nafuu kwa bei kwa watumiaji wa sukari. Katika kipindi cha mwezi Machi mpaka Juni mwaka huu

Serikali kwa kuzingatia maoni ya wadau imetoa vibali nya kuagiza sukari tani 135,610 kwa kutoa ushuru pungufu kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya 100 ili kutoa nafuu kwa bei kwa wananchi pamoja na kuziba pengo la uagizwaji wa sukari kutoka nje.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku nimekuona swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kukiri kuwa Tanzania hakuna uhaba wa sukari katika majibu yake na amesema baada ya miaka mitatu au minne uhaba huu utapungua hiki ni kiswahili alichokiandika.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa tukifika katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani pamekuwa na kadhia hii ya upungufu wa sukari. Haioni Serikali imefika wakati ipunguze punguzo hili ili kuwalinda wananchi ukizingatia wananchi ndio walivyoweka Serikali hii madarakani na si aibu viongozi wetu Zanzibar hao Marais wetu mara nyingi ikafika mwezi Mtukufu wa Ramadhani huondoa ada hii na Tanzania Bara imeiga mambo mengi kutoka Zanzibar ikiwemo vyama vingi vimeanzia Zanzibar, haki za binadamu zimeanzia Zanzibar, matumizi ya dola yameanzia Zanzibar si aibu kuiga. (*Makofii*)

Je, haioni imefika wakati kuiga *formula* hii mara kadhaa unalinda viwanda, viwanda hivyo haviwezi kulindika wakati huu?

Mheshimiwa Spika, la pili tumo kwenye Tume ya Afrika Mashariki, lakini mpaka leo bidhaa za Zanzibar haziwezi kufika kwenye soko hilo mpaka upitie Tanzania Bara. Je, haijafika wakati Tanzania Bara mkatamka kwa Zanzibar sasa hivi isiingie katika soko hili kwa kupitia mgongo huo?

**SPIKA:** Majibu ya maswli hayo, kwa kifupi Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Charles Mwijage tafadhali.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeeleza kwanini, sukari inayozalishwa Tanzania Bara inakuwa na gharama kubwa. Nimesema tumeamua kusimamia viwanda hivi ili tuweze kuzalisha ajira. Sasa kuhusu kupunguza nimeeleza kwamba ushuru kwa makubaliano yetu ya *East Africa* ni asilimia 100, tumepunguza kutoka asilimia 100 kuja 25 tumeshapunguza kuja asilimia 25. Kuhusu bidhaa ya Zanzibar kama kuna mfanyakiareshara ana matatizo awasiliana na Waziri wa Zanzibar ambaye mimi na Sekretarieti inawasiliana naye. Mimi Zanzibar sina matatizo bidhaa zinakuja zinaingia nchini kama mtu hafuati viwango ana matatizo yake. Lakini *TBS* ya Tanzania Bara na Viwango vya Zanzibar wanawasiliana haya mambo madogo madogo myawasilishwe kwa watendaji kule na watendaji watayashughulikia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kamishna Turky nilikuona, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Nassir.

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana ya Waziri. Lakini katika majibu haya kuna swalii la msingi ambalo Waziri naona kalikimbia, nalo ni kwamba Zanzibar kuna kiwanda cha sukari kinazalisha na kinauzi sukari ile kwa shilingi 65,000 na hawaagizi sukari kutoka nje wao wamewekeza wanazalisha sukari wanauza shilingi 65,000 kwa wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, swalii la msingi ni kwamba viwanda vyetu vya Bara kwa nini hawawezi kutushushia bei saa hizi na ushahidi kamili ni huu ambaa natoa na Bunge hili lisikie sasa hivi. Ni kwamba sukari sasa hivi katika soko la dunia linauzwa kwa bei ya dola 390, ukilipa kodi ya asilimia 25 na VAT asilimia 18 sukari hiyo inasimama kwa bei shilingi 65,000, leo Watanzania tunalanguliwa kwa kuuziwa sukari hiyo shilingi 110,000 kwa misingi gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na hapa hapa tulioomba *cost of production* ndani ya Bunge hili wakati Naibu Waziri akiwa

Malima toka mwaka ule mpaka leo *cost of production* ya viwanda hivi hatujaletewa ndani ya Bunge hili jamani. (*Makofî*)

**SPIKA:** Hilo ndilo swalî la Mheshimiwa Jaku tangu mwanzo, Mheshimiwa Waziri wa Biashara ufanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nimejitalidi kulieleza suala hili ila muda wenyewe hautoshi. Ni kwamba gharama za uzalishaji kwa viwanda vya Bara ziko juu kuliko Zanzibar, naomba nimepewa muda, muache niwaeleze.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, Zanzibar sukari haitoshi kwanza.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba niwaeleze hili suala sio rahisi namna hiyo mnavyofikiria, ndio siyo suala rahisi, *I am very good in talking a can talk, simple rahisi*, Mheshimiwa Turky ulipopewa kibali na Serikali kuagiza sukari kwa nini wewe ukuuza bei rahisi? (*Kicheko*)

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane tafadhali.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Basi Turky ajibu, Turky na yeye apewe nafasi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, swalî hili ni la msingi sana kwa maisha ya wananchi wa Tanzania na kwa kweli halijapa majibu. (*Makofî*)

Kwa hiyo, tutalipanga tena kwenye maswali ya wiki ijayo ili Serikali ituletee majibu ya uhakika kama kweli

wananchi wa Tanzania Bara wanalazimika kulipa mara mbili ya bei inayouzwa Zanzibar kisa tu kulinda wenye viwanda haiwezekani hiyo. (*Makof*)

Kwa hiyo, Bunge linahitaji majibu ya uhakika zaidi *Chief Whip* wiki ijayo tutalipanga swalii hili ili tupate hasa ya uhakika nini kinachoenda kwenye jambo hili. (*Makof*)

Swali la mwisho kwa leo Elimu, Sayansi na Teknolojia swalii la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo tafadhali.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kabla hajajibu neno mimba litoke liwe ujauzito. Nashukuru.

Na. 206

### **Wanafunzi Wanaopata Ujauzito Kutoendelea na Masomo**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Mwaka 2017 lilitolewa tamko la kukataza watoto wa shule wanaopata ujauzito kwa sababu yoyote ile kutoendelea na masomo.

Je, kwa katazo hilo, Serikali imejipangaje kuhakikisha kuwa zile sababu zilizo nje ya uwezo wa wanafunzi kuhimili zinapatiwa ufumbuzi haraka?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la wanafunzi wa shule kupata ujauzito wakiwa masomoni kwa sababu mbalimbali zikiwemo zile wasizoweza kuhimili, sababu hizo ni pamoja na kubakwa, kutembea umbali mrefu kufuata

shule, na hivyo kupata vishawishi, mila na desturi potofu ambazo humlazimisha au kumuingiza mwanafunzi katika ndoa au mahusiano ya kimapenzi na kukosa mahitaji ya msingi kutoka kwa mzazi, mlezi hali ambayo humlazimisha mwanafunzi kujilingiza katika mahusiano ili aweze kupata mahitaji yake.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha sababu hizo zinapatiwa ufumbuzi kwa lengo la kumlinda mwanafunzi wa kike Serikali imetekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, imefanya marekebisho katika Sheria ya Elimu Sura ya 353 Toleo la 2002 kuitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya mwaka 2016 ambayo imeongeza kifungu cha 60(a) ambacho kinatamka wazi kuwa mtu yejote atakaye muweka ujauzito mtoto wa shule atafungwa miaka 30 au kwa klingereza naomba ninukuu; *"Any person who impregnates a primary school or secondary girl commits an offence and shall on conviction, be liable to imprisonment for a term 30 years."* Imeweka mkazo juu ya elimu ya afya ya uzazi na jinsia katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu yaani unasihi ambayo kwa sasa Wizara imeandaa kiunzi kinachoitwa (*guidance and counseling with services a guide for counselors and schools and teacher colleges*) kwa ajili kutekeleza huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia imezifanya shule zote za sekondari za kidato cha tano na sita kuwa na mabweni hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kike; imehimiza ujenzi wa shule za sekondari kila Kata hasa kwenye maeneo yenye wanafunzi ili kupunguza wanafunzi wa kike kutembea umbali mrefu.

Pia Serikali imejenga hosteli katika baadhi ya shule za sekondai za kata kwenye maeneo ambayo wanafunzi wa kike wanalazimika kutembea umbali mrefu ili kufikia shule na kwenye maeneo ambayo kuna mila na desturi potofu ambazo umlazimisha au kumuingiza mwanafunzi katika ndoa au mahusiano ya kimapenzi.

Mheshimiwa Spika, mwanafunzi wa kike anayekatisha masomo anaweza kujiunga na masomo kupita mipango ya elimu inayotolewa na Taasisi elimu ya watu wazima na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) huandaa na kuendesha programu za elimu mbadala kwa vijana na watu wazima kulingana na mahitaji yao kama vile mafunzo ya muda mfupi na marefu ya ujasiriamali stadi za maisha, ufundi wa awali na programu za kimasomo cha kujiendelea kwa watu wazima ili waweze kuendesha maisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo tafadhali.

**MHE SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nashukuru kwamba Serikali inatambua kwamba kuna changamoto nyingi za watoto wao kushindwa kwenda shule.

Mimi nilikuwa mmoja wa Wajumbe katika Kamati iliyozunguka nchi nzima kuangalia ni jinsi gani watoto hawa wanawenza kurudi shulen na Serikali kama mtakumbuka mwaka 2017 Naibu Waziri alisema tayari wameshaandaa mwongozo wa jinsi gani ya kuwarudisha watoto hawa shule. Lakini ghafla bin vuu mtu mmoja tu Mheshimiwa Rais akatoa hilo katazo.

Mheshimiwa Spika, sasa swalilangu, ninaomba kuja kwamba Serikali imeshafanya tathimini ya kuona kuna athali gani za kijamii, kiuchumi na kisaikolojia kwa watoto hawa wa kike pamoja na watoto wanaozaliwa ni athari zipi hasa zinaweza kuwapata hasa ikizingatiwa kwamba hii sheria baba wa watoto hao nao atakuwa amefungwa miaka 30 hawaoni kwamba kutakuwa na athari kubwa sana?

Mheshimiwa Spika, swalilili nchi nyingi pamoja na Zanzibar wanafunzi wanaopata ujauzito wanaendelea na shule, sasa hili jibu kwamba kuna elimu ya watu wazima. Serikali haioni kwamba hawa watoto wanaopata ujauzito wa miaka 12 mpaka 15, 16 ni watoto wadogo sana kiasi kwamba wakienda kwenye hiyo elimu ya watu wazima wanaenda kukutana na watu wazima. Lakini vilevile elimu

hiyo ya watu wazima haiku *coordinated* hata kidogo na kwa maana hiyo wanawapelekea watoto hawa kufanya pia, mapenzi hawa watu wazima kwa vyovyyote vile watawapa washawishi.

Serikali haioni kweli kuna kila sababu ya kuwapatia watoto hawa *special education...*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE SUSAN A. J. LYIMO:** ...ili waweze kuendelea na masomo yao?

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lyimo ni mwalimu tena mzoefu na ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo na Huduma za Jamii. Kwa hiyo, haya masuala anayafahamu sana lakini ameamua kuleta mjadala. Lakini naomba maswali yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba katizo la wanafunzi wanaopata ujauzito kurudi mashulenii metolewa na Mheshimiwa Rais naomba nimsahihishe kwamba katazo hilo limekuwepo toka mwaka 2002 kwa mujibu wa kanuni inayoitwa *The Expulsion and Exclusion of Students from School Regulation 2002* ilioanzishwa kwa mujibu wa kipengele cha 60(o) ya Sheria ya Elimu ya mwaka 1978. Kwa hiyo, alichofanya Mheshimiwa Rais ni kusisitiza kitu ambacho kilishaamuliwa toka siku nyingi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuhusiana na swali lake la pili kwamba elimu ya watu wazima haiwafai wale wanafunzi kwa sababu bado ni wadogo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema yeye ni mwalimu Serikali imeamua kuchukua uamuzi huo kwa sababu ya kumlinda mtoto.

Mtoto ambaye anapata ujauzito mara nyingi akirudi shuleni anakuwa ananyanyapaliwa na wenzake. Kwa hiyo, hata ye ye mwenyewe ata ukimruhusu aendelee na shule bado hawesi kuwa katika mazingira mazuri kisaikolojia. Lakini vilevile ni kwa sababu tunataka tuweke wazi kwamba hatutegemei wanafunzi wetu katika umri mdogo waendelee kufanya mapenzi wakiwa shuleni kwa sababu inawaathiri katika masomo yao. Kwa hiyo, ni suala la kuchagua na sisi tumechagua kwamba hatutaki tuchanganye mapenzi na elimu katika huo umri mdogo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda mtaona muda wetu umepita sana wa maswali inabidi tuishie hapa kwa siku ya leo.

Ninao wageni katika Jukwaa la Spika ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa Baraza la Jukwaa la Vyama vyta Siasa wakiongozwa na Mwenyekiti wao ambaye ni Mheshimiwa Magale John Shibuda kutoka Chama cha ADATADEA, huyo ni Mheshimiwa John Magale Shibuda. (Makof)

Wajumbe wa jukwaa hilo wa Baraza la Jukwa la vyama vyta siasa walio pamoja naye ni pamoja na Naibu Katibu Mkuu CCM Zanzibar, Dkt. Abdallah Juma Abdallah Mabodi, Ndugu John Momose Cheyo wa UDP, huyu ni Mzee Mapesa, Ndugu Hassan Kisabya Almasi wa NRA, Ndugu Juju Martin Danda, NCCR MAGEUZI, Ndugu Mohamed Ali Abdula kutoka Makini, Ndugu Peter Magwira kutoka DP, Ndugu Mohamed Masoud Rashid kutoka CHAUMA, Ndugu Said Sudi Said kutoka AFP na Ndugu Salum Mwalimu kutoka CHADEMA. (Makof)

Mheshimiwa Shibuda na Wajumbe hao wa Kamati ya Uongozi ya Baraza la Vyama vyta Siasa napenda kuwapongeza sana kwa kazi nzuri mnayofanya ya kujaribu kupata ufumbuzi kwa changamoto kadhaa zinazojitokeza kwenye Vyama vyta Siasa. Ninyi ndio makamisaa katika mchezo wa siasa, Baraza lenu linahitaji kupewa nguvu na kuungwa mkono ili liweze kuwa na tija zaidi. Sina shaka mko

na kiongozi mahiri, Mheshimiwa Magale John Shibuda na ninaamini kabisa kuititia ninyi, baadhi ya changamoto tulizonazo katika Vyama vya Siasa zinaweza kupata ufumbuzi. Naomba niwatakie kila la heri katika kazi yenu nzuri na muhimu. (*Makofii*)

Wageni wengine tulionao ni pamoja na Kwaya kutoka kule Kongwa wako 25; hawa ni Mtakatifu Yakobo, Kanisa Anglikana popote pale simameni mlipo. Karibuni sana. Wanaongozwa na Ndugu Nicolaus Daudi. Natumaini mmetuletea karanga za Kongwa kwa ajili ya Wabunge wote hapa. Kongwa ndiyo kuna karanga bora kabisa Tanzania nzima Waheshimiwa Wabunge, mkihitaji semeni tu, Wanakwaya wataleta. (*Makofii*)

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni familia yake kutoka Pangani Mkoa wa Tanga wakiongozwa na Ndugu Mwirwa Hemed ambaye ni bibi yake mzaa mama. Ahsante. Karibu sana pale ulipo. (*Makofii*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Wale pale, karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Victor Mwambaliaswa ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. (*Makofii*)

Wakati nikiendelea na kutaja majina ya wageni wetu, tutakapoanza uchangiaji, mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mwenyekiti Chenge, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika. Muendelee kuijandaa.

Wageni 28 wa Mheshimiwa Hassan Masala ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. Wageni 21 wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. Wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambao ni wajasiriamali kutoka Songea, karibuni sana. Wageni 27

wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni wanamaombi kutoka Dodoma, karibuni popote pale mlipo wanamaombi. Wageni 31 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni *Praise Team Jehova Mercy* ya Dodoma, Karibuni sana. (*Makofi*)

Wengine ni wageni 15 wa Mheshimiwa George Simbachawene ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi wa Kata ya Mtera, Jimbo la Kibakwe wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Kata ya Mtera, Ndugu Philipo Makalangwa, karibuni sana. Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Oscar Mukasa ambaye ni rafiki yake kutoka Dar es Salaam, Ndugu Marcus Nyanda na kuna wageni 30 na Walimu sita kutoka Chuo cha Maendeleo ya Jamii na Ujasiriamali (*DIDES*) kilichopo Nzuguni Jijini Dodoma, karibuni sana. (*Makofi*)

Lingine ni tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa imani ya Kikristo linatoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada, *Chapel* ya Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mnaombwa kuhudhuria ibada katika *Chapel* ya Bunge, Ukumbi wa Pius Msekwa, Ghorofa ya Pili leo Jumanne tarehe 8 Mei, 2018 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana. Aidha, leo kutakuwa na Mtumishi wa Mungu, Nabii Richard Magenge wa Kanisa la Yehova Mercy, Dodoma. Wote mnakaribishwa. Tuendelee na shughuli nyingine sasa.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje nimekuona. *Senator* Lubeleje siku hizi ameamua. Makatibu nitajieni majina ya wengine.

**NDG. ASIA MINJA-KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Rashid.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Amina.

**NDG. ASIA MINJA-KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Rashid na Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Hujaniona Amina Mollel.

**NDG. ASIA MINJA-KATIBU MEZANI:** Yuko wapi? Mheshimiwa Amina Mollel.

**SPIKA:** Tuanze na Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBNEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hiyo. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, Bunge letu linaendeshwa kwa sheria, kanuni, taratibu na maamuzi mengine ya Maspika waliotangulia. Sasa kumekuwa na sintofahamu ndani ya Bunge lako kwenye maamuzi mbalimbali ambayo yanafanyika humu ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo kidogo. Mheshimiwa Naibu Spika alipokaa kwenye Kiti chako aliombwa mwongozo wa namna gani nchi mbalimbali zinavyoweza kutajwa kwenye Bunge hili au kuhusishwa na mambo mbalimbali. Mheshimiwa Naibu Spika alisema kwamba tusitaje nchi wala watu ambaao hawako ndani ya Bunge ili waweze kujitetea.

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa James Mbatia aliomba mwongozo kuhusu *ratio* ya wakati wa kushika shilingi kuhusiana na vyama mbalimbali, lakini Mwenyekiti aliyekuwa anaongoza Bunge alisema hayo ni Maamuzi ya Spika na tayari yameshafanywa na mtu yeote anayetaka kupinga, apinge kupitia Kanuni ya 5(4).

Mheshimiwa Spika, sasa wewe mwenyewe uliombwa mwongozo hapa ndani na Mheshimiwa Esther Matiko juu ya uchangiaji katika bajeti hizi, ukasema unalichukua jambo hilo, unakwenda kulifanya kazi na mtaliangalia kwenye Kamati zenu za Uongozi huko ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaomba mwongozo wako, maamuzi ya Bunge ni yapi? Je, ni yale ya kwako

yanayoelekeza kwamba jambo likitokea humu ndani ya Bunge mtakwenda kukaa na kulizungumza au haya maamuzi yanayotolewa na Wenyeviti wengine? Naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, mbele yetu kuna hoja ya Wizara ya Maji ambapo hoja hiyo mwisho inataka kujadiliwa na kuungwa mkono.

Mhesimiwa Spika, katika Bunge hili kuna maamuzi ambayo yametolewa na Kiti chako. Nafahamu Kanuni kuhusu mamlaka uliyonayo katika Kiti na hatutakiwi kuyajadili na kama tunatakiwa kuyajadili tuende katika Kanuni ya 5(4) yaani Mbunge au Wabunge wamwandikie Katibu na Katibu apeleke kwa Spika na hatma yake Spika apeleke katika Kamati ya Kanuni.

Mheshimiwa Spika, Wabunge tuna mkanganyiko mkubwa kuhusu Kanuni ya 56(2) ambapo Kiti chako kimetoa maamuzi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nataka mwongozo wako kuhusu tafsiri halisi sasa ya Kanuni ya 56(2).

**SPIKA:** Hebu isome ili wasiokuwa na Kanuni wawewe kuisikia.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Kanuni ya 56(2) inasema; "Mbunge atakapoitwa na Spika kutoa hoja atasimama mahali pake na kutoa hoja yake."

Mheshimiwa Spika, 56(2) ambayo ndiyo msimamo wangu; "Hoja au marekebisho au mabadiliko ya hoja yoyote yatahitaji kuungwa mkono kwa Wabunge wasiopungua 10 na endapo haitaungwa mkono hoja au marekebisho au

mabadiliko ya hoja, yatatenguka na Katibu ataweka kumbukumbu kwenye Taarifa Rasmi kwamba kwa kuwa hoja na marekebisho au mabadiliko ya hoja hayakuungwa mkono, basi hayakujadiliwa."

**SPIKA:** Umeeleweka. Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba Rais ni taasisi, ni Amiri Jeshi Mkuu na maamuzi yake au matamko yake tayari yapo kisheria.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kama ni sahihi au mimi nakosea tunaposema, mtu mmoja tu anaamka na kutoa maamuzi, Je, ni sahihi wakati tunafahamu kwamba Rais ni taasisi, ni Amiri Jeshi Mkuu na ndio kiongozi mwenye nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako tafadhali. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel, nani kasema hivyo?

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, alisema dada yangu Susan. Kwa hiyo, nikataka tu kufahamu ili kuweka mambo sawa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo, umesikia maneno hayo? Una cha kusema?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nadhani ni kiswahili tu, sawasawa kabisa kwamba katika swali langu la nyongeza niliuliza, wakati ambapo sisi kwa mfano, Kamati ya Bunge ilitoa ushauri na baadae Mheshimiwa Rais akazungumza na kutoa tamko kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Rais ni mtu?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Sasa Rais ni mtu au taasisi? Vyovoyote vile.

Mheshimiwa Spika, Amiri Jeshi Mkuu wa nchi hii ni mtu mmoja.

**SPIKA:** Tumpe nafasi jamani ajieleze.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Sasa mimi nashangaa, kwani shida iko wapi?

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, mimi ambacho labda sijaelewa, lakini tunaposema Rais wa nchi ni mtu mmoja na ndio Amiri Jeshi Mkuu wa nchi hii. Sasa ni watu wawilli, labda mnisaidle. Nilipokuwa nazungumza nilikuwa namaanisha mtu mmoja ambaye ni Rais na ndio Amiri Jeshi Mkuu wa nchi hii.

**SPIKA:** Ahsante sana. Ahsante kwa kufafanua vizuri. Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na uhaba wa sukari, leo nimesoma gazeti kwamba kumekuwa na upungufu mkubwa wa mafuta ya kula hapa nchini na wenye viwanda wanesitisha kwa sababu ya kukosa malighafi. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji anasemaje? Kama tutakosa mafuta ya kula nchi nzima, tufanye nini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nilikuwa naraka tu mwongozo wako na nianzie alikoishia Mzee Lubeleje. Leo bei ya mafuta ya kula ya lita kumi aina ya Korie imepanda kutoka shilingi 23,000 mpaka shilingi 40,000. Mafuta ya lita 20 yamepanda kutoka shilingi 50,000 mpaka shilingi 73,000.

Mheshimiwa Spika, kama itakupendeza naomba utoe mwongozo wako kwamba Serikali pamoja na jambo la sukari ije na kauli rasmi kujua kwamba hii *crisis* ya mafuta na *crisis* ya sukari katika nchi, *what is the way forward?* Tunafanya nini kama nchi ili kuweza kumpunguzia mzigo mwananchi? Kwa sababu ongezeko hili ni zaidi ya asilimia 20 kwa kipindi cha miezi miwili/mitatu na wakati huo huo Serikali kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri jana, alisema kwamba bado upimaji unaendelea kati ya Taasisi ya TBS, Mkemia Mkuu wa Serikali na *University of Dar es Salaam.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hizi ni taasisi ambazo zinatumika na Serikali; na tulipitisha sheria ndani ya Bunge ambazo zinatumika kama vyombo rasmi kuweza kutatua majibu ya sintofahamu iliyopo katika suala la mafuta.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati huo huo Mheshimiwa Waziri hapa leo wakati anazungumzia suala la sukari, Serikali imeamua kumpa *monopoly right* mzalishaji ndio mwagizaji wa *deficit*. Kwa hiyo, wame-create ukiritimba katika bidhaa ya sukari. Sasa nilitaka tuweze kupata majibu kama Wawakilishi wa Wananchi, Serikali ije na kauli rasmi juu ya hili jambo kwa kuwa kwa miaka miwili suala la sukari limekuwa kizungumkuti. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nianze na hili tulilomalizia. Masuala ya sukari nafikiri tulishayamaliza kwamba watarudi wiki ijayo kwenye swali lingine. Kwa hiyo, tuyaweke kwa ajili ya wiki ijayo.

Hili la mafuta, naambiwa jana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, alitoa maelezo hapa Bungeni. Sasa sijui maelezo yale ya jana hayatoshelezi! Labda tumsikie tena kwa sababu ya umuhimu hasa wa takwimu ambazo wamezitoa Waheshimiwa Wabunge za ongezeko kubwa kiasi hiki kwa haraka, tuweze kujua masaa 24 inawezekana kuna mambo ambayo yametokea. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji hili la mafuta ya kula likoje hadi sasa?

### **WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kutoa ufanuzi kuhusu ongezeko la uhaba wa mafuta ya kula.

Mheshimiwa Spika, napenda watu walielewe vizuri suala hili na kama nilivyokushukuru umenipa fursa na naomba niitumie fursa hii. Tanzania tunazalisha mafuta ya kula kutokana na mbegu mbalimbali, alizeti, karanga, ufuta na mafuta ya pamba. Kiasi tunachozalisha hakikidhi mahitaji ya nchi yetu. Tunaweza kuzalisha asilimia 30 kutokana na mbegu hizo na zile asilimia 30 kwa sababu mafuta ya alizeti yana soko nje, basi kiasi kingine huuzwa nchi za nje hasa Ulaya, nchi za Sweden.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi mahitaji ya nchi hii, huagizwa mafuta kutoka nje, mafuta ghafi au yaliyosafishwa na chenyé matatizo au utata ni mafuta ghafi. Huagizwa mafuta ghafi kutoka nchi za Indonesia na Malaysia. Hayo mafuta ghafi yanapoingia hapa nchini, sheria tuliyopitisha kwa usimamizi wako ni kwamba hutozwa asilimia kumi Tanzania wakati nchi nyingine zina viwango tofauti kwa kulenga *industries* zao. Sisi tunatoza asilimia kumi wakati Kenya wanatoza asilimia sifuri tukiwa tunalenga kuwapa faida wazalishaji wa mbegu za mafuta Tanzania na viwanda vya Tanzania viweze kusimama na kuweza kushindana.

Mheshimiwa Spika, katika uagizaji, suala lilitolutetea shida sasa, mafuta takribani tani 40,000 ambayo yako ndani ya matenki na meli zile ambazo ziko nje, kilichotolutetea shida ni katika vipimo. Mafuta yaliyotoka nje, wataalam wetu walipoyapima, kuna nyaraka zinasema haya mafuta ni ghafi. Kuna nyaraka zinasema mafuta haya siyo ghafi, mafuta haya siyo safi.

Mheshimiwa Spika, sasa mtoza ushuru akawa anasimama katikati na mafuta haya yakiweza kuingia nchini tukisema ni safi, Serikali itapoteza ushuru shilingi bilioni 22. Wale wenye jukumu la kukusanya ushuru wakawa wana utata, ikaundwa Tume au Kamati ya Serikali ambayo iko kwenye mamlaka juu yangu kwamba mtuangalie, hiki ni kipi?

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie, haichukui mwaka kupima mafuta haya, ila vipimo vyta wataalam ndivyo vyenyewe vimempeleka yule mtoza ushuru au mkusanya ushuru awe na mashaka. Unapomwambia hii siyo ghafi wala siyo safi, anabaki katikati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimezungumza na wataalam wanaohusika kuhusu suala hili na kwa sababu lina *implication* kubwa, tukalipeleka kwenye mamlaka. Niliahidi jana kwamba jana na leo tungeweza kupata jibu. Nina imani watalaam wangu watakuja kwa muda waweze kusuluuhisha suala hili, lakini mimi nilishatoa ushauri kwa *TRA* ambaosasa wale wenye mafuta hawakukubaliana nao ambapo nilisema nusu ya mzigo ushushwe kwa makubaliano ya *pending easily results* za *third part* kwa hiyo, ndipo suala hilo lilipo. Tatizo linalokuja, tunahukumiwa na historia. Mtu anakuja na historia kwenye kitu hallisi.

Mheshimiwa Spika, nakushauri hii kazi unipe mimi nikawasimamie watu watalaam wangu, majibu yaje hapa, nitakuja kuripoti kwako wewe kwamba nimeona nini kabla ya saa 11.00 hatujarudi Bungeni. Ndilo suala ambalo Waheshimiwa linalotukumba. Tunalazimika kuhakikisha kila shilingi inakusanya. Sasa wale walilotumwa kukusanya, wanapoona mashaka inakuwa shida.

Mheshimiwa Spika, napenda viwanda vifanye kazi, lakini tunapaswa kufanya kazi ili watu wapate bidhaa kwa bei nafuu, ndiyo *goal*. Kwa hiyo, tunalifuatilia, mimi siku nne nafuatilia suala hili na wahusika niko nao *online*. Tunafuatilia kusudi kila upande uwe na *win win*.

Mheshimiwa Spika, nimekuomba kwamba kabla ya saa 11.00 jioni nirudi nikupe *feedback* wewe kwamba hao watu wanaofanya huu uchunguzi wamefikia wapi ili kusudi wananchi wasiumie bila sababu. Naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nalikubali hilo la saa 11.00 jioni na bahati nzuri mimi mwenyewe nitakuwa hapa.

Nawaomba tu wenzangu Serikalini, ni utamaduni duniani kote hasa Waheshimiwa Mawaziri kwamba tunapokuwa Bungeni nilazima tuseme ukweli, yaani iko hivyo. (*Makofi*)

Tukiligeuza Bunge hili pakawa ni mahali pa kubangaiza hivi haitakuwa sawa sawa. Kwa hiyo saa 11.00 jioni tuje na maelezo ya jambo hili. Kwa sababu Kamati yako Mheshimiwa Waziri, labda Mwenyekiti wa Viwanda na Biashara upo eeh? Eeh, nafikiri kuna wakati mlikuwa na watu wa *TBS* walisemaje kwa kifupi, Mheshimiwa Mwenyekiti? (*Makofi*)

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YABUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba nitoe taarifa kwamba tulikuwa na semina siku ya Jumamosi. Semina ile ilikuwa imeandaliwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, wakaja watu wa *TBS*, *FCC* na watu wa *BRELA*. Katika semina ile likajitokeza suala hili ambalo meli mbili za mafuta ghafi ziko bandarini kwa muda wa zaidi ya wiki mbili.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo na *documents* zinaonesha kwamba *TBS* wamesema yale ni mafuta ghafi, Mkemia Mkuu wa Serikali *documents* zinaonesha na amesema ni mafuta ghafi, *TRA* wanasema siyo ghafi, siyo *semi refined*, yako katikati. Tukauliza, je, *TRA* wana maabara yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuuliza vile, suala lile likanza kwenye mijadala katika makundi mbalimbali hadi likafika leo mafuta yameanza kupanda bei na viwanda vile havina tena *raw material* kwa maana ya mafuta ghafi na bei zimeendelea kupanda.

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kufanya jitihada ya kupata muafaka wa suala hili, na mimi naomba saa 11.00 jioni tupate majibu ya uhakika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nimetoa nafasi hiyo kidogo tu kuipa pitch Serikali kwamba mnatufikisha mahali pagumu sana kwa mambo madogo sana. Mambo madogo mno! Hivi kweli nchi hii leo wale wote tuliosoma *chemistry* pamoja na mimi, hivi kweli kupima mafuta kujua kama haya ni *semi refined* au *crude*, hiyo ni *rocket science*? Kitu cha dakika 15, watu wanazunguka. (*Makofi/Kicheko*)

Nilisema siku ile ya Waziri Mkuu, kama *TRA* amefika mahali hamuamini *TBS*, sasa yeye ana maabara yake? Hamuamini Mkemia Mkuu huyu *TRA*, ana maabara yake? Pelekeni South Africa, pelekeni Nairobi, pelekeni London, dakika chache majibu unapata. Unapiga kodi, suala limeisha. (*Makofi*)

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Spika leo ameamka salama. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mungu akubariki. Spika unatosha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tukitengeneza mazingira ya *TRA* ya mbabe mmoja anakaa anasema mimi, haiwezi kuwa hivyo! Kama ni *semi refined*, ipigwe kodi ya *semi refined*, kama ni *crude* ni *crude*. Sasa ubishi wa nini? Hakuna sababu ya ubishi.

Kwa hiyo, tunategemea Serikali itakapokuja saa 11.00 kwa kweli iwe na majibu. Tunaumiza wananchi. Hata hayo mafuta yanayozidi kukaa huko bandarini yatakapoingia, atakayelipia hizo gharama zote ni mwananchi mlaji. Eeh, ndio atakayeumia. Wala siyo hao matajiri ambao sisi tunalumbana hapa, eeh, kaa huko, tunaunda Kamati. Atakayeumia ni mlaji, ndiyo gharama zile atapakuliwa zote hizo. Kama mlivyosema tunakwenda mwezi wa Ramadhani sidhani kama kuna nia; Mheshimiwa Waziri hebu kaeni mlimalize hili jambo. (*Makofi*)

Yale mengine yote tumeyachukua, tutayafanyia kazi. Katibu. (*Makofi*)

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali  
Wizara ya Maji na Umwagiliaji 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea. Nilisema mchangiaji wa kwanza Mheshimiwa Chenge, atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya asubuhi hii niseme kwa kufupi. Nampogeza sana Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Isack Kamwelwe na Naibu wake Mheshimwa Aweso.

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii Profesa Kitila Mkumbo, Naibu Katibu Mkuu *Engineer* Kalobel, watendaji wote na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kufanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri, imebeba matumaini kwa Watanzania kwenye sekta hii muhimu. Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni, lakini haki mpeni. Naamini Wizara hii ingeweza kufanya mambo makubwa, lakini *limitation* ya rasilimali fedha, hiyo ndiyo tunaiona sote. Tunawapongeza kwa haya, hata kwa ile pesa kidogo ambayo wameweza kupewa, mnaona matokeo kwa kazi waliyofanya kwa mwaka huu tunaomaliza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali, maana ukilinganisha bajeti ya mwaka 2017/2018 ambao tunaumaliza, kwa upande wa fedha za maendeleo mwaka huu Serikali tofauti na mwaka 2017/2018 ambapo sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo ilikuwa ya kutoka nje, safari

hii bajeti ya maendeleo ni fedha zetu za ndani. Naipongeza sana Serikali kwa hilo na tuendelee hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ila tu kwenye Fungu Na. 05 kwa upande wa umwagiliaji, bado sehemu kubwa ya fedha za kutoka nje. Nadhani kama tunataka tufikie malengo letu ambayo mpaka sasa tuko nyuma sana, maana tulikuwa tumepanga ifikapo mwaka 2015 tuwe tumekuwa na ekari milioni moja za umwagiliaji wala hatujafika huko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaiona hali hii, lakini hata kwako hapo, mimi huwa napita na Waheshimiwa Wabunge wote tunapita sehemu ya Itanana pale au Kibaigwa hapo, kipindi cha masika hayo maji tungeweza kuyavuna tukafanya mambo makubwa. Siyo mbali, hapo kwenye Jimbo lako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo niseme mambo ya Bariadi. Naishukuru sana Serikali, naona mradi wa kutoka Ziwa Victoria kupeleka Mkoa wa Simiyu, mradi mkubwa wa kitaifa unatoa matumaini. Nimeaangalia kitabu cha *Volume I*/Vsion mradi huo, ila kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye *schedule* ukurasa 198 naona zipo shilingi bilioni 15. Sasa napenda Mheshimiwa Waziri anapokuja ku-wind-up hoja yake hili suala tulielewe sote vizuri, kwa sababu haiwezekani tukapitisha mradi huo lakini kwenye eneo la pesa za maendeleo hazionekani. Yawezekana labda zimewekwa kwenye fungu lingine, sitaki kuwasemea lakini watanisaidia kulielewa hili.

Mheshimiwa Spika, tuwape wananchi wa Simiyu matumaini ya kupata maji salama ya uhakika. Sisi tuna shida sana ya maji, lakini kwa mradi huu naona tunaenda vizuri. Wananchi wa Busega, wananchi wa Bariadi, wananchi wa Itilima, wananchi wa Meatu na wananchi wa Maswa, mradi huu utatuleta manufaa makubwa sana kwa maendeleo yetu. Tuombe tu kwamba utekelezwe kwa haraka, usanifu huu ukamilike mwezi huu na kweli tuanze kazi ya kuandaa zabuni ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, la pili, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji tulianzisha zaidi ya miaka saba iliyopita, lakini napenda sasa Serikali iende na wakati. Tulanza na Wajumbe wanne; Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Mjumbe mmoja anatoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Jamani tunataka Mfuko huu uwe ndiyo *engine* ya maendeleo katika kusukuma miradi ya maji. Naomba basi tupanue sura ya uwakilishi kwenye bodi hiyo, isiendelee kukaa kama kitengo cha Wizara. Tunataka isimame iwe na *CO* wake, Sekretarieti yake, Meneja wa Mfuko, wasimamie shughuli hii. Naomba sana Serikali walione hilo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, lingine ni la skimu za umwagiliaji. Mwaka 2016 Serikali ilitaja kwenye bajeti yake, kulikuwa na mabwawa kama kumi na bwawa moja lilikuwa katika Jimbo langu la Bariadi, Bwawa la Kasoli. Sasa hapa katikati silioni tena. Mheshimiwa Waziri silioni Bwawa la Kasori, nimeangalia humu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeona Skimu ya Umwagiliaji ya Mwasibuya inaenda vizuri. Naishukuru Serikali kwa mipango hiyo na pesa ambayo nimeiona humo. Napenda kama siyo mwaka kesho tuweke Bwawa la Kasoli lakini pia na eneo la Ikungulyambesha, mbona Wajapani walikuja wakaangalia eneo hilo, lakini kwa sababu ya tatizo la usanifu haikuwa imekaa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (*BARUWASA*) Bariadi. Sijui tumekosea nini, hii ni *class*. Daraja la Tatu, Mamlaka hii ya *BARUWASA* ni *class three*. Kwa mujibu wa kanuni zetu, unapokuwa kwenye ngazi hiyo wewe unstahili kupewa na Serikali kuititia Wizara, ruzuku ya kulipia umeme wa *TANESCO* wa kuendesha hizi *pump* za kuzalisha maji. Sisi hatupewi, tumekosea nini nauliza?

Mheshimiwa Spika, napenda sana Mheshimiwa Waziri hili utusaidie utupatie majibu ambayo yatawapatia wananchi wa Bariadi matumaini. Tuna shida ya maji, kama yalivyo maeneo mengi ya nchi hii. Siwezi kuwa mchoyo, lakini kile

ambacho tunakipata tunataka rasilimali fedha hiyo itumike vizuri. Naelewa maeneo yetu mengi tuna tatizo la *absorption capacity*. Naiomba sana Serikali tuangalie watalaam wetu, tuwagawe katika njia ambao itawezesha Halmashauri zetu nyingi kunufaika na rasilimali fedha hizi ambazo zinatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nisingelipenda kupigiwa kengele ya pili; naipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayofanya. Tuendelee kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa John John Mnyika atafuatiwa na Mheshimiwa Lusinde na Mheshimiwa Selemani Bungara ajandae.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Toka jana nimekuwa nikisikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na leo na nimepitia taarifa ya Kamati na nimetafakari katika miaka niliyokaa Bungeni, nimekuja kugundua kwamba kwa miaka nane kwa kweli Bunge hili linajadili mambo yale yale, yaani ukiwa umeingia Bungeni leo tu au jana ukawa hujasikiliza Bunge huko nyuma, unaweza kufikiri sasa kuna Chama na Serikali mpya katika Bunge hili inajaribu kurekebisha mambo ya zamani. Kumbe ni chama kile kile na Serikali ile ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sentensi moja ambayo iko bayana katika haya ni kwamba ninyi mmeshindwa kutekeleza na kutimiza matakwa ya wananchi kwenye masuala ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kabla sijaendelea mbele nisisitize ninachoendelea kusitiza kwamba tiba ya kudumu ya haya matatizo tuliyonayo ni wananchi wa Tanzania kuwaondoa Serikali ya CCM madarakani na kuweka Serikali nyingine katika utawala wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wewe utakuwa unakumbuka vizuri kwa sababu ulikuwa kwenye kiti hicho hicho wakati ukiwa Naibu Spika. Tarehe 4 Februari, 2013 nilipoleta hoja Bungeni hapa juu ya maji Dar es Salaam na maji vijijini na namna ambavyo Wabunge wa CCM wakati huo Mheshimiwa Rais akiwa ndani ya Bunge, akiwa Waziri wa Ujenzi naye akisikiliza mlivyoshabikia kwa pamoja kwamba mambo yapo kwenye mkondo sahihi, kila kitu kipo sawasawa, hoja hii iondolewe isijadiliwe, hatimaye maji yakasababisha vurugu kubwa sana hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu au miwili na ushee, toka mwaka 2016 hadi 2017 na mpaka sasa mlinyamaza kimya kusema kuhusu maji, nikifikiri kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa sababu alikuwa Mbunge anayajua vizuri matatizo haya ya maji na kwa sababu alikuja hapa Bungeni akaahidi kwamba ifikapo mwaka 2020 asilimia 95 ya wananchi mijini ikiwemo Dar es Salaam watakuwa na maji na asilimia 85 wa vijijini watakuwa na maji, nikifikiri kwamba kutakuwa na tofauti. Nimekuja kugundua kwamba Mheshimiwa Magufuli ni yule yule na CCM ni ile ile, mambo ni yale yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa huwa tunajengewa matumaini sana. Mwaka 2006, mwaka 2007 katika Bunge la Bajeti Waheshimwia Wabunge walisema mambo haya haya ambayo wanasema sasa tukajengewa matumaini wakati wa majumuisho ya Serikali kwamba kutakuwa na mabadiliko. Safari hii mmekuja na mkakati huo huo; na sasa kuna *debate* ya tozo ya mafuta ya shilingi 50 ili ikishafika hatua ya majumuisho Serikali iki-*coincide*kutoa tozo ya shilingi 50 watu walainike wote, bajeti ipite, halafu mambo yaendelee kuwa yale yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inasema mpaka mwezi Machi Serikali imetoa asilimia 22 tu ya pesa za maendeleo. Hizi asilimia 22 za pesa maendeleo ni katika bajeti ya maji ambayo imepunguzwa badala ya kuingezwa kutoka bajeti iliyo tangulia. Halafu kwenye umwagiliaji hali ni mbaya zaidi asiliamia 12 na kati ya hiyo 12 pesa za ndani ni 0.8. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika suala la sukari ulisimama ukataka kuonesha ukali. Maji katika maisha ya wananchi ni zaidi ya sukari kwa sababu ukikosa sukari unaweza ukanywa chai bila sukari. Katika suala la mafuta umeonesha ukali, maji ni zaidi ya mafuta, kwa sababu ukikosa mafuta unaweza ukapika bila ya mafuta. Ila ukikosa maji huwezi kunywa bia, ukikosa maji huwezi..., ni uhai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, onesha ukali wako katika hili. Na mimi nakuomba ukubali, kwa sababu tumeishauri Serikali vya kutosha sana, lakinii haisikii. Sasa nani wakati Bunge kutumia mamlaka yake ya Kikatiba kusimamia Serikali. Mamlaka hayo yanaanza kwa kukubaliana kwamba hii bajeti ya Wizara ya Maji tusiipitishe sasa. Tukubaliane kwamba hii bajeti ya Wizara ya Maji tusiipitishe sasa. Sasa najua kwamba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wana shauku sana ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa siyo shauku ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ningesema nasimama sasa hivi kwa mujibu wa Kanuni ya 69(1) ambayo inaruhusu Mbunge kusimama wakati wowote kutoa hoja ya kwamba mjadala uahirishwe. Ningeweza kabisa kusema kwamba mjadala uahirishwe, sasa ni mwezi Mei na kuna bajeti zinajadiliwa mpaka mwanzoni mwa mwezi Juni, tungesema mjadala uahirishwe mpaka mwishoni mwa Mei ili Serikali katika makusanyo yake ya mwezi huu wa Serikali iingize pesa katika Wizara ya Maji, tuvuke kutoka hii asilimia 22, tufike juu ya asilimia 22.

Mheshimiwa Spika, tuna uwezo kabisa wa kufanya hivyo kwa kanuni za Bunge na tuna haki hiyo. Kwa sababu Waheshimiwia Wabunge wenzangu wana shauku ya kuendelea kuchangia, bado tunayo nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ruhusu Wabunge wengine waendelee kuchangia lakini wakishamaliza kuchangia kesho, Serikali isiruhusiwe kuhitimisha, mjadala uahirishwe na nipewe nafasi ya kutoa hoja hiyo kesho, mjadala uahirishwe mpaka tarehe ngapi kwa mujibu wa kanuni. (*Makofii*)

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Spika taarifa. Maulid Mtulia.

## T A A R I F A

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika kuna sauti naisikia. Ahsante Mtulia.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakiri hadharani kwamba mzungumzaji namheshimu sana na Mbunge mwenzangu wa Dar es Salaam, lakini pia ni Kiongozi wa Chama mkubwa sana. Nampa taarifa na ninakubaliana naye kwamba ni kweli Serikali imechangia siyo zaidi ya asilimia 20 lakini nampa taarifa kwamba katika zile tozo zetu shilingi 50 tulizopitisha mwaka 2017, pesa hizo zimesaidia sana na zimefikia zaidi ya asilimia 80. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sasa kwamba badala ya kuilazimisha Serikali imalizie zile pesa ndiyo maana tukaja na njia mbadala kuongeza shilingi 50 nyingine tukitegemea 80 ile na tukipata 80 nyingine, mipango yetu ya maji itakwenda vizuri na Ubungo maji yatapatikana.

Kwa hiyo, hakuna haja ya kuahirisha mjadala huu, badala yake tupitishe ile shilingi 50 ambayo watu wengi wanaiomba ili kuja kutatua tatizo hili. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Taarifa hiyo, Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA.** Mheshimiwa Spika, nilisema awali kwamba ni mbinu tu ya kukwepesha hii bajeti ipite.

Mheshimiwa Spika, tulishapitisha bajeti hii ambayo Serikali imetoa asilimia 22. Serikali ikishapitisha Bajeti ni wajibu wa Serikali kutoa pesa. Nasema tuahirishe mjadala ili Serikali ilazimishwe kutoa hizo pesa. Sasa masuala ya tozo ni masuala ya kwamba tunakwendaje mbele? Tukifika huko napo hata katika tozo, kuna tozo zinatozwa na bado pesa nyingine haziendi vilevile. Kama ilivyo kwenye maji, kama ilivyo kwenye umeme, kwenye REA, hiyo ni jambo lingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niendelee, Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wameeleza na kwa miaka kadhaa tumeeleza kuhusu ujisadi katika sekta ya maji na miradi ya ambayo kimsingi ni miradi ambayo imejengwa lakini maji hayatoki na matumizi mabaya ya fedha katika masuala ya miradi ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hali hii imeendelea, ipo katika sura nydingi hata mtu akisoma kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri, ukiangalia tu uchimbaji wa visima vya DCCA kuanzia ukurasa wa 267 utaona jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri anavyojipendelea katika Mkoa wa Katavi na katika Jimbo lake. Mimi nazungumzia kipengele cha matumizi mabaya ya fedha za miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ya nchini na miradi ya maji kutokufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya kero nydingi za ujisadi wa namna hii unaozungumzwa, nitaomba nafasi na ninaomba nitoe *notice* kabisa kwa mujibu wa Kanuni ya 120 ya Kanuni za Bunge 2A kwamba baada ya mjadala huu kukamilika, nipewe nafasi ya kutoa hoja ya kuundwa kwa Kamati teule ya kwenda kuchunguza masuala ya ujisadi na miradi mibovu katika masula ya maji maeneo yote nchini na katika maeneo mbalimbali nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wewe umeonesha kutaka kuunda Kamati za kiuchunguzi, umeunda Kamati ya Gesi, umeunda Kamati ya Tanzanite, umeunda Kamati ya Almasi na umeunda Kamati mbalimbali, lakini hizi Kamati zako ambazo taarifa zake hazijadili humu Bungeni na Wabunge wote, sasa katika hilli kwa sababu ya uzito wake iilundwe Kamati Teule ili ikachunguze na taarifa iletwe Bungeni ijadiliwe na hatua zichukuliwe. Ahsante sana. (*Makofii/Vigelegele*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Mnyika. Mheshimiwa Livingstone Lusinde. (*Makofii*)

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kupata nafasi asubuhi hii ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya Maji ambayo nyeti na muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtera niweze kueleza machache kwa ajili ya Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Spika, ni maneno mazuri sana yanazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge tangu jana mpaka asubuhi hii na wengine wanashauri sasa Serikali hii itolewe ingiziwe Serikali ambayo hamna kitu wala ofisi haina, halafu ilete maji. Vitu vya ajabu sana! Hata aliyeanzisha benki alihakikisha jengo zuri, imara, wahudumu wazuri ili kuweka imani ya watu kuweka hela zao. Lakini hiyo benki nyingine mtu aende akaweke huko, benki ya makuti, ofisi hakuna, matete, haiwezekani. Nadhani alikuwa anajifurahisha, haiwezekani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo, kama alivyotoa utangulizi aliyezungumza, na mimi naingia kwenye Wizara ya Maji. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, wanafanya kazi nzuri. Hata katika umri alionao *Engineer* tunamwona namna anavyohangaika kwenye Majimbo na mpaka Mheshimiwa Aweso anazidi kutoka kipara kwa kujitwisha ndoo za maji, pamoja na Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Maji ni Wizara muhimu sana na kama ikifanikiwa, kwa kiasi kikubwa itapunguza bajeti za Wizara nyingine, maana Wizara hii ni mtambuka, inaweza kusaidia Wizara ya Afya, inaweza kusaidia hata ongezeko la watu mijini. Hivi kwa sisi Wabunge wa vijijini, kwenye vijiji kule hakuna maji, hakuna barabara, hakuna afya, watu wataachaje kuja mjini kuzifuata huduma hizo?

Kwa hiyo, Wizara hii ikiweza kufanya kazi zake sawa sawa, watu wakapata maji safi na salama, baadhi ya magonjwa kama ya matumbo yanafutika kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka niishauri Serikali, wakati mwagine ijifunze kuitia vitu vidogo. Nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru sana watu wa *WFP* chini ya uongozi wa dada Neema Sitta kwa kazi nzuri waliyoifanya kwenye Jimbo la Mtera.

Mheshimiwa Spika, hapa Mheshimiwa Waziri akinisikiliza vizuri, anaweza kuona namna ambavyo Serikali wakati mwagine inashindwa kusimamia matumizi mazuri tu. Ikisimamia matumizi mazuri, *value for money* ikazingatiwa, tutapata maji mengi na kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano watu wa *WFP* wametupa shilingi milioni 799 kwenye Jimbo la Mtera. Katika milioni hizo hizo 799 tumepata matenki makubwa matatu ya lita 800,000, tumepata visima 18, tumepata mashamba heka 300 kwa ajili ya umwagiliaji, tumepata visima 12 vilivyofungwa *solar power* kwa ajili ya wananchi kupata maji.

Mheshimiwa Spika, hebu angalia matumizi haya ya shilingi milioni 800 tu hizi kasoro moja yameweza kuleta vitu hivyo vikubwa ambavyo wananchi leo hii wananaufaika. Ukija kwenye Serikali, hamna kitu. Inatolewa shilingi bilioni moja pale Mkwayungu kwa ajili ya kujenga bwawa la umwagiliaji, bwawa halijakamiliaka, hakuna miundombinu na shilingi bilioni moja imeliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona matumizi mabaya kwenye miradi ya maji kwa upande wa Serikali yanatuletea matatizo makubwa. Hawa wameweza kutoa shilingi milioni 800 zimetengeneza mambo ambayo ni maajabu kabisa. Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu na Naibu Waziri piteni mwone kwa macho namna ambavyo pesa ikisimamiwa hata ikiwa kidogo inaweza kufanya vitu vikubwa.

Mheshimiwa Spika, watu wamepata maji ya kunywa, wamepata *irrigation* wanamwagilia na maisha yao yako safi. Ukienda kwenye Kata ya Fufu katika Vijiji vya Suri, Chibori na Fufu yenyewe, *WFP* wametufanya mambo makubwa kwa pesa kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukienda mahali pengi kwenye miradi ya Serikali, hela nyigi zimetumika, zaidi ya shilingi bilioni moja imeliwa pale Mkwayungu na maji hakuna. Kwa hiyo, nakuomba sana, hebu twende tuangalie wenzetu hawa wamewezaje? Wamefanikiwaje? Wamefunga *solar system* katika visima vyote. Hakuna mwananchi anayehangaika kutafuta *bill* ya umeme, kutafuta nini na pampu za kisasa, zinazomwagilia mashamba kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, tumepata Makao Makuu ya Nchi, haitakuwa na maana kama Mkoaa wa Dodoma hautakuwa *scheme* za umwagiliaji. Vijana wakiweza kumwagilia huko kwenye Majimbo ya vijiji ni waleta bidhaa zao hapa mjini, zitakuja kuwanufaisha na wao na watoto wao. (*Makofî*)

Msheshimiwa Spika, Wizara ya Maji ikijitahidi kusimamia *resource* kidogo iliyopo, nina uhakika inaweza kutosha kutusukuma mbele. Kwa mfano, nimekuja hapa kuomba maji kwa ajili ya vijiji vyangu; Kijiji cha Loji hakina maji, Kijiji cha Ng'aheleze hakina maji, kijiji cha Handali hakina maji. Hivi ni vijiji vikubwa mnoo! Kijiji cha Ng'ng'i leo hii kina wakazi karibu 8,000 lakini hakina maji ya uhakika. Halafu Halmashauri baadhi ya visima vya zamani vikiharibika vinashindwa kuvitengeneza. Kwa hiyo, utakuta kuna matatizo ya visima vya zamani na kuna matatizo ya visima vipyta, havipatikani.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kujibu, atupatie maji katika Jimbo la Mtera na atupatie maji katika Kijiji cha Muheme.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

## TAARIFA

**SPIKA:** Mimi naomba kwa leo kwa kweli taarifa ziwe ni sahihi. Tuache utani utani ule. Simaanishi unatania, natoa tahadhari kwa wote tu kwamba leo mimi nitaruhusu taarifa lakini ziwe taarifa kweli. Karibu Mheshimiwa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji na pia nirejee maneno yako uliyoyasema, ni kweli tuwe na taarifa ambazo ziko sahihi.

Nilikuwa nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Lusinde pale kwamba hata ungekuwa na majengo makubwa, maghorofa mengi na ungekuwa na ofisi kubwa, lakini kama huna dhamira ya kweli, leo wanamlalamika kwamba fedha za umma zinalika, kwa hiyo, fedha zinaweza zikalika tu, kama anavyolalamika kuhusu miradi yake ya huko Mtera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ofisi tunayo na kama fedha hizo anazungumzia kuhusiana na mambo ya kutunza fedha, tuna uwezo na ndiyo maana tuko hapa tunaishauri Serikali ili miradi na fedha zote zinazokwenda kwenye miradi ziweze kufanya kazi vizuri. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kumbe Mheshimiwa lilikuwa bado linakooma, linakukereketa tu tangu saa zile. Mheshimiwa Lusinde, taarifa hiyo bwana. (*Kicheko*)

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, taarifa yake wala siwezi kuikataa, naipokea. Naipokea kwa maana ya kwamba akasimamie na pesa alizosema CAG zimeliwa kwenye chama chake, kama anao uwezo huo akasimamie ili ziweze kuleta maendeleo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilijua tu, ukisikia kelele ujue tayari tiba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mkoa wa Dodoma ambao hamna mito inayotiririka maji kwa msimu mzima, uangaliwe kwa makini hususan katika uchimbaji wa mabwawa. Sisi maji yetu yanapita tu, mvua ikinyesha, yanapita yanaondoka moja kwa moja. Hatuna mito inayotiririsha maji msimu mzima. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara ilitazame hilo kama eneo mahususi tukipata mabwawa ya kutosha, tuna uwezo mkubwa sana wa kuzalisha, tuna uwezo

mkubwa sana kwa kulima kilimo cha kisasa, tuna uwezo mkubwa sana wa kujisimamia. Tunachotaka Serikali mtuangalie muwe mnafanya *research* basi, kuna Mkoa huu tofauti yake na Mkoa huu.

Mheshimiwa Spika, *WFP* wameleta hela kidogo lakini zimefanya mambo makubwa, zimejenga mpaka matanki ya maji ya shule za msingi, hela kidogo hii! Ndiyo maana namwomba Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu na Naibu Waziri watembelee wakaone, siyo vibaya kuona kwa macho na kuja kusimamia pesa zenu mizonazo ili ziweze kutusogezza mbele. Hata mabwawa ya zamani yaliyochimbwa enzi za Mwalimu Nyerere, leo hii yapo; mengine yameshajifukia. Liko bwawa la Mkulabi hapa Dodoma Mjini, lipo Bwawa Mlowa Bwawani pale. Mwalimu alichimba mabwawa makubwa lakini leo hii hayana maana yoyote.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana atakaposimama Mheshimiwa Waziri atusaidie sana kupata maji katika vijiji nilivyovitaja vya Jimbo la Mtera na kuhakikisha kwamba tunapata kilimo cha umwagiliaji. Mbona nimewaomba sana kwenda Mkwayungu kuona ule mradi ambaa Serikali imetumbukiza shilingi bilioni moja, lakini hamna kitu chochote? Mbona hamuendi? Twendeni mkaone kwa macho ili mfananishe yale yaliyofanyika pale Mkwayungu na ambayo wenzenu wanaweza kufanya.

Mheshimiwa Spika, tukifanya namna hiyo tutakuwa tunazuia ulaji, tutakuwa tunazuia wizi na umangimeza na nina uhakika Serikali ya Awamu ya Tano itazuia mambo hayo na ndiyo maana nawasihi mfike mwone ufisadi uliofanyika, mchukue hatua ili wananchi wa Kijiji cha Mkwayungu waweez kupata maendeleo kwa kilimo cha umwagiliaji ambacho kilikusudiwa kufanyika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri mnayoifanya. Wizara hii lazima iwe na kelele kwa sababu maji ni muhimu sana. Tunataka kuwatua ndoo kichwani akina mama. Tusiwatue wa mijini tu, hebu

tazameni na Majimbo ya vijjini jamani. Vijjini nako kuna akina mama wengi wanaoteseka, wanatoa maji mbali, wanachelewa kufanya kazi zao za kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anafanya ziara mwenyewe anakutana na hiyo hali, tusaidieni na sisi Wabunge wa vijjini. Hawa wa mjini ambao wana lami, wana hospitali nzuri na nini, nao kwa maji wangesubiri kidogo, geukieni upande mwininge.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante na ninaunga mokono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Lusinde. Nikwambie tu mdogo wangu, mjini watu wakitoka *salon* hawaweki ndoo kichwani hata siku moja. Wanaoweka ndoo kichwani ni kijjini kule ambako hawaendi *salon*. Tunakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri kama alivyosema Mheshimiwa Lusinde, fedha za maji ni nyingi, tatizo lake *ownership* ya kwenye Halmashauri kule, Madiwani na nani hatuna. Ni fedha ambazo ma-*consultant* na makandarasi na ma-*engineer* wenu wamesha-*design* kijjji kimoja shilingi milioni 700 au shilingi milioni 800 kijjji kimoja. Kijjji kimoja mabomba yanayotandikwa kilometra 20 hadi kilometra 30, urefu wa mabomba *twenty kilometers*. Nani anahitaji mabomba marefu namna hiyo? Kutoka kwenye chanzo mpaka kwenye tanki, kilometra tano. Yakiwekwa mabomba *fake* hapo, yanapiga mizinga humo katikati, mkishatoka tu, ule mradi ni *white elephant*. (*Makofii*)

Nani atakarabati mradi wa kilometra kwa kilometra mabomba yamepasuka? Sisi hapa Dodoma hatuhitaji. Tunahitaji chanzo kimoja au viwili kwa kijjji, ambapo hiyo shilingi milioni 700 au 800 uliyotumbukiza hapo ungetumia shilingi milioni 100 imetosha. Hizo nyingine zote, mkikaa na sisi wenyewe kule tukawaambia tunahitaji nini, tutaokoa fedha nyingi sana na tutafanya kitu ambacho kwa kweli ni kizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Selemani Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi. Leo nakuona kabisa kama Spika kweli kweli! Uko *strong*, hongera sana. (*Makofii*)

Msheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi leo na mimi niseme kuhusu habari ya maji. Pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji. Tulikuwa tunadai hela tangu mwaka 1992, wananchi wangu walitoa eneo, walikuwa hawajalipwa, lakini kwa Waziri huyu aliyejukua, nilipomwandikia barua moja tu, basi *Alhamdulillah* vijana wangu wamelipwa hela zao zote. Namshukuru Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasema kila siku, tatizo siyo Mawaziri, hakuna Waziri mzigo katika Serikali ya CCM, hakuna! Tena nampongeza Waziri wa Kilimo vilevile vijana wangu walikuwa wanadai, wamellipwa. Naomba sana, Mawaziri hamna makosa, tatizo ni Serikali ya CCM. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilisema siku moja na wakati huo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Waziri wa Ujenzi ndani ya Bunge hili. Nilimwambia Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwamba wewe sio mzigo, mzigo ni Serikali ya CCM. Nikisema hivyo, leo tunasema asilimia 22 ya miradi ya maendeleo ya maji ndiyo imetolewa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Bungara, nimesikia Taarifa huku.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Masikio yangu tu eeh! (*Kicheko*)

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Ah, kama ama...!  
(*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Bungara endelea.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, kama kuna taarifa, nikae chini nisikilize hiyo taarifa.

## **MBUNGE FULANI:** Endelea bwana!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, afanye nini Waziri wa Maji wakati asilimia 22 ndiyo aliyopata na asilimia 78 hajapata? Mheshimiwa Waziri tumlaumu wapi? Na sisi ndiyo maana ikija hapa bajeti, tunasema hapana! Siyo hapana hatutaki bajeti ipite, tunasema hapana kwa sababu tunajua ninyi hamuwezi kutekeleza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tunasema hapana tunajua tunachokisema ndiyo, hakiwi ndiyo. Kwa hiyo, tunasema hapana kwa sababu tunataka hapana yetu iwe ndiyo, ninyi m jitahidi sasa mseme kwa kuwa Wapinzani wanasesma hapana, tufanye mambo haya tuwaone kwamba Wapinzani kama wana..., yale yale, asilimia 22! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Serikali ya CCM pelekeni fedha katika miradi ya maendeleo. Mkipeleka fedha katika miradi ya maendeleo, sisi tutasema ndiyo. Kama hampeleki fedha, tutasema hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunasema hapana kwa sababu tunajua mnachokisema sicho mnachokitenda. Hii nasema tena, hivi leo mwananchi umuulize ndege na maji nini kianze? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninyi Waheshimiwa Wabunge kama kweli kabisa mnawaonea wananchi huruma, tuwaulize kweli Waheshimiwa Wabunge wa CCM, kununua ndege na kuwapa watu maji, bora nini? Hapa tuseme sasa, wanaosema inunuliwe ndege msimame juu, halafu wananchi wawaone. Halafu wanaosema tuanze maji, wasimame juu halafu tuone kama mtarudi ninyi, mimi sio Bwege. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakuomba uulize swali hilo, wanaosema ndege inunuliwe wasimame, halafu wanaosema maji yawepo tusimame, halafu tukaoneshe Watanzania huko, he, he, he! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, utaruhusu kidogo tusimame? Naomba sana tuwajali watu wetu, hamna Waziri mbaya, hayupo. Waziri ni Mbunge na anajua matatizo ya wananchi, lakini Serikali ya CCM ni mzigo. Simsemi Mheshimiwa Dkt. Magufuli, ah, ah, Serikali ya CCM ni mzigo. Sio Mheshimiwa Dkt. Magufuli! Mheshimiwa Dkt. Magufuli sio mzigo, Serikali ya CCM ni mzigo. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba sana sisi tuna matatizo ya maji katika Mji wa asili wa Kilwa Kivinje, mji mdogo tu wa Kivinje. Mwaka 1980 Mji wa Kivinje tulikuwa tuna mabomba yetu, tunafungua maji, tuliyarithi kwa mkoloni. Leo Kilwa Kivinje kuna Hospitali ya Wilaya. Ndani ya Hospitali ya Wilaya hakuna maji na nilisema siku moja hapa kwamba Hospitali ya Wilaya ya Kilwa Kivinje hakuna maji. Akasimama Mheshimiwa Mkuchika wakachukua matenki ya maji wakaweka hospitalini, wakafungua wakasema Bwege muongo, maji yanafunguka haya. Kumbe wamechukua maji Nangurukuru. (*Makof*)

Tunaomba sana, Mji wa Kilwa Kivinje, Mheshimiwa Mkuchika anajua hilo. Wakanisololea sana hapa, lakini Mji wa Kilwa Kivinje hakuna maji. Hospitali ya Wilaya iko Kivinje, watu wanununa maji shilingi 1,000 wanapeleka hospitali. Hospitali ya Wilaya, halafu ninyi mnanunua ndege maskini. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri, Hospitali ya Wilaya ipate maji na Mji wa Kivinje na Mji Mdogo wa Kivinje upate maji. Kuna vitongoji saba Nangurukuru, Matandu, Singino, Mgongeni, Magengeni, Mayungiyungi, Kisangi Mjini, Kisangi Shamba, vyote havina maji. Tunaomba sana tupate maji. Kuna vijiji havijapata maji vingi tu, Vimaliao, Pande, Kikole, Luatwe na Nanjilinji hakuna maji. Miaka 57 ya CCM tunaongelea habari ya maji wakati ndiyo nchi ya nne kuwa na maji duniani, lakini hakuna. Hohaa! Serikali ya CCM, amkeni! Hohaa! (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hakuna maji, na nimesema hapa Bunge liliopita, kama hatupati maji mwaka 2020 CCM

kwaheri, *bye, bye*, Waheshimiwa! Maji ni uhai, leo mashehe wetu wako Magereza huko, Magereza hakuna maji, na sisi hatuwezi kuswali bila maji. Lazima tutie udhu, tupate maji. Mashehe wako Magereza ya Segerea, maji hakuna. Hawaswali, hawafanyi chochote huko.

Mheshimiwa Spika, tunawaambia kila binadamu kaumbwa na maji, maji ni uhai. Nakusifu sana Waziri wa Maji, namsifu sana Katibu wa Wizara ya Maji Mheshimiwa Kitila Mkumbo, alikuwa huku huku na sijui ilikuwajekuwaje, alikuwa huku huku kwetu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana tuuze ndege mbili tutatue tatizo la maji. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Bungara. Nakushukuru sana.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Ndiyo. Sijamaliza, kengele haijalia.

**SPIKA:** Tayari dakika zako zimeisha.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, basi kwa kuwa leo uko vizuri, hebu piga kura, wanaotaka ndege na maji wengi nani? Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Bungara. Tunakushukuru sana kwa mchango wako. Maneno mengine jamani tunaambiwa ukweli tu, kwa sababu hata tukimlaumu Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, tutakuwa tunawaonea tu. Maana ukiacha ule Mfuko wa Maji, Serikali imetoa asilimia 11 tu ya vyanzo vya ndani kwa Wizara hii. (*Makofi*)

Kwa hiyo, *actually* kwa sababu tu watu wa Wizara ya Fedha hawapo hapa, lakini tukiwapata mpaka kesho itabidi wasimame hapa watuambie hivi sasa watafanyaje? Mtasimama mtawalaumu. Hivi hata ungekuwa wewe ndio Waziri ungefanyaje sasa kama hela hukupata? (*Makofi*)

Mheshimiwa Khadija Aboud na Mheshimiwa Dunstan Kitandula. Karibu Mheshimiwa Khadija, Mheshimiwa Kitandula ajlandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa jitihada zake zote inazofanya kuwasaidia wananchi wa Tanzania katika kuwalettea maendeleo na pia kuwasaidia kupata huduma muhimu ikiwemo ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naanza na Mfuko wa Maji ambao ni chanzo muhimu sana cha upatikanaji wa fedha za kusaidia maendeleo ya maji na tumeona ufanisi wake kwa kipindi hiki kwa kufanyiwa mpango na Serikali kutoza tozo ya shilingi 50 kwa kila lita. Ombi langu kwa Serikali, tuongeze tena shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli ili kuufanya mfuko huu ukusanye jumla ya shilingi bilioni 316, fedha hizi zikipatikana zitasaidia sana miradi ya maji vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taasisi za maji au Mamlaka za Maji zinakabiliwa na madeni makubwa ya maji kwa takribani shillingi bilioni 38. Naishauri Serikali ili Mamlaka za Maji ziweze kuijendesha na kuongeza huduma za maji kwa wananchi, madeni haya yalipwe kwa haraka ili mamlaka zetu ziweze kuijendesha na kutanua huduma za maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Maji kwa kuanzisha *prepaid meter* ambazo zitasaidia sasa, wale wadaiwa sugu wa maji watakuwa hawana tena njia ya kukwepa kulipa madeni hayo. Namshauri Mheshimiwa Waziri, hizi *prepaid meter* watakapozifunga, wazianzishe kwa wale wadaiwa sugu wa madeni makubwa ya maji, muanzie huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maji yanahitaji dawa za kusafishia na kutibu. Katiba dawa za kusafishia na kutibu maji, naishauri Serikali iondoe au ipunguze kodi ili dawa hizi zipatikane kwa nafuu ili kumpunguzia mzigo mwananchi kwa sababu dawa

hizi zinagharimu fedha nyingi na ni lazima tuzipate ili tusafishe maji yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashauri au nakubaliana na wazo la Wizara kwa kuhamasisha wananchi sasa katika Halmashauri, Wilaya na Mikoa na maeneo yote yanayojengwa, uvunaji wa maji ya mvua. Maji ya mvua uvunaji wake baada ya kutengeneza miundombinu inakuwa ni rahisi na salama na hayahitaji tena madeni makubwa ya kulipia umeme katika kuyavuta maji. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tukihamasishana sisi wananchi katika uvunaji wa maji ya mvua, hii itasaidia sana kutatua baadhi ya matatizo hasa kwenye kilimo na mifugo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini. Wakala wa Maji Vijijini itaisaidla sasa Wizara kusimamia moja kwa moja miradi ya maji lakini pia itasimamia moja kwa moja matumizi ya fedha za miradi ya maji na kufuatilia maendeleo yake kwa haraka zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea, niongelee kuhusu Tume ya Umwagiliaji. Tume hii ndiyo chemchem na chimbuko la kilimo cha umwagiliaji. Hivyo ni vyema basi fedha zinazotengwa kwa ajili ya Tume ya Umwagiliaji zipelekwe kwa wakati na pia kutafuta vyanzo mbalimbali vyta fedha vyta kusaldia Tume hii ya Umwagiliaji ili kuweza kutekeleza majukumu yake, kwani kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi kilimo chetu kimekuwa kinayumba. Kwa hiyo, kilimo cha kumwagilia ndiyo kilimo kitakachomkomboea mwananchi wa kijijini katika kukamilisha azma ya kujiletea uchumi wa maendeleo, uchumi wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa wa wataalam wa maji na umwagiliaji, naishauri Wizara inayohusika na kuajiri itoe kibali sasa, Wizara iajiri wataalam hao wa maji na pia wataalam wa umwagiliaji ili kuweza kutekeleza majukumu ya kumsaidia mwananchi katika kilimo bora na pia kumsaidia mwananchi kule aliko kijijini kwenye

Mamlaka za Maji na Halmashauri kuweza kupata wataalam wa maji na miundombinu ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ya kukaribia kukamilisha zile fedha za miradi ya maji ya Mfuko wa India ambazo fedha hizi zikipatikana zitasaidia miji 17 ya Tanzania kupata maji. Hapo tutakuwa tumetatua tatizo kwa kiasi fulani la upungufu wa maji ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti maji yasipotee, hatua ya Wizara ya kutengeneza miundombinu ya maji iliyochakavu na kutengeneza mingine mipyä ili kudhibiti maji yasipotee kiholea, nashauri suala hili litiliwe mkazo. Katika kutengeneza miundombinu hiyo ya maji na kuanzisha mingine mipyä, tuangalie ubora wa vifaa, mitambo na miundombinu hiyo kwa sababu inaelekea kuna baadhi ya vifaa na miundombinu ni mipyä lakini tayari imeshakuwa chakavu na inavujisha maji ovyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika uhifadhi wa vyanzo vyä maji, naipongeza Serikali kwa kuhifadhi vyanzo vyä maji vyote nchini na pia kuongeza vyanzo vipyä vyä maji na kuvifanya kuwa maeneo tengefu. Hili la uhifadhi wa vyanzo vyä maji linahitaji sote wananchi tulipe kipaumbele kwa sababu baadhi ya vyanzo vyä maji wananchi wanavichafua kwa makusudi. Kwa hiyo, jitihada za wazi zinahitajika katika kuhifadhi vyanzo vyetu vyä maji ambavyo ndiyo chanzo kikuu cha maji. Tuvihifadhi na tuviwekee uangalifu wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Chuo cha Maji, hiki ndiyo chuo ambacho kwa Tanzania hii kinatoa wataalam wa maji na wataalam wa uchimbaji wa visima na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, nashauri chuo hiki kiendeleee kuongeza wanafunzi na kuongezewa fedha ili tupate wataalam wengi wa maji, tuwasambaze vijijini kote ili wakasaidie miradi ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Uchimbaji Visima (*DDCA*), nashauri Serikali, kwa sababu hiki kitengo ndiyo kinachosaidia kuchimba visima na mabwawa ndani ya nchi yetu, kiongezewe mitambo ya kisasa na wataalam wa kisasa wanaoweza kuchunguza maji ndani ya Tanzania yetu, wapi yapo, yapo kwa kima gani, kwa ukubwa gani, kwa mita ngapi ili tuweze kufanya kazi ya uchimbaji wa visima kwa usahihi zaidi na kupusha kuchimba visima ambavyo baadaye havitoi maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii *DDCA* inatakiwa ijengewe uwezo wa kutosha na vijana wetu watakaotoka *DDCA* wasambazwe wilayani na mikoani ili kusaidia uchimbaji wa visima, mabwawa na utengenezaji wa mabwawa ya kuvunia maji ili wananchi tuvune maji na tupate maji kwa uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho namalizia kwa kusema naipongeza Wizara kwa jitihada zake. Suala la maji ni la msingi, wananchi tunahitaji maji, mimea inahitaji maji, wanyama wanahitaji maji. Suala la maji sasa hivi Serikali tumejitwisha kwenye mabega, inafaa kwa wakati huu tuliweke kichwani liwe ndiyo *agenda* kubwa ya maji katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Aboud. Mheshimiwa Dunstan Kitandula atafuatiwa na Waheshimiwa watakaogawana dakika tano tano, Mheshimiwa Suzana Mgonukulima na Susan Kiwanga.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi nitoe mchango wangu kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema ambaye ametupa uhai na tunaweza kuwatumikia Watanzania. Namuomba anipe uwezo wa kuchangia vyema, nichangie nikiwa sober katika suala hili muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ziara yake aliyoifanya Jimboni kwangu Mkinga, kuja kujionea mwenyewe changamoto kubwa ya maji katika Wilaya ya Mkinga. Ulijiona mwenyewe kwamba Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga hatuna maji, lakini uliona vilevile miradi inayoendelea na changamoto zake. Mheshimiwa Waziri nikukumbushe tu ziko hati tatu mezani kwako, Hati ya Mradi wa Doda shilingi milioni 166, hati ya Mradi wa Bwagamacho shilingi milioni 54, Hati ya Mradi wa Mbuto shilingi milioni 227. Tunaomba fedha hizi zilipwe ili kazi ya miradi ya vijijini iendelee. Mheshimiwa Waziri utakumbuka pale Parungu Kasero ulipokuja tulikumbana na changamoto ya kupeleka umeme mwezi wa 11 ulipokuja ukaahidi kutoa shilingi milioni 49 fedha zile hazijafika, tunaomba sana utusaidie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa tumesikia kwamba maji ni uhai, tumekua tukisikia kauli hiyo kwamba maji ni uhai lakini kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri kinatuambia takribani asilimia 41 ya wananchi wakioko vijijini hawapati maji, maana yake hakuna uhai.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Mataifa mwaka 2010 kwa kutambua changamoto hii ikasema maji safi na salama ni haki ya msingi kwa maisha ya binadamu na kwamba ikifika mwaka 2015 tuwe tumetatua tatizo la maji vijijini kwa asilimia 50. Sasa ukiangalia *Human Development Report* ya recent na ukiangalia machapisho ya wenzentu wa *ESRF* wanatuambia nguvu yetu kwenda kutatua tatizo la maji inakwenda taratibu mno. Kutoka asilimia 45 mwaka 2004/2005 mpaka leo tunazungumzia asilimia 58 tunakwenda taratibu mno. Wakati hali ikiwa hivyo, leo hii tunazungumzia cases 5,800 za kipindupindu zinari potiwa kila mwaka nchini. Wakati hali ikiwa hivyo tunapoteza vijana wetu wa chini ya miaka mitano vinapatikana vifo vya watoto 18,500 na katika hao asilimia 90 vinasababishwa na kukosekana kwa maji safi na salama. Kama Taifa tutaendelea kuiachia hali hii mpaka lini? Mpaka lini tutakubali kupoteza nguvu kazi hii.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonesha kwamba

kila mwaka kwa kutopeleka maji safi na salama tunapoteza biliioni 301mpaka lini kama Taifa tutakubali udhaifu huu. Nimesoma ripoti ya Kamati wanasema tumepeleka kwa asilimia 22 tu za fedha zile. Kwenye umwagiliaji ndiyo usiseme, hapa tunasema kilimo kitukwamue kutoka kwenye umaskini wetu, kilimo cha kisasa cha umwagiliaji hatupeleki fedha, tunakusudia nini. Nawasihi sana tupeleke fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilisema hapa kwamba tulipoamua kupeleka umeme vijiji tulipoamua kuweka tozo Serikali walikuwa wagumu kukubali tozo ile lakini leo hii tozo ile ndiyo inatusaidia kupeleka umeme vijiji. Nikashauri hapa mwaka jana kwamba hii tozo inayopigiwa kelele na Wabunge kwenye mfuko wa maji tuiongeze tufikie shilingi 100; hatukuongeza. Lakini leo kinachotuondoa aibu ni Mfuko wa Maji kupidia tozo ile. Nawaomba sana Serikali muwe waslikivu tunaposhauri mambo haya tuongeze tozo lile ili twende tukaondoe tatizo la maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, bado narudia kusema Makao Makuu ya Mkinga hatuna maji nimeona kwenye vitabu mmetupangia shilingi billioni mbili kwa ajili ya kuanza usanifu kwa Miji kama mitano hivi ya Mkoa wa Tanga. Nawashukuru kwa *gesture* hii, lakini nikumbushe tu mwaka jana mlifanya hivi na fedha hazikwenda. Tunaomba safari hii fedha hizi zitoke ili usanifu ule uweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, nimeona mmetupangia shilingi milioni 500 pale Horohoro lakini mkumbuke wakati mkitupa shilingi milioni 500 mradi ule wa kupeleka maji Horohoro lakini mkumbuke wakati mkitupa shilingi milioni 500 mradi ule wa kupeleka maji Horohoro unazungumzia billioni sita ni mradi unaoenda ku-save kile kituo chetu pale cha *one stop border center*, tuondoleeni aibu ya watu wetu kwenda kuchota maji Kenya. Haipendezi sana kila siku tukisema maneno haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mradi ule wa kupeleka maji kutoka Mto Zigi ni muhimu sana. Ni mradi ambao utatusaidia kupeleka maji kwenye viwanda vile 10 ambavyo tunakusudia

kuvijenga, uwekezaji wa trillioni 7.6 hautaweza kufanikiwa kama hatutapeleka maji kwenye eneo lile, tunawasihi sana muone umuhimu wa kupeleka maji kwenye eneo lile. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dunstan Kitandula kama nilivyosema akina Suzan wakimaliza ataanza Mgonokulima atafuatia Susan Kiwanga kwa dakika tano tano, atafuata Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa na Mheshimiwa Daniel Nzanzugwanko. Mheshimiwa Mgonokulima.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa afya siku hii ya leo niweze kuchangia kwenye Wizara hii. Ninakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara ya Maji ukizigatia tunavyosema maji, maji ni kila kitu katika maisha yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia suala la maji kama ni uhai na ukiangalia kwa jinsi Serikali yetu haitaki kutekeleza ili sera hii ya kuwa maji ni uhai iweze kuwepo mimi nasikitika sana. Maji ni tatizo kwa nchi nzima hususan hata kwenye Mkoa wangu wa Iringa ukiangalia Nyakavangalala, Mkulula, Usolanga, Area Mgungwe, Luhota maji hatupati.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwenye kitabu cha Waziri ukurasa 267 hadi 279 visima ambavyo vimechimbwa kwenye Mkoa wa Katavi, jumla kulikuwa na visima 225 kwa nchi nzima lakini Mkoa wa Katavi peke yake ni visima 79.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko hayo ukitoa unaona ni visima 146 vinavyobaki kugawanya Mikoa 29 na ukigawa kwenye mikoa 29 unaona kila Mkoa utapata visima 7.7 ukifanya *estimation* ni visima nane lakini Mkoa mmoja tu visima 79. Haya ni masikitiko kwa sababu Mkoa wa Katavi ndiko anakotoka Waziri wa Maji. Tukisema sisi watu wa...

**SPIKA:** Suzan Mgonokulima kuna taarifa, Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa Mjumbe kwamba utekelezaji wa miradi kuchagua teknolojia ya kwamba unachimba kisima, unatumia bwawa au unatumia maji ya mteremko ni suala la Wilaya husika. Sasa kama Mkoa umeamua kuchimba visima, mimi kwangu siwezi kuchimba kisima kwa sababu siwezi kupata maji, lakini napata maji kutoka vyanzo vingine. Kwa hiyo, nataka tu kumpa taarifa kwamba kwa Mheshimiwa Waziri ndio teknolojia waliyoitumia na kila Wilaya inapanga yenyewe na siyo Waziri wa Maji anayejipangia.

Mheshimiwa Spika, nilitaka apate hiyo taarifa.  
*(Makofî)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Suzan taarifa hiyo endelea.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo siipokei kwa sababu Waziri wa Maji ndiye anayesimamia Mikoa yote ya Tanzania wapate maji, kwa msimamo huo yeye angelazimika kuhakikisha wataalam wanaenda kutoa elimu hiyo kwa Mikoa yote ya Tanzania.  
*(Makofî)*

Mheshimiwa Spika, ninaona upinzani tukisema tunataka Mawaziri wasitokane na mfumo wa Vyama vya Siasa ni kwenye tija kama hii, maana wakipatikana Mawaziri wenye taaluma unapoingia kwenye miradi kama hii hutapendelea huko unakotaka upate kura wewe. Sisi wote Wabunge tunataka turudi humu ndani. Namuomba Waziri wa Maji anapohitimisha hoja yake hii hebu aniambie vijiji nilivyosema atapeleka wataalamu lini wakatoe elimu hiyo kamaaliyoifanya kwake Katavi hatimaye wakapata hivyo visima 79 badala ya kupata visima 7.7. *(Makofî)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa hii miradi mikubwa ya maji ambapo Serikali inawekeza ukiangalia bajeti ya

mwaka jana 2017/2018 Bunge hili lilipitisha bajeti ya bilioni moja kwa ajili ya mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Kahama, Shinyanga hatimaye Tabora. Hadi 30 Machi, 2018 hakuna hata senti tano iliyoenda. Sasa tumbakiwa na miezi mitatu ili bajeti ya mwaka 2017 ifungwe, ninaomba Waziri wa Fedha anataka kuniambia katika miezi mitatu iliyobakia hiyo trillioni moja tulioipitisha hapa ndivyo ataitekeleza kwa kipindi kifupi hiki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri ni vema tufikie wakati wa kupanga miradi yenye uwezo wa fedha ambazo tunazipata kwenye nchi yetu ili iweze kutekelezeka hatimaye Watanzania wote waweze kupata maji. Kwanza nina masikitiko makubwa ninapozungumza hapa katika Mkoa wa Iringa Wilaya ya Kilolo, Kijiji cha Nyanzu chenye wakazi wasiopungua 2,500 wenyewe kazi yao ni kilimo cha umwagiliaji ambapo takribani kama heka zisizopungua 2500 ni shamba la umwagiliaji. Hadi ninapozungumza hivi heka hizo zote vitunguu vimekauaka kwa sababu ya kukosa maji. Sasa mnaponiambia Mjumbe aliyepita anasema ni Halmashauri ambazo zinatakiwa zisimamie suala la maji wakati Waziri mwenye dhamana yupo, mwenye wataalam wake...

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba maji watu wa Nyazwa wapate waweze kumwagilia mashamba yao. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, mimi siku zote nilikuwa najua Suzan Mgonokulima ndiyo mpole katika wote, kumbe huku hakuna aliyepoa. Mheshimiwa Susan Kiwanga kwa dakika tano. (*Kicheko*)

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba nilindiwe dakika zangu.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi na naanza moja kwa moja kwa sababu dakika zenyewe tano,

kwamba miaka mitatu mfululizo kwa mujibu wa vitabu vyao na takwimu zinaonesha kwamba Serikali ya CCM ilikuwa tunapitisha bajeti Bungeni mabilioni ya pesa, lakini ni asilimia 26 tu ya pesa tunazopitisha na Bunge ndiyo zinaenda kufanya kazi ya maji. Ndiyo maana tunapotaka kusema kwamba hii bajeti ukilinganisha na bajeti ya ndege yaani ni mara mbili ya bajeti ya maji. Sasa tukisema Serikali ya CCM kipaumbele chake ni ndege siyo maji mnakataa nini? Tukisema Serikali ya CCM inashughulikia maendeleo ya vitu badala ya watu mnakataa nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hiyo ni hatari kwa Taifa letu, ndiyo hivyo hivyo Mheshimiwa Jenista siku ile alinipunja dakika zangu unamwona yule ameshaanza. Nilindie dakika zangu Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Nitazilinda kabisa Susan usiwe na wasiwasi, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa HK.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante nimesimama ili kumpa taarifa msemaji na hususan kwenye jambo linalohusiana na namna kama nchi tunavyoweza ku-set vipaumbele vyetu kwamba tununue ndege ama tununue maji. Naona limejirudia tena mara ya kwanza nilivumilia, lakini naona sasa safari hii niseme kidogo kutoa ufanuzi kwa mujibu wa Kanuni 68(8) ambayo inahusu taarifa na ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, kwenye nchi mnawenza mkaamua kipi kianze na inaweza ikawa kama hadithi ya kuku na yai, kwamba mfanye uwekezaji kwenye sekta za kiuchumi ama mfanye uwekezaji kwenye sekta za huduma. Mkifanya uwekezaji kwenye sekta za kiuchumi maana yake mnatia chachu ya kukua kwa uchumi ama muamue kuwashudumia wananchi wetu. Kwenye sekta ya utalii tunahitaji ndege na sekta ya utalii inachangia Pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 17.6, inachangia fedha za kigeni.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, inachangia zaidi ya dola bilioni 2.3 kwa mwaka. Sasa tunapowekeza huku lengo letu tupate kodi, tupate mapato ambayo yatatusaidia kwenda kuwashudumia wananchi kwenye sekta za huduma kama maji, elimu na afya.

Mheshimiwa Spika, nilipenda apokee taarifa hiyo ili aelewé tu kwamba kwenye *ku-set priorities* za nchi unaweza ukaamua kuwekeza kwenye sekta za kiuchumi ama kwenye sekta za huduma, na kuamua uanzie wapi ni changamoto kidogo ambayo tunaweza tukaijadili sisi kama Wabunge.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge taarifa hiyo alikuwa anapewa Susan Kiwanga siyo ninyi kwa hiyo Mheshimiwa Suzan Kiwanga taarifa hiyo?

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, Bunge lingekuwa *live* ingekuwa tamu sana. Hii taarifa siipokei kwa asilimia 220 kwa vile umekuwa Waziri sasa ndiyo maana unasema hayo unayoyasema, ulivyokuwa unakaa hapa mbona ulikuwa husemi hivyo, acha hizo wewe. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi namuuliza huyo aliyesema hiyo taarifa kama nyumbani kwake ana shilingi 100 na chakula cha watoto kinagharimu shilingi 80 na anataka aende akajenge nyumba ya shilingi 100, je atatoa 100 kwenda kujenga nyumba au atalisha kwanza watoto? Acha hizo wewe! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninasema hapa nikiwa na uchungu mkubwa, leo ndani ya Jimbo la Mlimba Naibu Waziri nakushukuru ulienda na mimi mama yako, uliona wananchi wa Mlimba walivyokulilia na wewe ukashuka ukalia nao. Machozi yananitoka, wanaimbä Mlimba maji, Mlimba maji, mito mingi lakini kuna kisima kimoja, haki ya Mungu nasema akina mama, watoto, wazee wanapata maji kwa wiki moja mpaka wiki mbili kwa mzunguko. Naibu Waziri umewaona wananchi wa Mlimba, leo unaniambia kipaumbele ndege wewe Mungu atakulaani Kigwangalla, haki ya Mungu

nasema hapa nikimaanisha. Ukiniambia leo kianze nini nasema maji, wananchi wa Mlimba wanataka maji. Kuna mito mingi lakini inatuharibu wakati wa mvua, inatupasulia nyumba, barabara lakini ikiisha mvua hakuna maji, nataka maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tulipita na Naibu Waziri kuna mradi mkubwa wa umwagiliaji pale Njage, Kata ya Mchombe Serikali imeingiza hela nyingi lakini cha kushangaza ule mradi wanamwagilia wakati wa mvua, wakati wa kiangazi hakuna maji. Ndiyo maana tunaomba tuwekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa kuchimba mabwawa ili kuleta tija kwa pesa mnazopeleka, kwa mfano pale Njage Serikali itengeta pesa kwa kujenga bwawa ili tukinge maji ya mvua, tumwagilie na tupate mpunga masika na kiangazi.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai, hapa wote mmeoga maji, mnakunywa maji, hebu mkae hapa Mawaziri wote na wote tusioge angalau siku mbili tuone kama tutafungua *air condition* humu ndani! Maji ni kipaumbele. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niseme kwa Watanzania Serikali ya CCM ya Awamu ya Tano inashughulikia vitu siyo maendeleo ya watu hiyo haiwezekani. Muda haunitoshi mpaka nimelia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga taarifa, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mdogo wangu Susan, ninajua maji ni kipaumbele, lakini suala la maendeleo la watu liko kwenye mpango wa miaka mitano wa pili, imeandikwa kabisa kwamba maendeleo ya watu na siyo maendeleo ya vitu na inatokana na Serikali hii ya CCM.

Kwa hiyo, ni kweli Serikali inafanya mambo yote kwa ajili ya kuelekeza kwa watu kama alivyosema Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kigwangalla, tumepeleka kwenye ndege tupate hela nyingi kwenye utalii tupeleke kwenye maji.

Kwa hivyo, Serikali ina-pursue maendeleo ya watu na siyo maendeleo ya vitu, na ninaomba Mheshimiwa Susan kwa hilo uliachie Serikali ya CCM, lakini maji ni kipaumbele.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa yake naipokea kwa tahadhari kwa kuwaambia kwamba wananchi wa kule Jimboni kwake wanakunywa tope, tena pamoja na punda. Naikataa kwamba, kipaumbele, eti vitu kwanza, wewe vipi? Yaani wewe uanze kwanza kujenga nyumba watoto ndani wasile? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nyumba yenyewe unajenga na maji, viwanda vyenyewe maji, umeme *Stiglers' Gorge* maji, kila kitu maji, leo unasema maji siyo kipaumbele. Tunataka kipaumbele kiende kwanza, halafu hivi vingine vitakuja, hamuwezi mkatunanhii, Serikali ya CCM ya Awamu ya Tano inafanya maendeleo ya vitu siyo maendeleo ya watu, ndiyo maana mnapeleka asilimia ndogo sana kwenye masuala muhimu kama ya maji. Naomba wapeni pesa hawa Mawaziri ili wafanye kazi.

**SPIKA:** Nakupa dakika moja umalizie.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kweli leo eeh, shughuli ipo.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, angalia hao taarifa nyininge!

**SPIKA:** Mwachseni amalizie.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hata kwenye Jimbo lako la Kongwa tunapita barabarani tunaona watu wanavyokwangua maji. Kwanza ni aibu barabara kubwa inayokuja Makao Makuu watu wanachota maji kwenye madimbwi, *shame Tanzania, shame*

CCM. Hebu boresheni wapeni pesa za kutosha kama tunavyopitisha, ili watuletee tuwasulubu Mawaziri, kwa sasa hivi hatuwezi kuwasulubu wanajitahidi lakini hawana pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama alivyoomba Mheshimiwa Mnyika badala ya bajeti hii tufanye kweli, mbona tulifanya kweli kwenye Wizara ya Ujenzi, tuliweka mguu chini wakaenda wakajadili wakaongeza pesa na safari hii tuwaoneshe Bunge kwamba hawa lazima wapewe pesa ili miradi iongezeke huku chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na Mungu atusimamie. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Kiruswa Stephen atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko. Dkt. Kiruswa la Longido.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia pia fursa hii kumpongeza Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya na kuipongeza timu yake ya Baraza la Mawaziri, na Watendaji Wakuu wa Serikali kwa sababu kazi ya Serikali ya Awamu ya Tano inaonekana na inasikika, mwenye macho haambiwi tazama, mwenye masikio pia haambiwi sikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana kazi kubwa aliyofanya Waziri kuandaa hotuba hii. Napishana na walisema kwamba hotuba hii ni kubwa na haina kitu, hotuba hii ni nzuri ina vielelezo vyta kutosheleza, ina *details* za kutosha kwa wale wanaopenda *details* na wengine kwa sababu ya haiba zao wanapenda tu kuangalia *facts*, ina *facts* za kutosha nimeona viambatanisho ambavyo sijaona katika hotuba nyingine zilizotangulia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kugusia haya maoni ya Kamati na kwa kweli ninaiunga mkono asilimia mia moja hasa kwenye mapendekezo matatu ambayo bila hayo nafikiri bado tutasuasua sana kama Taifa linalotaka kujenga Taifa lenye uendelevu wa viwanda. Walipotoa maoni kwamba, sekta ya umwagiliaji iongezewe pesa wawze kukuza kilimo cha umwagiliaji hawajakosea, tuzingatia kwamba sasa hivi tuko katika zama za mabadiliko ya tabianchi, mabadiliko ya hali ya hewa, bila kukuza kilimo cha umwagiliaji hatutatoka katika umaskini na upungufu wa chakula katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono 100 kwa 100 kwamba, hiyo sekta ya umwagiliaji iongezewe pesa, tena ipewe nyangi kwa sababu japo kule Longido hatuna mito mingi ya kumwagilia, lakini kuna mto mmoja ambao unatirisha maji hadi kwetu Ngarenanyuki na nitaongelea katika muda huu wa dakika chache nilizonazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia katika maoni haya ya kamati ninaunga mkono hili suala la tozo, hizi tozo kwenye mafuta kwa lita ya petroli na dizeli kuelekezwa katika kusaidia kufikisha maji katika vijiji vingi katika nchi yetu ambavyo bado havina maji ni suala lenye tija. Ninaunga mkono na ninaomba hili lizingatiwe ili tuone kama tutapunguza kero ya maji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninaunga mkono mapendekezo ya kamati katika suala la kuanzisha Wakala wa Maji Vijiji. Kama vile ambavyo Wakala wa Barabara za Vijiji (*TARURA*) imanzishwa tena hivi karibuni, naomba hili nalo lipewe kipaumbele tuone kama tutatoboa katika kupunguza kero ya maji katika vijiji yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo basi naomba nidonoe vipengele vichache katika taarifa hii ya hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Kwanza napenda kuendelea kuishukuru Serikali kwa mradi mkubwa wa maji ya Mto Simba kuja katika Mji wa Longido ambao unajengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 15. Mradi huu ambao uligawanywa

katika sehemu nne na Waziri amebainisha vizuri katika hotuba yake hii, ulikuwa na hivyo vipengele vinne; ujenzi wa chanzo, ambao kwa masikitiko makubwa nashangaa kuona kwamba umeshatimizwa kwa asilimia 40 tu na muda unazidi kwenda, ulazaji wa mabomba umekamilika kwa asilimia 42 tu, ujenzi wa tenki kwa asilimia 90 na ninashangaa hili tanki likimalizika na maji hayajafika matokeo yake ni nini kama sio kukauka na kupasuka kwa kukosa maji na pia mfumo wa usambazaji wa mabomba ambao umekamilika kwa asilimia 75. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nasikitika kwamba juzi nilipita Jimboni kwa haraka nikaona kwamba katika huu mfumo wa usambazaji kuna mitaro ilichimbwa ikaachwa wazi maji yakaja yakafukia na sasa hivi pia kwa sababu labda wameshituka tunajadili hii bajeti, nimeona wanaanza kuchimbua na kutoa *pipes* nyiningine kule chini, inawezekana waliweka ambazo ziko chini ya kiwango. Naomba sana wakandarasi wa mradi huu wafuatiliwe kwa makini na Serikali ijaribu kuukaribia huu mradi maana wananchi watakata tamaa kama ahadi ya kupelekewa maji ndani ya mwaka huu tena ilikuwa ni ndani ya mwezi huu haitatimia kwa muda mfupi iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, pia, nashukuru kwa sababu nimeona kuna fungu la shilingi bilioni sita limetengwa ili kukamilisha mradi huu. Basi naomba Serikali iweke mkono uende kwa kasi zaidi kuliko ilivyo kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kujulisha Bunge lako tukufu kwamba maji haya yakifika Longido tu na Orbomba na Engikahet ambapo inakiswiwa kwamba itawanufaisha watu takribani 16,712 isije ikachukuliwa kwamba Longido kero ya maji imemalizika. Longido ina vijiji 49 na kutakuwa bado maana hivi ni kama vijiji vitatu tu maji yanafikia hayatakuwa hata yamesambazwa, kuna zaidi ya vijiji 45 bado vina kero kubwa ya maji na hivyo Serikali katika bajeti hii sijaona kama wametupatia kipaumbele katika kuendeleza miradi ya maji, hasa maji ya visima virefu sehemu ambapo hakuna mito ya kupeleka maji karibu vikiweko vijiji

vyo Wosiwosi, vijiji vya Magadini kule ambako hata sasa hivi nasikitika kusema kwamba baada ya mvua kubwa kunyesha na mafuriko kutokea kumezuka ugonjwa wa kuhara na kutapika ambaao dalili zake hazipishani sana na kipindupindu, lakini sina taarifa rasmi niweze kutamka hivyo, ila kuna watu wamepoteza maisha na tusipopeleka maji kwa haraka katika ukanda huo wa Ziwa Natron kuna hatari mara mbili, kuna hiyo milipuko na pia kuna hatari kubwa ya watu kuendelea kuumia mifupa kama alivyosema dada yangu Mheshimiwa Mollel na ninamuunga mkono jana kwa upande wa Arumeru, maji ya *Lake Natron* nayo ni hatari sana yanapinda hata mpaka miguu ya wanyama wanaokunywa maji yale na watu wale wanaishi tu kama kilometra nane kutoka Mlima Gelai ambako maji ya bomba yangeweza kufikishwa kule tena ni maji masafi kutoka chemchemi, hiyo kero ingeweza kuondoka.

Mheshimiwa Spika, pia nipende kugusia kwa sababu ya muda kwamba katika huu Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji pale Longido hatuna mto, lakini Arumeru ndugu zetu wana maji ya Mto Engarenanyuki. Ule mto ni mkubwa, unapeleka maji mengi tu mpaka kule bondeni katika eneo la Wilaya ya Longido hasa katika Kata ya Tingatinga, lakini wakulima wa Kiholela wanaolima nyanya na ni zao kubwa la biashara wametumia mifumo isiyo ya kisasa, maji mengi yanapotea, maji yanaelekea katika mashamba kwa mifereji.

Mheshimiwa Spika, naomba mto huu ujumuishwe kati ya mito ambayo imebainishwa katika hotuba hii ambayo itafanyiwa usanifu ili kilimo cha kisasa kiweze kutekelezwa, matenki makubwa yajengwe na mabomba yaunganishwe watu walioko Tingatinga hasa vijiji vya Ngereiyani nao wawewe kufaidika na kilimo cha nyanya maana maji haya yana *fluoride* na *chloride* kwa wingi kiasi kwamba hayafai kwa matumizi ya binadamu lakini ni maji mazuri sana kwa kilimo cha nyanya.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda ninaomba pia nisiashe kusemea kidogo suala la Wakala wa Uchimbaji

wa Visima (*DDCA*). Nimeona kwamba katika bajeti hii hatujaguswa kabisa katika visima ambavyo vitachimbwa, sijaona popote kwamba Longido watachimbiwa visima nya maji ukizingatia kwamba kero ya maji katika zaidi ya vijiji 45 iko palepale na Wilaya ya Longido ni moja ya Wilaya kame sana katika nchi yetu. Tena niombe *DDCA* pia wapeleke wataalam, wafanye survey ya maji katika vijiji vyote nchi hii ili tuwe tayari tunajua kwamba maji yako wapi, pesa zinapopatikana hasa mkitutengea hizi za mafuta tuweze kuchimba visima na kuondoa kero ya maji.

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kusema kwamba katika huu mradi wa kujenga mabwawa, hatuna bwawa hata moja ambalo limebainishwa. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba katika mvua za mwaka huu ambazo zimekuja kwa kasi kubwa baada ya kiangazi cha miaka mingi, tumebomokewa na mabwawa mawili makubwa yaliyokuwa yanasaidia maisha ya wananchi wa Longido. Bwawa la Kimokouwa limepasuka, Bwawa la Emuriatata limepasuka na Bwawa la Sinoniki lilishapasuka tangu mwaka juzi na ningeomba sana katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri hebu angalia jinsi ya kutusaidia hayo mabwawa yaweze kufanyiwa ukarabati kwa sababu, ndiyo yanayosaidia maisha ya watu wa Longido.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna mabwawa yaliyojaa udongo, bwawa la Tingale Sing'ita ambalo huwa halikauki kabisa na linasaidia maisha ya watu wa Kata mbili na Tarafa mbili, Tarafa ya Longido, Tarafa ya Ngaranaibo, ninaomba hili bwawa pia liangaliwe ili liweze kufukuliwa na tuna lingine ambalo liko katika Kijiji cha Ngoswe linaitwa Ngweseiya, pia limejaa udongo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nihitimishe hoja yangu kwa kusema kwamba sambamba na harakati za Serikali za kutuletea maji safi, pia kuna ahadi mbili zilishatolewa na Mawaziri hapa, Waziri wa Mifugo na Waziri wa Maji pia kwamba watatuchimbia mabwawa katika Kata ya Tingatinga na katika Kata ya Gilai Lumbwa upande wa Wosiwosi. Ni maeneo ambayo yana kero kubwa ya maji na

upimaji ulishafanyika, survey imefanyika, usanifu umefanyika na sijaona kama kuna mradi umewekwa katika bajeti hii ili tupate maji hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho tuna kero kubwa moja ili niweze kumalizia kwa sababu ya muda. Kwamba, katika hii miradi inayotekelawa Longido, hasa ule wa *World Bank* uliochukua miaka saba na bado haujakamiliwa wananchi wanaanza kupoteza matumaini maana miundombinu mingine ilijengwa, kulaza mabomba, kuweka visima sehemu za kunywa watu maji...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kisurwa dakika zako zimeisha.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja, lakini tuisahaulike katika suala moja la msingi kwamba maji ya *World Bank* yakafanyiwe uchunguzi na siyo hiyo tu ningeomba pia wananchi hawa wa Longido washirikishwe Halmashauri ishirikishwe katika huu mradi wa maji ya mto Simba maana Halmashauri haihusiki imetoka Wizarani ikaenda Mkoani.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa muda.  
*(Makof)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, na mimi kwa namna ya pekee naomba kwa kweli kuwapa hongera nyingi sana Waziri *Engineer Kamwelwe*, Naibu wako Waziri, Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo, Naibu Katibu Mkuu *Engineer Kalobero* na Wakurugenzi wote wakiongozwa na ndugu Mafuru mnafanya kazi nzuri, hongereni sana. Mnafanya kazi katika mazingira magumu na kwa kweli ukiangalia taarifa ya Kamati na hotuba ya bajeti kwa kiwango kikubwa mmefanyia kazi zile shilingi bilioni 158 za

Mfuko wa Maji ambazo zimekuwa *ring fenced*, hongereni sana kwa kazi nzuri ambayo mmefanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa kwenye Kamati ya Maji kipindi kilichopita, najua uwekezaji mliouweka ni mkubwa sana katika maeneo mbalimbali ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam. Mmefanya kazi kubwa sana, miradi mikubwa mliyowekeza sasa muisimamie iweze kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la takwimu, katika ukurasa 214 na 215 kwenye skimu za umwagiliaji na katika skimu zilizoko katika Mkoa wa Kigoma kuna skimu moja muhimu sana hamkuiweka pale, nafikiri ni *oversight*, Skimu ya Maji ya Msambala ni muhimu sana pale na iko katika Mji wa Kasulu. Ninaomba kwenye kumbukumbu zenu muiweke sikuionna humu na inawezekana katika mfumo wa kibajeti na yenye mwaka mmeisahau, nilikuwa nakumbusha tu jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, nianze na fedha za India, miradi ya miji 17 ambayo umeitaja kwenye kitabu chako. Naomba Mheshimiwa Waziri najua juhudini zinakwenda, Serikali imeshapiga hatua kubwa kuhusu fedha za mkopo kutoka Serikali ya India kwa miji ile 17 na miji hiyo 17 ni pamoja na Mji wa Kasulu. Kwenye kitabu chako hiki cha hotuba umeeleza kwamba, itakwenda kwa *phases*, kuna *phase one* Zanzibar na miji mingine mitatu/minne, halafu *phase two* na miji mingine iliyo baki. Sasa sikuelewa *logic* kama mradi wa maji unatekelezwa Zanzibar au unatekelezwa Njombe unazuia vipi mradi wa Kasulu usitekelezwe?

Mheshimiwa Spika, sikuelewa *logic* sikuionna hata kidogo, kwa hiyo nilikuwa nafikiri *good practise* kwa sababu hii miradi tumeisubiri muda mrefu na itakuwa na fedha za kutosha, hii miradi ingeanza *simultaneously*. Kama unatekelezwa Zanzibar, unatekelezwa Makambako na utekelezwe na Kasulu kwa wakati huo huo kwa sababu wahandisi tunao wa kutosha wa kufanya kazi hii. Sikuona *logic* ya kuanza kuweka kwa *phase* kwamba hii ni *phase one* na *phase two*, maana kwa tafsiri hii ni kwamba *phase*

two sisi pamoja na Mji wa Kasulu itabidi tusubiri miaka mingine mitatu minne tingoje *phase*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa uweze kuliweka vizuri na wataalam wako wanansikiliza. Tunataka miradi hii, tumeisubiri sana, ianze mara moja katika maeneo yote kwa sababu kuna wakandarasi na wahandisi wengi wa kutosha. Nilifikiri nianze na jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulisema kwa sauti kubwa kwa kweli ni kukushukuru sana. Waziri ninakushukuru sana wewe na timu yako, mmefanya kazi kubwa sana. Katika Jimbo langu nimepokea shilingi bilioni 1.3 kwa kweli zimefanya kazi kubwa sana. Tumejenga chanzo kipyta cha maji katika Mji wa Kasulu ambacho hakikuwepo katika eneo la Kimobwa, Kijiji cha Heru Juu chenye wakazi zaidi ya 15,000 sasa wanapata maji safi na salama. Kijiji cha Muhunga mradi unakwenda vizuri, tunahitaji fedha nadhani watakuwa wameshakuletea *certificate* ili uweze kutupa fedha nyingine kukamilisha mradi ule, kazi ni nzuri na tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, *again* kwenye kitabu chako hiki kuna miradi ambayo imetengewa fedha, nimeona kijiji cha Muganza, nimeona mradi wa maji Marumba unaendelea, kuna miradi Mheshimiwa Waziri ile nimikuwa nikisema sana kwenye Wizara yako, miradi ya siku nyingi, kule kwetu ilianzishwa na watu wa *NORAD Water Project*. Kuna miradi ya siku nyingi sana na jambo hili nimeshazungumza na hata na Katibu Mkuu wako na Ndugu Kalobero. Tuna mradi mkubwa sana wa Kijiji cha Ruhita - Kanazi ni miradi wa siku nyingi inahitaji tu kufanyiwa *rehabilitation*. Ninafikiri mwaka huu wa fedha ungetafuta fedha, mradi huu ni muhimu sana unahudumia vijiji vitatu kwa mara moja, unahudumia zaidi ya wakazi 50,000 katika vijiji vile. Kwa sababu *system* ipo ni suala la kupeleka wataalam na kuangalia namna bora ya *ku-rehabilitate* ili hatimaye wakazi hawa waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nikukumbushe Mheshimiwa Waziri ni mradi wetu mkubwa wa

maji unaofadhiliwa na Serikali ya Ubelgiji chini ya *BTC*. Ule ni mradi mkubwa sana kwa watu wa Kigoma, una-*cover* Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma, unaanzia Kigoma, Kasulu, Kibondo mpaka Kakonko. Ule mradi inaonekana umekwama na nimezungumza na *RAS* ananiambia tatizo kubwa ni kwamba Serikali ya Ubelgiji inataka *procurement procedures* zifuate Sheria ya Ubelgiji ya *Procurement*, haikuングia kwenye kichwa changu Mheshimiwa Waziri, wewe mwenyewe kwa juhudzi zako umeshafanya mawasiliano na watu wa Kigoma, nilikuwa nafikiri kuna haja ya *ku-fast track* jambo hili. Ule mradi tuna uhitaji sana, fedha zipo, Waziri wa Fedha ameshasaini ile *Financial Agreement* tayari, kwa hiyo tuna fedha zetu kupitia Serikali ya Ubelgiji ambazo zinahitaji *fast tracking* na *control* ya aina fulani ili mradi ule uanze.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mradi wa maji usubiri miaka miwili kufanyiwa *procurement*, *it is just too long*. Ni muda mrefu sana na wananchi hawa wanataka maji. Huu mradi wa Ubelgiji pale Kasulu Mjini ni muhimu sana kwetu kwa sababu una-*cover* vijiji vitatu, Vijihi vya Nyasha, Nyatale na Kijiji cha Kigondo ni vijiji vyenye wakazi wengi sana ningependa sana miradi hii Mheshimiwa Waziri ikamilike.

Mheshimiwa Spika, najua muda hautoshi nizungumzie pia suala hili la kulinda vyanzo vya maji. Hili jambo hata mwaka jana nimelisema. Nakushauri Mheshimiwa Waziri wa Maji wewe na mwenzako wa Mazingira hata Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kigwangalla, muangalie njia nzuri ya ile mito mikubwa tuliyonayo katika nchi hii. Nimeona kwenye kitabu chako kuna mito michache ume-*identify* hapa ukurasa 107. Ukiangalia ukurasa wa 107 kuna mito umeitaja pale, lakini mito hiyo hamjautaja Mto Malagarasi wala hamjataja Mto Kilombero na nimeshangaa sana hata Mto Rufiji hamkuutaja nimeshangaa kidogo. Hiyo ni mito mikubwa sana, mmetaja Ruaha, Wami, Ruvu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu naomba Serikali nzima mkae chini na muangalie namna ya kulinda mito hii mikubwa. Katika nchi hii mito mikubwa ni mito 14 tu, mito mikubwa sana. Mnahitaji kufanya kama mlivyofanya kwa

Ruaha Mkuu mito hii ilindwe kwa sababu ina uhakika wa maji na pengine hii ya kufikiria kwamba maji yatatoka tu Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria pengine itakuwa si sawa sana, wakati kuna mito mikubwa 14 katika nchi hii ambayo tunaweza tukailinda. Kama Serikali mkawa na *strategy* kabisa ya kulinda mito hii ambayo tunataka iendelee kuwepo kwa manufaa ya vizazi vijavyo ni jambo la muhimu sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwisho niwakumbushe tu tulitembelea miradi mikubwa sana mmewekeza katika Jiji la Dar es Salaam. Tumetembelea Ruvu Juu, Ruvu Chini lakini unakumbuka Mheshimiwa Waziri watu wa DAWASCO na DAWASA wakati ule kabla ya hizi fikra za kuwaunganisha walikuwa na changamoto zao nydingi sana, baadhi ya miradi ilikuwa haijakamilika. Miradi ya Changanyikeni, Salasala, miradi mikubwa sana. Kujenga matenki makubwa sana kwa ajili ya kuondoa shida ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Nilikuwa nashauri *strongly* uwekezaji ule uliowekwa katika Jiji la Dar es Salaam na Mheshimiwa John Mnyika hiyo kamati ndiyo tulikuwa wote pamoja uwekezaji ni mkubwa sana umewekezwa katika miradi ile. Ilikuwa ni matumaini yangu kwamba Wizara kwa kushirikiana na DAWASCO off course na DAWASA miradi ile ni mikubwa sana ikamilike kwa wakati ili kuondoa shida ya maji kabisa katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nilikuwa namkumbusha ndugu yangu Mheshimiwa Mnyika kwamba tulikuwa naye kwenye Kamati ya Maji, hakuna uwekezaji mkubwa kama uwekezaji uliofanyika katika Jiji la Dar es Salaam.

**SPIKA:** Kumbe mambo ni mazuri namna hiyo halafu Mnyika hapa anasema hapana. (*Kicheko*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa namkumbusha tu. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimmtaja Mheshimiwa Cecil Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na muda ukituruhusu Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutumia muda huu kuchangia kwenye hotuba iliyoko mbele yetu ambayo ni Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikitaarifu kiti chako kwa sababu Mheshimiwa Nsanzugwanko hapa ametoka kumalizia anasema kwamba kuna uwezekano mkubwa *DAWASA* na *DAWASCO* sasa hivi wanakwenda kuunganishwa, hii ni kwa ajili ya wakazi wa Dar es Salaam lakini naomba tu tuwasaidie jambo moja na kiti chako kifahamu kwamba kuna ubadhirifu mkubwa sana umefanyika ndani ya *DAWASCO* na wanapokwenda sasa hivi kuunganisha *DAWASCO* na *DAWASA* madeni haya yote yatarudi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya shillingi bilioni 800 na kuna madeni makubwa sana pale ndani, kwa hiyo tunaomba tufahamu, kuna madeni ya umeme ambayo ni shillingi bilioni 3.5; kuna madeni ya *NSSF* pamoja na *PSPF* karibu shillingi bilioni 12; kuna madeni pale ya *TRA* na madeni mengine mengi kiasi wale wafanyakazi wa *DAWASCO* na wafanyakazi wa *DAWASA* wao hawaelewi wanasimama upande gani kwenye kulikamilisha hilli jambo lao. Kwa hiyo, tunamuomba Waziri na ikiwezekana uagize kiti chake kifanye *Special Audit* kabla ya hizi taasisi mbili hazijaunganishwa kutoptaka na madeni yaliyoko kule ndani, otherwise tunakwenda kuwasababishia matatizo makubwa sana watumishi wanaobaki na wale wengine watakaohama pale.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema toka mwanzo Wizara hii ni Wizara nyeti sana inagusa maeneo yote ya Tanzania na kilio kimekuwa kikubwa sana kwa Wabunge wote na wewe mwenyewe pia umeshuhudia kinachotokea hapa. Naomba nitumie nafasi yangu kuwakumbusha pia Wabunge wenzangu majukumu yetu kimsingi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niseme tunatakiwa tuwe wazalendo kwa ajili ya Taifa letu. Jambo la pili tuhakikishe tunasimama mguu mmoja na wapiga kura wetu

lazima tuone maslahi ya wapiga kura wetu yanasisimamiwa na jambo la tatu lazima tuwe na uhakika kwamba tunavitetea na kuviilinda vyama vyetu kwa uchache wake lakini ni jambo la tatu; na mwisho kabisa tuangalie nafsi zetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako na ninavyoona mimi nilivyojifunza kwa hizi siku chache nilizoko hapa ndani kwamba sasa hivi linaanza kuegemea upande mmoja tu, tunaangalia sana maslahi ya chama, tunasahau wapiga kura wetu, tunasahau uzalendo juu ya nchi yetu, lakini pia tunasahau kuhusu nafsi zetu wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumepokea hizi taarifa zote mbili kutoka kwa Kamati, lakini pia tumepokea taarifa ya Waziri mwenyewe kwenye kitabu chake. Vitabu hivi ukiviangalia kwa pamoja vinatofautiana sana kwenye baadhi ya maeneo. Tukianza moja kwa moja kwenye suala la umwagiliaji. Ukienda kwenye kitabu cha Waziri, suala la umwagiliaji ukurasa wa 11 wanasema hivi; “Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina eneo la hekta 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, ambapo hekta 2.3 zina uwezekano mkubwa wa kumwagiliwa, hekta 4.8 uwezekano wa kati na hekta 22.3 zina uwezekano mdogo wa kumwagiliwa.” Anaendelea kusema kwamba; “Serikali ina nia ya kujenga miundombini yenye jumla ya hekta milioni moja kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wadogo wadogo. Hadi mwezi Machi, 2018 jumla ya hekta 475,000 zinamwagiliwa sawa na asilimia 47.44 ya lengo la asilimia 1.6 eneo linalofaa kumwagiliwa”

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu taarifa hizi zote walizotupatia huku juu zilikuwa *irrelevant*. Taarifa hapa ya muhimu walikuwa watuonyeshe namna hii heka milioni moja ambavyo wao wanakwenda kuitumia, matokeo yake wanatuletea taarifa zenye kuvutia, zinazoongea habari za heka milioni 29.4 mwisho kabisa wanakwenda kumalizia kwa kuongelea tu hekta milioni moja ambazo nazo hatujafanikiwa wanakwenda kusema tunakwenda kufanya asilimia 47.44.

Mheshimiwa Spika, tunasema tunataka kwenda kuwa nchi ya viwanda. Sasa tujiulize tunakwenda kwenye viwanda vya aina gani, kwa sababu tunapoenda kung'ang'ana bila kuwasaidia wakulima wa nchi hii maeneo mengi yanafaa kabisa kwa kilimo na yapo yanaonekana tunakwenda kuoanisha vipi kati ya viwanda hivi na sekta ya kilimo. Kwa nini tusitumie nguvu nyangi kuwaongeza nguvu wakulima, tukawaongeza asilimia kidogo pale kwenye suala la umwagiliaji tukaenda kuwasaidia badala ya sasa hivi kujikita kwenye viwanda vya uzalishaji mali. Kwa mfano, tunasema tunakwenda kutengeneza nondo na vitu vingine. Tunawasaidiaje wakulima amba ni asilimia 85 ya wananchi wetu hapa Tanzania ili wao waweze kujkwamua kiuchumi tuweze kusogea mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wameongelea hapa kwenye Fungu Na. 49 kwenye suala la pesa za maendeleo. Ukienda kwenye kitabu cha Kamati wanasema wenyewe hapa kwamba *So far...* kwenye Kitabu hiki cha Waziri wanasema wamepata pesa walizozipokea mpaka sasa hivi walizokuwa wametengewa ni shilingi bilioni 648 lakini wao mpaka sasa wamepokea shilingi bilioni 347. Kamati inatuambia wamepokea shilingi bilioni 135 sasa tumuelewe nani? Ndiyo maana Wabunge wengine wamependekeza hili sasa suala la kuwakalisha Kamati na Wizara watuambie pesa walizozipata mpaka sasa hivi kiasi gani ili tuweze kuwaeleza Watanzania kwamba Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na juhudzi zake zote anashindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu hana ushirikiano mzuri au watu wa Wizara ya Fedha wanataka kumuangusha kwa makusudi. Haiwezekani watengewe bajeti yote hii halafu waende kupata tu pesa kiasi kidogo wakati wenyewe tunasema tuna nia ya kutaka kumtua Mama ndoo kichwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukienda hata kwenye hiki kitabu chao labda ndiyo maana iko hivi, Mheshimiwa hapa anaonekana Mheshimiwa Makamu wa Rais akimtwisha Mama ndoo kichwani. Kwa hiyo, tafsiri yake ni kwamba Serikali haitaki kuwatua ndoo akina mama halafu tunakuja kuitetea hii Wizara kwamba ipate pesa ya kutosha kwa ajili

ya kwenda kuwatua ndoo akina mama na ndiyo maana basi utakuta Wizara ya Fedha haipeleki pesa ya kutosha kuhakikisha miradi ya maji maeneo mbalimbali inakamilika. Kwa hiyo, kwa namna ya pekee kabisa tuwaombe Wizara ya Fedha wahakikishe pesa za maji kila mara zinafika pale kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi hapa umetajwa sana wa *Stiglers' Gorge*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe hii picha siyo kwamba anamtua ndoo?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, anamtwisha. Hiyo picha hapo Mheshimiwa Makamu wa Rais anamtwisha mama huyu ndoo na huyu mama mwenyewe anaonekana yupo Chama cha Mapinduzi amevaa na kilemba kabisa.

**SPIKA:** Kuna wabunge wananiambia anamtua ndoo pale.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Naam!

**SPIKA:** Endelea kuchangia. (*Kicheko*)

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Tunaongelea hapa kuhusu mradi wa *Stiglers' Gorge*. Huu mradi nia yake ilikuwa ni kuongeza uzalishaji wa umeme ili twende kwenye nchi ya viwanda. Sasa tunasema kufikia mwaka 2025 Tanzania itakuwa ni nchi ya viwanda, lakini tukumbuke Bunge hili liliazimia kwamba miradi hii ya kimkakati na ndiyo kisa cha kwenda kuwekeza kwenye miradi ya gesi. Inakuwaje tunakwenda kwenye gesi, gesi inayosemwa inatumika kwa asilimia saba tu, leo tunaacha hii pesa ingekwenda kutumika kuwasaidia akina mama kupata maji tunakwenda kuwekeza *Stiglers' Gorge* wakati Mto Rufiji sasa hivi hata yale makingio yake ya maji yameanza kupungua. Mwanzoni Mto Rufiji ulikuwa unapokea maji kutoka mito midogo midogo 29. Sasa hivi Mto Rufiji unapokea maji kutoka kwenye mitano

tu, kwa hiyo kwa vyovyote huu mto baada ya muda fulani unaweza ukashangaa unakauka.

## T A A R I F A

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil kuna taarifa. Ni Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Maji tunazungumzia kwamba ni mita 400 kutoka nyumbani, Serikali haiwezi kuingizia kila mtu ndani ya nyumba yake maji na ni maji safi na salama. Hapa mama huyu anatwikwa maji safi na salama mita 400 kutoka nyumbani kwake, tatizo liko wapi Mheshimiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil pokea taarifa hiyo.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nilitaarifu Bunge lako kwamba *nusu ya Wabunge humu ndani siyo wapumbavu*. Mimi naomba niendelee. (*Makofi*) [**Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**]

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe naomba ufute hiyo kauli yako, unaposema nusu ya Wabunge siyo wapumbavu unamaanisha nusu ya Wabunge wangu ni wapumbavu. (*Kicheko*)

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba kufuta hiyo kauli na niweze kuendelea kuchangia. Kwa hiyo, nataka tu nikueleze...

**SPIKA:** Sijakusikia bado.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Nimefuta kauli yangu.

**SPIKA:** Haya endelea.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikuambie kwamba kutokana na haya mambo yanayotokea kama hivi unavyoona hii michango na vitu vingine

tunashindwa hasa kusimamia uzalendo ule tunaouhitaji wa kuweza kwenda kumtua mama sasa ndoo kichwani. Tumebakisha tu kwenda kusifia tunafikiri hii ndiyo sifa ya msingi ya Ubunge badala ya kusimamia na kuishauri Serikali. Tumebakisha kupongeza badala ya kwenda kutoa michango yetu ili iweze ku-*improve* hizi ripoti zilizoko pale.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo yanayohusiana na Taifa kwa ujumla sasa nirudi Jimboni kwangu. Tuna vijiji kule kwetu vingi sana, ukienda Kata ya Mlingura, ukienda Kata ya Namajani, ukienda Kata ya Msikisi pamoja na Malembo, Chingulungulu, Nanganga pamoja na Liputo haya maeneo yote ndiko ambako linapita bomba la Mbwinji linalopeleka maji Wilaya ya Nachingwea, lakini pia linapeleka maji Wilaya ya Ruangwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali hapa mwaka jana ilituambia vijiji vyote ambavyo viko kwenye *radius* ya kilometra kumi kutoka kwenye bomba kubwa vitapatiwa maji. Mimi nilisema hapa na nikatoa ushauri mnataka tusichimbe visima virefu kwa sababu tunafahamu lile bomba liko mita tano tu toka usawa wa ardhi, tutakwenda sasa kutoboa ili wananchi wapate yale maji kirahisi kama Serikali haitaamua kuyapeleka yale maji vijiji moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu kuna chombo kinaitwa *MANAWASA* ndiyo kinachotusababishia maji watu wa Masasi pamoja na watu wa Nachingwea. Mara nydingi wamekuwa wakiahidiwa kupata pesa, ukiongea na Mkurugenzi wa *MANAWASA* anasema chombo kile kikiongezewa nguvu kina uwezo wa kutatua tatizo la maji Kanda ya Kusini kuanzia Nachingwea mpaka Kilwa, wanahitaji tu kupewa pesa kidogo. Lakini kuna sintofahamu inayoendelea, kuna miradi ya mabwawa inaendelea kwenye maeneo haya na mtakumbuka hapa Waziri wa TAMISEMI alituambia kwamba wanataka kwenda kutengeneza Bwawa Lukuledi kwa kutumia pesa shilingi milioni 60 kufanya upembuzi yakinifu. Wakati tayari tulifanikiwa kupeleka maji Kijiji cha Chikunja kwa kutumia shilingi milioni 70, sasa hatuoni faida kubwa sana ya mabwawa haya badala ya kuwekeza kwenda

kupata maji safi na salama. Muwashirikishe wenyeji wa maeneo husika ili kuweza kujua miradi ya kipaumbele kwenye maeneo yao, vinginevyo tutakuwa tunatumia nguvu kubwa kwenye eneo lisilohusika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa maji unaoanzia Kata ya Mwena, Chikundi, Chigugu, Chikukwe na Vijiji vya Maparagwe pamoja na Mbemba. Mradi huu tunashukuru unaendelea vizuri lakini kuna tatizo moja, mkandarasi analalamika halipwi pesa zake kwa wakati mradi unasuasua... (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecil Mwambe. Umeunga mkono hoja? Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nianze kwa kuipongeza Serikali yangu kwa jinsi ambavyo inaendelea kufanya kazi ya kutatua matatizo ya maji katika maeneo mengi. Pamoja na hilo pia nimewasiliza wachangiaji wengi na wengi wao nimewasiliza vizuri sana, naomba tu nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba kinacholalamikiwa kikubwa zaidi kama umewasiliza wachangiaji wengi ni kitu ambacho kwa lugha ya kingereza tunaweza kusema ni *poor project management* ambayo mnayo katika Wizara yako. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani miradi ya maji kwa mfano nikizungumzia mradi wa maji wa Chalinze ambao sasa una miaka zaidi ya 15 kila siku tumekuwa tunazungumzia mradi huo wa maji, Mheshimiwa Waziri nina imani kwamba sasa baada ya kumaliza kuitisha bajeti hii unaweza ukaenda ukaliangalia vizuri hili. Nina imani pia kwamba kuna vijana wazuri wa Kitanzania ambao wamesomea *project management* ambao tukiwapa kazi ya kusimamia *project* hizi wanaweza wakatufanya kazi iliyo nzuri zaidi, lakini utaratibu ule wa kwenda kuwapa hela moja kwa moja Wakandarasi kama ambavyo umefanya pale Chalinze, ndiyo ambao umetufikisha hapa.

Mimi nakuomba sana Mheshimiwa Waziri ambaye ninaamini kabisa kwa *experience* yako kama *Engineer*, msomi mzuri na ambaye uko tayari kuhakikisha kwamba maisha ya watu yanatoka katika taabu wanayoipata naomba jambo hili uliangalie vizuri sana. Nasema hivi Mheshimiwa Waziri ni kwa sababu siyo mara ya kwanza kutoa ushauri mzuri wa namna hii.

Mheshimiwa Spika, nimewahi kutoa ushauri wa namna hii miaka mitatu iliyopita, juu ya kujengwa kwa tekeo pale katika chanzo chetu Wami, lakini miaka yote Mheshimiwa Waziri imekuwa ni uamuzi ambao au ushauri ambao hamkuwahi kuufanya kazi. Faraja yangu leo hii kwenye kitabu hiki katika moja ya jambo kubwa ambalo mnakwenda kulifanya pale Chalinze ni kwenda kutengeneza lile wazo ambalo niliwashauri na kipindi kile nilishangaa kwa nini halikufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo pia nimesoma vizuri kitabu chako cha hotuba ya bajeti Mheshimiwa Waziri. Uharibifu mkubwa unaofanya katika vyanzo vyetu ni kweli lakini katika jambo ambalo sikuliona humu ndani ni nafasi ya mifugo yetu tunayokwenda kunywesha katika vyanzo vyetu na ambayo inapelekea kuharibu vyanzo hivyo. Jambo hilo hamjalizungumza humu ndani, lakini nikupe mfano mmoja wa Chalinze hasa kwa ndugu yangu kule Mheshimiwa Murrad hayupo humu ndani leo, kwamba katika eneo kubwa ambalo linasababisha matatizo ni mifugo ya wafugaji inayopelekwa katika chanzo cha Mto Wami ambayo inapelekea kuingiza matope mengi na udongo mwingi katika maji ambayo ikipeleka kule kwenye tekeo letu liliopo linapelekea panajaa matope na hata pia wakati mwingine maji yale tunashindwa kuzalisha kwa wingi kwa sababu ya uchafu huu ambao unaletwa na mifugo hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hiyo pia Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana kwa hatua kubwa ambazo mmekwishazifanya, Serikali mkishirikiana na Wizara ya Mazingira kwa jinsi ambavyo mnaendelea ku-*preserve* vyanzo vyetu vya maji na kuvifanya vyanzo vyetu viendelee kuwa

salama. Ninaamini kama hamtoliangalia hili jambo la mifugo yetu inayofugwa na kunyweshwa kiholela katika vyanzo vyetu, hata yale mazingira mazuri ambayo mnatengeneza itakuwa nayo ni taabu tupu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo lingine Mheshimiwa Waziri ambalo umelizungumzia kwa ufundu mkubwa zaidi ni usimamizi wa mamlaka za maji. Mheshimiwa Waziri ni ukweli kazi kubwa mnaifanya na maji hayawesi kutoka vizuri kama usimamizi utakuwa *poor*, lakini nikizungumza kwa mfano wa Mradi wa Maji wa Chalinze bado tumeendelea kuwa na taabu kubwa sana katika usimamizi wa maji yale. Imefika kipindi kwamba hata unapotaka kuuliza maswali yanayohusu maendeleo ya mradi ule kumekuwa na sintofahamu kwamba huyu anaweza kukwambia hili, huyu akakwambia hili, lakini haya yote ni kwa sababu nazungumzia tu lile kwamba kutokuwa na utaratibu mzuri juu ya upashanaji wa habari, lakini pia juu ya usimamizi mzuri wa maji yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo pia Mheshimiwa Waziri liko eneo kubwa ambalo nimekuwa na *interest* nalo sana ni katika miradi ya matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Waziri unakumbuka ulipokuja mara ya mwisho wakati nazungumzia juu ya kusuluhisha tatizo la maji Chalinze, tulizungumza juu ya mradi wa maji yatakayotoka Ruvu kwenda Chalinze mpaka maeneo ya Mboga kwenye kiwanda kikubwa kinachoalisha *products* za matunda. Mheshimiwa Waziri mradi ule kwangu ni moja ya miradi ambayo naiona ni miradi ambayo inatupelekea kupata matokeo mazuri katika muda mfupi. Kitu cha ajabu zaidi katika kitabu chako hiki hakuna sehemu ambayo mradi ule umetajwa, labda sijasoma vizuri lakini kwa kuangalia kwangu katika *pages* zinazozungumzia miradi ya namna hiyo ya matokeo ya haraka, mradi ule haupo. Mheshimiwa Waziri naomba utakaposimama utujibu kwamba mradi ule umekufa, mmekataa kuuanzisha au ni nini kinachoendelea ili wananchi wa Chalinze wajue kama tunaendelea kunywa maji pamoja na mifugo katika malambo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja hilo, ninakupongeza sana kwa hatua kubwa unazoendelea kuzifanya hasa ile taarifa ya ukamilishaji wa uchambuzi au upembuzi yakinifu katika Mradi wa Maji wa Kidunda. Mheshimiwa Waziri mradi ule ulipofikia sasa hivi wanachohitaji ni pesa na katika kitabu chako hiki ukurasa wa 57 mmeeleza juu ya matarajio yenu ya kutafuta pesa ili mradi uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika jambo hili naomba tu nikutie moyo na kukupa nguvu zaidi ya kwamba ukamilifu wa mradi ule ndiyo ukombozi wa watu ambao tunategemea sana mradi huu. Bwawa la Kidunda litakapokamilika faida zake kama ulivyoziyeza kwenye kitabu, lakini niwaongezee kwa faida ya Watanzania wengine kwamba maji mengi tunayopoteza yanayokwenda bahrini tutayapunguza. Leo hii ukienda pale kwa mfano kama ukitoka Msata unakwenda Bagamoyo, unaona katika lile Bonde la Mto Ruvu livilyojaa maji mengi sana, maji yale mengi Mheshimiwa Waziri tunayapoteza ambapo kama tungeweza kutengeneza mabwawa makubwa kama la Kidunda, tungeweza kuwa na faida kubwa sana ya kupata maji ambayo wakulima wetu wa Bagamoyo pale wanaotegemea bonde lile wangeweza kufaidika sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, pia tunategemea kupata nguvu ya umeme ambayo pia najua watu wa Chalinze na maeneo mengine ikiwemo watu wa Morogoro Vijijiini tutaweza kufaidika nalo sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikupe moyo na kuendelea kukupa nguvu kwamba jambo hili lisimamie kwa sababu hapa ndiyo unakwenda kuwakomboa Waswahili au Watanzania wanaoishi katika maeneo ya Pwani hususan eneo la Chalinze, Bagamoyo na Dar es Salaam. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa sana maana leo ni siku ya kushauri tu ni eneo la Jangwani. Wengine tunaishi Dar es Salaam pia, eneo la Jangwani hasa katika Bonde la Jangwani pale ambapo kuna Mradi mkubwa wa Mabasi ya Mwendokasi, matope au mchanga umejaa

mpaka umekaribia sasa kufikia *level* ya chini ya daraja. Ninavyofahamu kwa udogo wake, kwamba mchanga au matope yakijaa maana yake maji yatapita juu ya matope yale na ndiyo jambo ambalo limepelekeo leo hii bonde lile panaponyesha mvua hata ya millilita mia moja yanapita juu ya daraja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mmeandika vizuri katika kitabu chenu kwamba sasa mnataka kutafauta kujenga mabomba makubwa ambayo yatasafirisha maji taka. Bonde la Jangwani sidhani kama linahitaji mabomba makubwa ya kusafirisha maji taka. Bonde la Jangwani linachohitaji ni *master plan* nzuri ambayo inaweza ikasaidia kutatua tatizo lile moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii ukija na hadithi ya kutengeneza mabomba unachozungumzia ni kutafuta maji yapite wapi, tatizo la Jangwani siyo maji yapite wapi, tatizo la Jangwani kwamba watu wamejenga, wameziba njia, wameharibu miundombinu na wameharibu mazingira. Kinachotakiwa ni kutengeneza *master plan* mpya ambayo itahakikisha kwamba maji pale yanapita vizuri kufika katika Bahari yetu ya Hindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miaka minne kama siyo mitano iliyopita alikuja mama yangu Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka akatupa mpango mkakati juu ya jinsi gani wanataka kutengeneza Bonde la Jangwani ili liweze kuwa sehemu nzuri ya kivutio, lakini pia liweze kutumika kwa ajili ya kupitisha maji, mpango ule sijui ulifikia wapi. Taarifa nilizonazo ni kwamba ulikataliwa lakini pamoja na kukataliwa huko kuna kitu cha muhimu cha kufanya ambacho Mheshimiwa Waziri nina uhakika kabisa unajua na wewe nina hakika umetembea.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa London wametengeneza mto wao pale ambao unaitwa *River Thames* ambao unapita katikati ya Jiji la London, umekuwa ni sehemu ya kivutio na sehemu nzuri, leo hii London hawana wasiwasi wa kupata mafuriko, tunashindwa nini kutengeneza

Bonde la Jangwani lile kutoka katika maeneo ya Tabata mpaka kwenye Daraja la Salender ili maji yaende baharini na maji yanayotoka baharini, na maji yanayotoka baharini hata ikiwezekana baadae huko kama nchi itakuwa imepata mambo mazuri zaidi ikiwezekana tutengeneze *boats* nazo ziweze kupita pale zipeleke watu mpaka huko Tabata na iwe sehemu ya kivutio pia katika maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo la mabwawa, Mheshimiwa Waziri naomba nikukumbushe wakati Mheshimiwa Maghembe, Mbunge kwa sasa akiwa Waziri wa Wizara yako, Serikali ilibuni mradi wa kutengeneza bwawa kubwa la maji katika Kijiji chetu cha Mjenge kule Kibindu, Chalinze. Bwawa lile lilikuwa ni *substitute* ya mradi wa maji wa Wami – Chalinze, mradi ambao kwa mujibu wa mchoro wake ulikuwa haufiki katika eneo la Kata ya Kibindu. Mheshimiwa Waziri nimejaribu kutazama kitabu chako hiki, katika hotuba ya mwaka jana bwawa hilo limetajwa, lakini mwaka huu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani dakika zako zimeisha.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja naomba bwawa hili nalo lifanyiwe kazi, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Lulida, tafadhalii.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi hii kuchangia hoja ili yopo mezani.

Mheshimiwa Spika, sina matatizo na Waziri, Naibu Waziri wala Katibu Mkuu hawa ni wageni, mimi kila nikzungumza nazungumza tuwe wazalendo kwa nchi na Taifa letu. Tukiangalia pesa na mikopo mbalimbali

inayotumika kwa ajili ya maji, tukatathmini na maji yaliyopatikana kwa kweli ni mtihani mzito sana kwa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia kwanza Manispaa ya Lindi na Mradi wa Maji wa Lindi mpaka Mheshimiwa Rais alipata hasira kutaka kumtia ndani yule *consultant*. Jambo la kushangaza taarifa atakayoambiwa Waziri ataambiwa Lindi kuna maji wakati Lindi hakuna maji. Ule mradi unatia huruma na huzuni kwa nchi hii, zimetumika pesa za mkopo lakini akaunti imefunguliwa India siyo Tanzania. *Consultant* anakaa India, anatoka India kwa mwezi kuja kuangalia mradi Lindi na anafikia katika mahotelii makubwa anatumia gharama kubwa lakini gharama zile zipo ndani ya huu mradi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukifikiria huu ni mkopo, wao wanatumia gharama nydingi sana kuliko hata uwekezaji wenyewe wa maji, sasa hasara hii nani mnataka abebe? Hii ndiyo miradi yote ya maji unayiona Tanzania imefikishwa hapo, kuiingiza nchi katika dhahama wakati wao ndiyo wanafaidika hapa tunaendelea kubeba mikopo mikubwa ambayo haina faida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa Mjumbe wa Bodi ya Maji Lindi, mradi wa kutandika mabomba alipewa *Ms Jandu*, amechukua mara ya kwanza shilingi bilioni saba kutandika mabomba ya maji yakapasuka, akaomba tena bilioni sita ikawa shilingi bilioni 13. Leo ninachokuaambia Lindi ukifungua maji yale mabomba yanapasuka, Serikali inaingia tena mzigo wa pili kwa kutengeneza mabomba na siyo kumuadhibu yule mkandarasi. Jamani tunakwenda wapi, huyu mkandarasi yupo na amepewa tena ndiyo miradi miwili wa Chalinze na wa Lindi, miradi hii yote miwili haifanyi kazi, wenyewe wanakaa India, kila kitu India na akaunti India. Hii ndiyo mikataba mibovu ya maji! Haimuhusu Waziri Kamwelwe wao wanaohusika ndiyo watajua kwa nini wanatuingiza katika mikataba ambayo nchi inapata *frustration* ya kutosha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiiangalia miradi hii ya mikopo ya *World Bank* Tanzania nzima utaona ni kafara, kafara hii itawaangukia hawa ambao mwanzo wala mwisho. Tulipewa semina ya jinsi Watanzania tunavyopata tatizo katika masuala ya miradi. Tupo vizuri kuandika *feasibility study*, kufanya *strategic plan, action plan* na *commitment* lakini tupo *poorkatika management*. Ameizungumza Mheshimiwa Ridhiwani kwa kweli usimamizi mbovu hata kama tutawaleta shilingi bilioni 500 bado maji hayatapatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kitabu hiki nimeona cha Wizara ya Maji wanasema tuna upungufu wa wataalam kwa vile wale watalaam wa zamani wamestaifu, sasa hata kama unapeleka pesa hauna wataalam kuna nini tena hapo? Ina maana wewe unachukua pesa unapeleka kwa watu ambao siyo wataalam, matokeo yake zile hela zitafujwa na wananchi watakuwa hawapati maji. Tathmini yake ni kuwa hizi hela mnazozipeleka kwa vile hakuna wataalam, hakuna maji, aibu. Tufike mahali tuijulize tumekwama wapi, tumenasa wapi. Suala la kusema tunaomba pesa sikatai ombeni pesa, lakini je hizo pesa zitafanya kazi iliyoandalisha? Hamna wataalam mnazungumza na kama hamna wataalam kila siku mlikuwa wapi msiseme suala la wataalam, mnafika mahali sasa hivi mnapigana na hela lakini hela ile mkiitoa hamna mtaalam, yale maji yatapatikana wapi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tulipata miradi ya *World Bank* katika vijiji pamoja na Mradi wa Sabodo, jambo la kusikitisha nenda Mchinga hakuna maji, ina maana *surveyor* na mchimbaji ni watu wawili tofauti, hawana ushirikiano na matokeo yake maji yamekwenda kila walipochimba maji Mvuleni, Mchinga, Kilangala na Chikonje hakuna maji. Hivyo, tena wanatafuta pesa zingine kupeleka kwa ajili ya maji wakati hela zilishapelekwa, hii ni *double standard* inafanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, inanisikitisha kujiuliza suala la maji unasema unataka kumkomboa mwanamke, hata wanaume

wanaweza kujitika maji maana haiwezekani kuleta kuwa lazima maji ajitwike mwanamke, hapana vilevile wanaume wanayo haki ya kuchota maji lakini suala la kujitwika maji na kukomboa maji ni lazima liwe la kila Mtanzania lakini uwepo uzalendo kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la mazingira na tabianchi, nimehudhuria mikutano ya mazingira na tabianchi. Kwa vile Serikali haioni umuhimu hakuna wawakilishi wanaokwenda kuhudhuria mikutano ya mazingira na tabianchi (*climate change*). Nimekwenda mwaka jana na mwaka juzi hakuna Waziri aliyewakilisha, nchi nzima haina uwakilishi sasa utapate taarifa ya *climate change* ili angalau muweze kuangalia nini tufanye, haya maporomoko ya maji yanásabishwa na nini ina maana hamtaki kujifunza vitu ambavyo baadae vitakuja kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unakuta kuna mradi unatakiwa shilingi bilioni 500, nakubali lakini kuna kitu kinaingia ndani yake kwanza *consultant* na *ma-expatriate* wanatoka India wanaingia ndani ya huo mradi, matokeo yake wao peke yake watatumia karibu shilingi bilioni 100, sasa hata kama utaniambia nalipa ile riba kwa miaka 20 lile deni ina maana kila mwaka mimi nikilipa shilingi bilioni 25 mwakani ita-subsidize itabakia pale pale, ule mradi utachukua hata miaka 50 Serikali hii haiwezi kulipa lile deni na itakuwa ni madeni ya kudumu kila siku tunaingia katika madeni ambayo hayalipiki.

Mheshimiwa Spika, kama mdau naomba andaa Tume Maalum ikaangalie kuna nini kwenye maji, mikataba yao na usimamizi wao uje utupe ripoti hapa tuweze kuichangia tuweze kujadili. Masuala ya kumuingiza mbuzi ndani ya gunia ukaniletea mbuzi sokoni mimi silielewii. Mara nydingi tunafanya miradi wanasema mikataba sikuoneshi, kama hata Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo haioni mikataba hii inasema nini, mnatuambia nini hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mikataba imefichwa na kama imefichwa kinachoendelea ni nini, ni kuhakikisha nchi inaingia katika dhiki kubwa ya maji lakini hela zinaliwa na wageni.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hapo nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Lulida kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki ni mdogo sana tutaendelea jioni, niwahakikishie wote ambao wapo kwenye orodha za pande zote watapata nafasi ya kuchangia bajeti hili muhimu kabisa kwa ajili ya wapiga kura wetu, Bajeti ya Maji. Kwa hiyo, tukutane tena saa kumi na moja jioni ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali – Wizara ya Maji na Umwagiliaji 2018/2019**

(*Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA:** Tunaendelea na uchangiajiji, tunaanza na Mheshimiwa Selemani Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa William Ngeleja. Mheshimiwa Zedi, tafadhali.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa jitihada kubwa inazofanya kuhakikisha kwamba tatizo la maji katika nchi yetu linapatiwa ufumbuzi na kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata maji safi na salama kama ambavyo tumeahidi kwenye llani yetu ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa maji, hasa maeneo ya vijijiini bado siyo nzuri na hairidhishi. Nashauri kwamba namna ambavyo tunapima upatikanaji wa maji kuna haja ya kuangalia kama upimaji huu unatupa *figures* ambazo ni sahihi. Tunasema kwamba upatikanaji wa maji sasa hivi maeneo ya vijijiini ni asilimia 58 lakini ukienda maeneo ya vijijiini kwenye majimbo yetu jinsi hali ya upatikanaji wa maji ilivyo ukiwaambia wananchi upatikanaji wa maji ni asilimia 58, wananchi wanakushangaa. Hali haiko vizuri kabisa na nadhani kuna haja ya kupima kupata hali halisi badala ya hizi takwimu ambazo kimsingi hazioneshi picha halisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nadhani namna wanavyopima hii *percentage* ya upatikanaji wa maji wanaangalia tu fedha zilizotumika kujenga miradi ya maji na kwamba miradi hiyo ingehudumia wananchi wangapi lakini kimsingi kuna miradi mingi fedha zimetumika, imejengwa imefika mwisho lakini haitoi maji na haimnufaishi yejote.

Mimi Jimboni kwangu kuna miradi miwili ya tangu wakati ile ya Benki ya Dunia, miradi kumi kila Wilaya, kuna miradi mikubwa zaidi ya milioni 400/400 karibu shilingi bilioni moja imetumika lakini mpaka leo miradi ile haitoi maji, wananchi hawanufaiki. Kwa hiyo, katika mahesabu ya wananchi wangapi wamenufaika na yenewe utakuta inahesabiwa. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kuwa na hesabu za uhakika kuliko kuwa na *figure* ambayo ina-*mislead*; tunasema asilimia 58 maeneo ya vijijiini, lakini kimsingi maeneo hayo bado yako chini sana kwa upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia ukurasa wa 130, Halmashauri yangu ya Nzega imepatiwa shilingi milioni 884

kama fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji vijiji, lakini kama Halmashauri nzima ni shilingi bilioni 2.6 nyingi ni fedha za nje, za ndani ni shilingi milioni 884. Kwa hali halisi ilivyo ya tatizo la maji fedha hizi ni ndogo mno na najua bila fedha hakuna chochote unachowea kufanya. Kwa hiyo, nashawishika kuunga mkono pendekezo la kuongeza shilingi 50 kwenye bei ya lita moja ya dizeli na petroli ili tupate fedha za kutosha na Halmashauri zetu zipangiwe fedha za kutosha. Hii shilingi milioni 884 kwa mwaka mzima kwa Halmashauri kubwa kama ya Nzega yenye vijiji zaidi ya 167 ambavyo vyote vina hali ngumu ya upatikanaji wa maji, kwa kweli mimi naona hazitatuifisha popote pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Wizara na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kuyafikisha Tabora Mjini ambayo yanapita pia Wilaya ya Nzega na baadae yata-*branch* kwenda Igunga. Huu ni mradi mkubwa, zaidi ya shilingi bilioni 600 zitatumika, siyo jambo dogo, ni jambo kubwa sana. Rai yangu hapa tu ni kwamba usimamizi wa makini unahitajika ili ujenzi wa mradi huu uende kwa spidi ambayo inatakiwa na muda ambaao tumewaaahidi wananchi kupata maji waweze kupata maji. Kwa sababu zaidi ya vijiji 110 na wananchi zaidi ya milioni 1.1 ndani ya Mkoa wa Tabora watafaidika na maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba sisi watu wa Nzega na hasa Mkoa wa Tabora kwa ujumla tunaangalia maji haya yanayotoka Ziwa Victoria yatakapofika Tabora; Nzega – Tabora – Igunga, sisi haya ndiyo yatakuwa chanzo sasa cha maji kuyatoa yalipofika kuanza kusambaza maeneo mengine. Kwa sababu Mkoa wa Tabora na hasa Wilaya ya Nzega, tuna tatizo la kupata maji chini ya ardhi, visima vingi vinachimbwa hata ukipata maji lakini ni machache ambayo kiangazi visima karibu vyote vinakauka.

Kwa hiyo, tuna shida ya maji chini ya ardhi, sasa maji ya Ziwa Victoria yakishafika Nzega tunayachukulia kama ndiyo chanzo sasa, kuanzia pale tutaanza kuyasambaza kuingiza ndani na kwenye vijiji vingine. Kwa hiyo, tunachukulia

maji ya Ziwa Victoria kama kitakuwa chanzo muhimu cha kutupatia maji sasa na kuyasambaza kuelekea maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara hapa kuwe na *flexibility* kidogo. Sasa hivi Halmashauri ya Wilaya ya Nzega tuna shilingi bilioni tatu za miradi mikubwa ya visima vyta maji, lakini mkandarasi tuliyemba kazi amechimba visima karibu 26 lakini visima ambavyo vimepata maji ya wingi wa lita 4,000 kwa saa ni visima vitatu tu kwa sababu ni shida sana kupata maji chini ya ardhi. Kwa hiyo, kuna hofu kubwa tarehe 30 Juni itafika hela hazijatumika na zitapaswa kurudi na zinarudi siyo kwa sababu ya uzembe wa Halmashauri kutozitumia lakini kwa hali halisi na *nature* ya Nzega maji chini visima vimechimbwa vyta kutosha lakini vyote hakuna maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hapa *flexibility* ya Wizara kwamba fedha hizi sasa badala ya kutumika kutafuta maji chini ambayo hayapo zitumike kwa usambazaji (*distribution*) kutoka kwenye vyanzo vyta mabwawa na hapo ambako maji ya Ziwa Victoria yatafika. Kwa hiyo, naomba *flexibility* hiyo Wizara ijaribu kuiangalia. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kidogo kuhusu skimu za umwagiliaji. Kwangu mimi naona hii ni *solution* ambayo itafanya wananchi wetu ambao hawana uhakika wa maji wawe na kilimo cha uhakika kwa kuwa na mabwawa ya umwagiliaji. Halmashauri ya Wilaya ya Nzega tumepata mabwawa mawili ya Kahama Nhalanga na Lusu, kazi imekamilika, wananchi wameanza kunufaika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ni kubwa mno, vijiji 167, vijiji viwili tu kupata mabwawa haitoshi. Tunapenda mabwawa haya watu wa Mambali ambako tathmini ilifanyika kuna uwezekano wa bwawa kubwa kujengwa lijengwe; watu wa Kasela ambako tathmini imefanyika kuna uwezekano wa bwawa kujengwa, lijengwe; watu wa Mwangoye na vijiji vingine vingi tu ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ambavyo tathmini za

mabwawa makubwa ya umwagiliaji zilifanyika na zinasubiri tu pesa ni vema mabwabwa yakajengwe. Kwa hiyo, naiomba Wizara ijaribu kufanya upendeleo maalum kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kwa sababu ni halmashauri kubwa, ina viji vingi na mtawanyiko wa mvua siyo mzuri, haya mabwawa yatatusaidia katika kuhakikisha kwamba tunapata kilimo cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nisisitize tu kwamba Serikali ikubali ombi la Waheshimiwa Wabunge la kuongeza hiyo shilingi 50 kwenye bei ya lita ya petroli na bei ya lita ya dizeli. Tuumie sasa lakini tunaumia kwa ajili ya manufaa ya kupata fedha ziende kwenye miradi ya maji ili wananchi wetu waweze kunufaika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la msingi tu hapa ni kwamba fedha hizi kweli ziende kwenye miradi ya maji na iwe maji vijijini. Tunafahamu kwamba miradi mikubwa ya maji maeneo ya mijini hasa miji mikubwa ya Dar es Salaam, Arusha na miji mingine ina vyanzo vingine vya fedha, kwa hiyo, hizi fedha za tozo ya mafuta ziwe ni za maji vijijini siyo maji mijini...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa William Ngeleja atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Nami naanza kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Waziri pamoja na Wizara kwa ujumla kwa hotuba yao nzuri, lakini pia na mipango ambayo wameonesha katika hotuba yao.

Mheshimiwa Spika, katika maisha ya mwanadamu hakuna jambo lisilokuwa na changamoto, lakini kiukweli kabisa ukifuatilia utendaji kazi wa Wizara kwa sasa pamoja na wasaidizi wao, unaungana tu na wanaosema usipokuwa muungwana hutakubali hata kidogo unachokipata, lakini ukiwa muungwana utasema ahsante. Tunazungumza hapa lakini kila mmoja anazungumzia eneo lake na ndilo lenye uzoefu kuonesha namna ambavyo mipango ya Serikali kuititia Wizara hii ilivyosimama vizuri ama kama ina kasoro zinazohitaji kufanyiwa maboresho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Profesa Kitila Mkumbo na Naibu Katibu Mkuu Injinia Kalobelio, nikitambua *staffnzima* ya Wizara ya Maji nimitaje Mkurugenzi wa Maji Vijijini, kaa sijakosea *Engineer* Mafuru. Kwa wale ambao tumepata nafasi ya kufanya nao kazi utakubali kwamba wanajitahidi kwa kadri inavyowezekana kuisukuma sekta hii kuisogeza mbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu mimi ni mionganoni mwa watu wanaotoa ushahidi wa kuona kwa sababu nimekaa nao na nimeona *reflectionya* yale ambayo tumeyazungumza wakati tunafuatilia miradi kwenye hotuba hii. Hapa nazungumzia kuona utekelezaji wa visima vya Vijiji vya Nyamililo, Mlaga, Imlalamawazo, Nyamatongo, Kinyenye, Ishishang'olo, kule Sengerema sasa, maana yake hapo nazungumzia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema. Hivi ni visima ambavyo nimeahidiwa baada ya kufuatilia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia naona kuna miradi ambayo inatekelezwa kutokana na chanzo cha Ziwa Victoria. Hapa nauona Mradi wa Buyagu, Kalangalala hadi Bitoto nakotoka mimi.

Pia naona Mradi wa Chamabanda kwenda Nyandakubwa, ni mambo ambayo tumezungumza nao yameingizwa kwenye mpango na hatimaye tunaiona taswira ya hotuba ikiwa imezingatia haya ambayo tumezungumza

nao. Ndiyo maana nasema wanachokistahili tuwape, lakini kwenye changamoto tuwasaidie kuboresha mazingira ya kazi yalivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kule Sengerema pia tumepata bahati, Sengerema tuna hadhi ya Mamlaka ya Mji na tuna mradi mkubwa wa maji ambaeo Mheshimiwa Rais mwaka jana aliuzindua tarehe 4 Julai. Ni mkubwa kiasi kwamba wana mitambo ambayo mpaka sasa hivi hatujaweza kuitumia kwa ukamilifu. Kwa kuzingatia hilo, tumekuwa na mipango ya kupanua miundombinu iwafikie wananchi wengi zaidi katika vijiji vingi zaidi. Hapa nauona mradi huo ukiwa umetengewa fedha kwa ajili ya kuuboresha kuwafikishia wananchi maji katika vijiji ambavyo mitambo ama miundombinu ya mradi huo inapita. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri nasema imeandaliwa kutokana na mambo mengi, moja ni llani ya Chama cha Mapinduzi, Mpango wa Maendeleo Awamu ya Pili, pia umezingatia ahadi na maelekezo ya viongozi wetu wakuu na hapa nazungumzia kuanzia Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Sengerema liliivyo tuna bahati ya aina yake, Rais wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, anapokwenda Chato kama anatokea Mwanza lazima atapita Jimbo la Sengerema. Kwa sababu ni Mheshimiwa Rais aliyechaguliwa kutokana na kura za wananchi ni utaratibu wa kawaida kila anapopita anazungumza na Wanaserema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Sengerema tumbahatika kupata ugeni wa Mheshimiwa Rais mara mbili toka achaguliwe na amezungumza na wananchi pamoja na mambo mengine amezungumzia habari za maji, ameahidi kufikisha maji katika baadhi ya maeneo. Nawashukuru wataalam na Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo wamekuwa wakifanyia kazi ahadi ambazo Mheshimiwa Rais ametoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nazungumzia mpango wa kufikisha maji kwenye Kijiji cha Nyampande ambacho Mheshimiwa Rais aliahidi, lakini pia naona mipango ya kufikisha maji kwenye Vijiji vya Sima, Tunyenye, Nyamililo pamoja na Nyamahona ambako ndio chanzo cha maji kinaanzia. Naishukuru sana Serikali kuititia Wizara hii kwa namna ambavyo imezingatia ahadi ya Mheshimiwa Rais na inaonekana katika hotuba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukipitia majedwali ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 124 unaelezea fedha ambazo zimegawiwa katika halmashauri mbalimbali kusaidia miradi ya maji vijijini. Naishukuru Serikali kwa sababu Sengerema tumepagiwa shilingi 1,700,000,000. Ahsanteni sana kwa kutusikiliza na kuzingatia hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ambayo yanakwenda kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kwa Watanzania. Kwa sababu miradi hii itakapokamiliika kwa hakika kwa vyovyyote vile tutakuwa tumefaidika.

Mheshimiwa Spika, lakini nauona Mradi wa Nyasigu, Lubungo, Ngoma A ambao sasa hivi mchakato wake unaendelea, Serikali mlishatupa kibali, tenda ilishatangazwa, tunakamilisha taratibu za kupata mkandarasi. Nauona Mradi wa Chamabanda/Kasomeko; nauona Mradi wa Kamanga/Chinfunfu na hapa ndipo napompongeza sana Mkurugenzi wa Maji Vijijini, *Engineer Mafuru*, ametusikiliza, ametuma wataalam wamekuja kufanya upembuzi wa awali na hatimaye wameonesha kwenye mipango yao ya utekelezaji. Kwa hiyo, sisi Sengerema tunasema ahsante sana, kwa hapa mtakuwa mmetusaidia kupunguza adha ya Watanzania kwenye kiwango cha maji wanachokipata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali, ukisoma ukurasa wa 189 utakuta Miji ya Sengerema, Nansio na Geita tumetengewa shilingi bilioni 4.7 na huu ni mwendelezo wa miradi ambayo imekuwa ikitikelezwa katika miji ambayo inazunguka Ziwa Victoria. Ninachokiuliza na naomba Serikali mfanue mtakapokuwa mnafanya majumuisho, katika utatu

wetu huu, huu mgawanyo wa shilingi bilioni 4.7 umesimamaje, Sengerema sisi chetu ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kitabu hapa kinavyoonesha mmetufunga wote watatu, mnasema ni shilingi bilioni 4.7. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe ufanuzi ukurasa wa 189; Nansio wanapata kiasi gani huko Ukerewe, Geita wanapata kiasi gani na sisi Sengerema tunapata kiasi gani ili iwe rahisi kufuutilia kujua Wanaseremana wanastahili kiasi gani na tunachokistahili kuwafikishia wananchi kwa sababu hizi fedha zinakuja kuendelea kuboresha hudumaya maji katika Mji wa Sengerema na vijiji vyake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumezungumza kwa mtazamo tofauti hapa Bungeni. Tupo tunaoamini kwamba changamoto kubwa iliyopo katika Wilaya hii siyo fedha isipokuwa ni utekelezaji na tupo tunaoamini kwamba fedha ni tatizo. Mimi naamini kwamba pamoja na yote yanayofanya lakini bado kuna ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, tuna taarifa hapa ya Kamati inaonyesha kiwango cha fedha ambacho kimeshatoka kwenye miradi ya maendeleo kinatofautiana na ambacho kimesemwa na Mheshimiwa, tunaoamini Mheshimiwa Waziri atakuja nalo. Taarifa hizi zinavyosema ni mpaka tarehe 31 Machi, lakini leo ni tarehe 8 Mei, inawezekana Serikali labda ina taarifa za hivi karibuni hatujui lakini watasema wao.

Mheshimiwa Spika, nachotaka kusema kwa vyovytile fedha hizi hazitoshii kutufika kwenye lengo letu la kufikisha maji mijini asilimia 95 na vijiji asilimia 85 mwaka 2020. Kwa hiyo, lazima tufanye yale ambayo tunaona yanaweza kutufikisha mbali.

Moja ni hilo ambalo tumekuwa tukisema, naungana na taarifa ya Kamati kwamba tuongeze shilingi 50 kwa mara nyingine kwenye mafuta ya dizeli na petroli. Tulifanya mwaka jana zimepatikana fedha kiasi fulani na zimetufikisha pazuri na sasa naomba tena tufanye hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukisema hapa, tulivoanzisha Wakala wa Umeme Vijiji ni tulifanikiwa sana na hivi karibuni kwenye barabara tumetengeneza *TARURA* na hapa tulisema tuanzishe Wakala wa Maji Vijiji ni, tunaomba hili jambo likamilike. Najua Serikali inasema kwamba mchakato wa kuanda wakala huo unaendelea, tunaomba basi ifanyike haraka ili tuone manufaa tuliyoyakusudia kwa sababu tunaamini tukiwa na wakala unaosimamia maji vijiji ni tutafika mbali zaidi kwa kasi kubwa kuliko ilivyo sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu skimu za umwagiliaji, narudia hoja yangu ya kila mwaka, ukisoma hata *Hansard* utaona, nadhani Wizara ya Maji mnanisikia vizuri, tumeongea na watendaji, sina hakika kama mnayo *inventory* ya miradi ambayo Serikali ilishaianzisha lakini ikakwama na haiendelei. Kwangu wamesema kuna huo Mradi wa Katunguru, kwa nini fedha mlizoziveka pale shillingi milioni 700 hamuongezi tuukamilishe kwa sababu ulikuwa unahitaji shillingi bilioni 2.5.

Mheshimiwa Spika, nimepata maelezo kwamba wanafanya uchambuzi kwanza waone hatua za kuchukua, nasema kwa niaba ya wananchi wa Sengerema tukamilishe uchambuzi huu haraka halafu mradi uendelee kwa sababu shillingi milioni 700 zilizowekwa pale ni kama zimetupwa na sisi hatuamini kama Serikali ilikuwa nia ya kutupa fedha hizo. Kwa hiyo, naomba sana huu Mradi wa Katunguru tuukamilishe.

Mheshimiwa Spika, mawili ya mwisho, moja, taarifa katika ukurasa wa 97 Serikali imetukumbusha Waheshimiwa Wabunge hapa madeni ambayo taasisi zake zinadaiwa na hasa hizi Mamlaka za Maji kwenye maeneo mbalimbali imewasilisha madeni hayo Wizara ya Fedha ili yalipwe juu kwa juu. Nazungumza hili nikikumbushia kilichotokea mwishoni mwa mwaka jana na mwazoni mwaka huu, Halmashauri nyingi ziliathirika ikiwemo Sengerema, wananchi waliadhibiwa na kama tunavyofamu hakuna fidia, wananchi wameumia kwa makosa ambayo hayakuwa ya kwao. Kwa yale madeni ya Serikali tunaomba jambo lile lisijirudie na niipongeze Serikali kwa kuonesha hapa. (*Makofii*)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa siyo kwa umuhimu, miradi mingi hapa tunalalamika Waheshimiwa Wabunge siyo kwa sababu haina wakandarasi mingi ina wakandarasi lakini *certificate* walizonazo ambazo wamekuwa wakizileta kwa utaratibu wa kawaida wapate huduma waendeleze kazi zile hazijalipwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngeleja, tunakushukuru sana.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, naomba *certificates* ambazo zimeshaletwa Wizara zilipwe ili miradi iendeleee.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.  
*(Makof)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omary Mgumba atafuatiwa, twende CHADEMA sasa, Mheshimiwa Frank Mwakajoka na Qambalo Willy, dakika tano tano. Mheshimiwa Mgumba, tafadhalii.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu katika Wizara hii muhimu ya Maji. Nichukue nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya na uzima tumekutana jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, hakuna ziada mbaya na mimi niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara Profesa Kitila pamoja na watumishi wote wa Serikali katika Wizara hii kwa juhudini kubwa ambazo wanazifanya kwa kuwaleta maji wananchi wa Tanzania. Wote ni mashahidi tumeona kwamba wanachapa kazi na wanatembelea sehemu mbalimbali kujua changamoto za Watanzania lakini changamoto kubwa ni upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, pia niishukuru Serikali kwa miradi mbalimbali inayoendelea katika jimbo langu katika vijiji vichache. Pia nimeona humu nia ya Serikali kulijenga Bwawa la Kidunda, niipongeze sana na nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutimiza ndoto za Mwalimu Nyerere za miaka ya 1960 ambazo anazitekeleza sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali, Kidunda siyo mara ya kwanza kuiona kwenye vitabu, nimeiona mwaka juzi wakati nikiwa mwaka wa kwanza hapa Bungeni, nimeona mwaka jana nikiwa mwaka wa pili hapa Bungeni na mwaka huu pia nimeiona, lakini utekelezaji wake haufanani na kinachoandikwa. Niwaombe sana mwaka twende tukatekeleze mradi huo, ni mradi wa miaka mingi na una manufaa makubwa sana katika nchi yetu hasa kwa upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, Pwani na Morogoro hasa kwa hivi viwanda vyetu kuwa na uhakika wa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii ni mipango ya muda mrefu ya Mwalimu Nyerere, nikikumbuka pale Morogoro alivyotujengea viwanda zaidi ya 11 kutoka msaada wa *World Bank* alijenga na Bwawa lile la Mindu kwa ajili ya ku-supply maji. Kwa hiyo, tunafuata nyendo zake hata huko aliko anafurahia namna gani Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anatimiza ndoto zake alizoziacha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi na shukrani hizo, nianze kuomba maombi ya kwenye jimbo langu. Kama nilivyo sema kuna miradi michache inatekelezwa lakini kuna mambo mbalimbali niwaombe. Kuna Mradi wa Chalinze III, ni mradi wa kabla mimi sijakuwa Mbunge tangu 2009, tulipata vijiji saba, miundombinu yote ilijengwa tangu 2009 lakini mpaka leo hiyo miundombinu imeshakuwa chakavu na imeanza kubomoka hatujaweza kupata maji. Mheshimiwa Waziri unapokuja kufunga hoja yako tunataka majibu ya Chalinze III maji yatatoka lini? Mwaka jana ulisema kuna mambo mnayafanya mchakato unafikika mwisho lakini tumebakiza miezi miwili kumaliza hii bajeti bado hatuna matumaini Chalinze III itaanza kutoa maji lini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia katika Chalinze III hiyo hiyo kuna vijiji vitatu ambavyo vilisahaulika kujengewa miundombinu yake ambavyo ni Gwata, Masewe na Lubongo. Tunaomba sana hizo hela tukamalizie hiyo miundombinu ili ikianza kutoa maji Chalinze III na sisi pale tupate maji.

Mheshimiwa Spika, pia katika Tarafa ya Ngerengere karibu kata zote hatuna maji safi na salama. Niombe wataalam wa Wizara na Halmashauri waje wafanye utafiti wa kupata maji ardhini ili tuweze kupatiwa visima katika zile kata ambazo haziwezi kufikiwa na vyanzo vya maji vya mserereko ambavyo tunavyo kule Morogoro. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi kuungana na wenzangu wengi waliopendekeza kwamba tuongeze shilingi 50 katika tozo ya mafuta kwa ajili ya kuongezea Mfuko wa Maji ili tuweze kusambaza vizuri maji huko vijijini. La pili niungane na wenzangu pia waliopendekeza kwamba Wakala wa Maji Vijijini ianzishwe.

## TAARIFA

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgumba kuna taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAKUKA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa muongeaji, pamoja na kwamba Wabunge wanaendelea kupendeza shilingi 50 iongezwe kwenye maji hii siyo kipaumbele cha Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu ziko pesa ambazo zimetengwa kama vile pesa za *UCSAF* zimeondoka na *export levy* kwenye korosho zimeondoka. Kwa hiyo, kutenga siyo sababu, ni nini kipaumbele cha Serikali ndiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nampa hiyo taarifa. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgumba taarifa hiyo.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana ndugu yangu, lakini nikuombe wewe muda wangu uutunze ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu kwenye Wizara hii. Suala la *export levy* tutakuja kulijibu Wizara ya Kilimo ikija hapa, lakini sasa tunazungumzia masuala ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nikubaliane na wenzangu ambao wanataka tuanzisha Wakala wa Maji Vijijiini, lakini naomba nitofautiane kidogo au nitoe mawazo yangu kidogo. Tukianzisha wakala huu sasa hivi kabla hatujauja miradi ya maji imekwama wapi tutarithisha matatizo kutoka katika Mamlaka za Maji zilizoko sasa hivi na kupeleka kwenye huo wakala mpya.

Mheshimiwa Spika, pendelekezo langu, kabla ya kuanzisha wakala huo, ni vizuri ama Serikali au wewe au CAG afanye ukaguzi maalum katika miradi yote ya maji nzima ili tubaini tatizo la miradi hii kutekelezwa chini ya kiwango au miradi hewa ni nini? Baada ya hapo wakija na majibu na mapendelekezo ndiyo Serikali ichukue na sisi Wabunge tutakuwa na uelewa mpana wa kuishauri Serikali kutoka hapa kwenye mkwamo twende wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Miradi mingi ambayo ilikuwa inaanizisha na kandarasi nyingi watu walikuwa wanapeana kiujanaujanja. Wakandarasi waliokuwa wanapewa hawana sifa wala vigezo, kwa sababu ni mtoto wa mjomba au mtu kwa sababu ana fursa hiyo iko pale anaanzisha kampuni yake, anamwambia ndugu yake weka hapa *tender anashinda*, uwezo hana, vifaa hana na ndiyo maana mpaka sasa hivi tuna miradi hewa na miradi mingine huko maji hayatoki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kabla hatujaunda huu Wakala wa Maji ni vizuri kabisa kwanza tukabaini matatizo ni nini, nani alihusika na majina yao bila kujali vyeo vyao, yawe wazi ili tuisaidie Serikali tuondoke kwenye mkwamo huu wa maji tuliokwama. (*Makofii*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Ester.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa Mheshimiwa mchangiaji na mchango wake mzuri sana kwamba moja ya hao watoto wa vigogo ni mtoto wa Stephen Masato Wasira ambaye alipewa Mradi wa Mgeta Nyangaranga wenye thamani ya shilingi milioni 800 umekamilika na mpaka sasa hivi maji hayatoki. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgumba, endelelea.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Hiyo taarifa kwa sababu haina ushahidi wala uhakika nikiichukua atanirushia kesi ambayo haihusiki hapa, twende kwenye kuchangia maji tu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu washauri elekezi wa miradi ya maji, hiki ni kichaka kingine cha kutafuna fedha. Utakuta mradi wa maji wa kisima kimoja mshauri elekezi anatoka Arusha, Dar es Salaam ndiyo anakuja kusimamia kwenye halmashauri. Ushauri wangu kwa Serikali kwa sababu wana wataalam wao ndani ya Halmashauri na mkoa hata kwenye Mamlaka ya Maji, kwenye miradi hii midogo midogo ni vizuri washauri elekezi wakatumwa hao watumishi wa Serikali ili kuokoa fedha nydingi na hawa washauri elekezi wakatumika kwenye miradi mikubwa tu kama Kidunda, Chalinze III na mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, tunalumbana hapa tatizo ni sababu ya pesa kidogo na niipongeze sana Serikali kwa kuja na mikakati ya kujiongezea pesa. Tunafahamu biashara ni uwekezaji na katika uwekezaji huo inayotuingizia mapato mengi kuliko yote ni kilimo asilimia zaidi ya 25 lakini ya pili ni utalii, watalii wanaongezeka namna gani? Lazima tupate watalii wengi na ndiyo maana Serikali imekuja na jibu la kuongeza mapato kwa kununua ndege ili watalii hawa wawe wengi sana. (*Makofi*)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, leo tulikuwa kwenye semina na wanasema watalii wengi tunaopata ni wazee, huwezi kumsafirisha mtalii mzee kwa gari kutoka Arusha kama unakuja Selous, haiwezekani, lazima atumie ndege. Niishauri Serikali siyo hizi kubwa tu wanunue hata ndege ndogo, tunaona hata wakati wa uchaguzi kuna vyama CCM na vingine tunakodisha ndege kutoka Kenya maana yake tunahamisha uchumi kuwatahirisha Kenya, ni bora zinunuliwe ndege nydingi ndogo hapa nchini tunakodisha na uchumi huo utaendelea kubaki ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wale wanaobeza suala la ununuzi wa ndege jambo hili ni la kwenda kuimarisha mapato ya Serikali kwa sababu mionganoni mwa kinachochangia mapato makubwa Serikalini ni utalii kwa zaidi ya asilimia 17.6. Kwa hiyo, kwa kununua ndege hizo tuna uhakika watalii wetu wataongezeka. Tuipongeze Serikali kwa ununuzi huu wa ndege na kwa ubunifu huu wa kuongeza mapato badala ya kuwabeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa dakika tano, tano wanagawana Mheshimiwa Mwakajoka na Mheshimiwa Qambalo na atafuata Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba hali iliyopo sasa hivi kwenye nchi hii ni lazima tufike mahali Wabunge tukubaliane, kila mmoja anasema hapa kwamba hali ni mbaya sana katika jimbo lake, lakini wako watu wanapongeza baadae wanaanza kulalamika kwamba hali ni mbaya. Hiki kitu ndio kinachotuchelewesha sana kuleta maendeleo kwa sababu tunazungumza jambo ambalo

hatuna uhakika nalo huku tukijua kwamba hali ni mbaya sana katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016/2017 kwenye bajeti iliyopita kulikuwa na mradi mkubwa ambao ultaka kutekelezwa kwenye Mji wa Tunduma na kampuni kutoka Ubelgiji. Mradi huu ulikuwa na thamani ya *Euro* milioni 100. Mradi huu umeyeyuka na sasa hivi hata kwenye vitabu hivi vya Waziri huwezi kuuona mradi huo. Ukiangalia kwenye Mji wa Tunduma ambao uko mpakani mwa nchi nyingi ambazo zinapitia pale karibu nchi nane hakuna maji kabisa. Wananchi wangu ambao wamewekeza kwenye Mji wa Tunduma leo hii wanakosa maji, wageni wanaokuja kutembelea kwenye Mji wa Tunduma na kuingia kwenye nchi sasa wanalala Zambia. Kwa hiyo, tunakosa mapato na Serikali inakosa mapato kwa sababu hoteli nydingi pia zimeanza kufungwa kwenye Mji wetu wa Tunduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nikuambie tu kwamba mimi wananchi wangu wameathirika sana, sasa hivi pale kwenye Mji wetu wa Tunduma na Wilaya nzima ya Mbozi pamoja na Momba tuna tatizo kubwa la *typhoid* kwa sababu ya kukosa maji. Watu wengi wanapoteza maisha kwa sababu ya kupata maji ambayo si safi na salama. Mimi jambo hili kwa kweli sitakubaliana nalo kabisa na nataka niseme Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi wafike mahali waelewe kwamba kipaumbele kikubwa ni kuhakikisha kwamba afya za Watanzania zinakuwa bora ili waweze kuzalisha na waishi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nchi hii ukizunguka maeneo yote kwenye Taifa hili, tumejaribu kuzunguka kila maeneo tukiwa na ziara ya Kamati ya Nishati na Madini wanafikirii sisi ni Kamati ya Maji, kila mtu anasema jamani maji huku hatuna. Nchi nzima hakuna maji, hali ni mbaya sana katika Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi Tunduma pale nahitaji miradi mikubwa ya maji. Juzi kulikuwa na miradi imekuja midogo sana ambayo haiwezi kutosheleza wakazi wa Mji wa

Tunduma, tunahitaji maji ya kutosha kwenye Mji wa Tunduma ili wananchi wangu waweze kupona magonjwa ambayo wanaendelea kupambana nayo ya *typhoid* kwenye mji wetu. Tumepoteza watu wengi mno kwa sababu ya uzembe wa Serikali kuendelea kutokutoa fedha kwenye Wizara ya Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, watu wengi sana wanawaangalia vibaya Waheshimiwa Mawaziri lakini ukweli ni kwamba Mawaziri hawa wafanye nini? Tunaangalia bajeti ya miaka mitatu iliyopita ukijaribu kuangalia bajeti ya mwaka...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, sekunde tu. Mheshimiwa Ntimizi na wenzako mmeanzisha Bunge lenu huko. Endelea Mheshimiwa. (*Makofii*)

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ukiangalia miaka mitatu kuanzia mwaka 2015/2016, 2016/2017, 2017/2018 huwezi kuamini utekelezaji wa bajeti ya maji ni asilimia 26 tu kwa miaka yote mitatu ukichukua uwiano. Kweli tunaweza tukasema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ina lengo la kupunguza tatizo la maji kwa wananchi wa Tanzania kama kweli inatekeleza kwa asilimia 26 ndani ya miaka mitatu uwiano tumejaribu kuangalia. Wananchi wa Tanzania wameiamini Serikali hii na mkapigwa kura halafu baadae mmeanza kuwababaisha wananchi wa Tanzania. Tunataka maji kwenye Taifa hili, tunataka kuondoa matizo kwenye Taifa hili yanayotokana na maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo hii wameweka bajeti ya maji kidogo na utekelezaji wake kama tulivyozungumza lakini huwezi kuamini leo tunakwenda kununua ndege, tena juzi tumenunua ndege sita na juzi Mheshimiwa Rais anasema anaongeza ndege ya saba eti wanakwenda kuchukua tena *cash* hakuna kukopa. Hivi wananchi wa Tanzania asilimia tano wanaopanda ndege ndiyo waliomchagua Mheshimiwa Rais? Hivi asilimia tano wanaopanda ndege ndiyo waliowachagua Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ambaao ni wengi ndani ya Bunge hili wanashindwa kuona

huruma kwa wananchi wa Tanzania ili kuhamkisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata maji, afya nzuri na wanapunguza vifo ambavyo vinatokana na magonjwa ya maji? Mimi sikubaliani hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna mambo ya msingi, tulisema tunahitaji tuwe na kilimo cha umwagiliaji ili tuwe na kilimo bora ambacho kitakuwa kinazalisha chakula kwa muda wote. Huwezi kuamini mwaka 2016/2017 tulitenga bajeti ya shilingi bilioni 25 fedha iliyokwenda ni shilingi bilioni 1.2 peke yake. Mwaka 2017/2018 tumetenga shilingi bilioni 24 lakini fedha iliyokwenda ni shilingi bilioni mbili peke yake, tunafanya nini katika Taifa hili. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakajoka, nakushukuru sana. Sasa ni Mheshimiwa Willy Qambalo, dakika tano tafadhali.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana kwa ajili maisha na uhai wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na eneo la uhifadhi wa mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji. Yapo mambo ambayo tunaweza kusema yanahitaji fedha nyingi lakini yako mambo ambayo pengine hayahitaji fedha kiasi hicho ni suala tu la umakini na utekelezaji wa sera na taratibu ambazo tumejiwekea.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa alifanya ziara ya kikazi katika Bonde la Eyasi mwishoni mwa mwaka 2016. Wananchi walieleza kero zao nyingi ikiwemo uharibifu wa chanzo cha maji cha Mto Qangded. Baada ya Waziri Mkuu kuwasikiliza wananchi hao na kuona ukubwa wa jambo hilo alitoa maagizo mawili yafutayo; jambo la kwanza; eneo la chanzo cha Mto Qangded lihifadhiwe kwa mita zisizopungua 500 kila upande. Jambo la pili, mashine zote za ku-*pump* maji zilizoko kwenye

mto na kwenye chanzo ziondolewe jioni ya siku hiyo na zisirudi kwenye chanzo hicho. Jambo la kushangaza hadi leo mwaka na nusu maagizo ya Waziri Mkuu bado hayajatekelezwa. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Maji unisikilize kwa sababu naongea na wewe, naona unaongea pemberi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni jambo kidogo la kusikitisha kama Kiongozi Mkuu wa Pili wa nchi anatoa maagizo na maelekezo halafu mwaka na nusu unapita hakuna jambo ambalo limefanyika. Mbaya zaidi hawa watu wenye kiburi, wenye jeuri wanaoharibu vyanzo hivyo sasa wamevuta na umeme wa gridi kuupeleka kwenye vyanzo vya maji ili wa-pump vizuri maji hayo na wale walioko chini hawapati maji, tunakwenda wapi? Ni jambo ambalo haliiingii kwenye akili ya kawaida huku tunasema hatuna fedha za kufanya miradi lakini hata hili la kusimamia sheria tumeshindwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri juzi uliulizwa maswali mawili ya nyongeza hapa na Mheshimiwa Paresso na dada yangu Mheshimiwa Catherine kuhusu chanzo hiki hiki na ukasimama, ukalidanganya Bunge kwamba chanzo kile kimepimwa. Mimi naomba nikuhakikishie chanzo kile bado hakijapimwa. Wataalam wako wa Bonde la Kati walikwenda Bonde la Eyasi, wamekaa kwa siku moja lakini wakakwamishwa na viongozi walioko chini yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni suala la athari za mafuriko. Ukiungelea chanzo cha Qangded, Bonde la Eyasi unaongea juu ya uhai wa wananchi wasiopungua 70,000. Chanzo kile kikipotea wanachi hao maisha yao yako hatarini. Juji wananchi wa Mang'ola baada ya chanzo kile kuharibika wamejichangisha zaidi ya shilingi milioni 21 na Halmashauri ya Karatu ikaweka shilingi milioni 35 ili kunusuru chanzo hicho. Nikuombe sasa na wewe uweke mkono kwa sababu wewe uko kwenye chungu kikubwa ili kuhakikisha chanzo hicho kinaendelea kutoa huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri ulipokuwa Mang'ola kabla kidogo ya ziara ya Waziri Mkuu

ulitoa ahadi ya kuboresha miundombinu katika eneo hilo. Nikukumbushe tu kwamba bado wananchi wanakumbushia utekeleze ahadi yako ya kuboresha baadhi ya miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nimesoma katika kitabu cha Waziri, mwaka 1962, kiwango cha maji kwa mtu katika nchi hii ilikuwa ni mita za ujazo 7,862 lakini mwaka huu ni mita 1,800 za ujazo kwa mtu kwa mwaka. Tunakwenda chini kwa kasi kubwa sana. Nadhani kama nchi tuna kila sababu ya kuchukua hatua. Kama miaka 50 kumekuwa na tofauti kubwa kiasi hicho, miaka 50 inayokuja nadhani tutakwenda chini ya mita 100 za ujazo. Kwa hiyo, mimi nishauri hebu Serikali fanyeni jitihada za makusudi za kuhakikisha vyanzo vya maji nchi hii vinalindwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015/2016 asilimia 28 ya fedha ambazo tulipitisha ndio zimekuja, mwaka uliofuata asilimia 25, mwaka huu ambao tunamalizia asilimia 22. Mheshimiwa Waziri una jeuri gani kuja mbele yetu leo na mabilioni ya hela wakati siku zilizopita umekuwa unapata hiso asilimia chache? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia mimi simuoni Waziri kama anasikitika, simuoni Waziri kama analia, Waziri unataka tukusaidiaje? Hebu lia tusikie halafu na sisi tukusaidie. Mimi naona wewe unaridhika tu na hicho unachopewa. Pambana kama wenzio upate hela za kutosha, maana yake hapa tutakurushia madongo na mawe ya kila aina lakini mwisho wa siku kama ulikuwa unashuka na ukafika 22, bajeti hii hata 20 haitafika. Kwa hiyo, mimi nadhani ndugu zangu suala la maji halina mbadala, mtu aitaka maji unampa maji. Kwa hiyo, mimi niombe hebu tuweke jitihada za makusudi nchi hii tuhakikishe eneo hili linapewa fedha za kutosha. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Qambalo dakika tano zimeshakwisha.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Nilidhani wewe mwenyewe ungelia kidogo, ungeyesha *demo* angalau, halafu Waziri angekuunga mkono. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ally Keissy nilishakutaja na utafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. ALY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa namshukuru Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe*, Naibu Waziri, Mheshimiwa Aweso kusema kweli baada ya kulalamika hapa Bungeni walifunga safari ingawa Nkasi ni mbali walifika mpaka Nkasi kuangalia jinsi miradi ya maji inavyoibowi.

Mheshimiwa Spika, katika kuibwa hii Wizara ndiyo inaibiwa, yaani hakuna sehemu tunaibiwa kama Wizara ya Maji. Mheshimiwa Aweso alijiona mwenyewe alivyofika Kirando, Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe* alijiona mweyewe alivyofika Kabwe, wamejiona miradi ya kusadikika yaani ni miradi ya ajabu ajabu. Kabla ya wiki moja hajafika Mheshimiwa Kamwelwe pale tenki lilibomoka kidogo liue wanafunzi, yeye mwenyewe shahidi aliona. Alifika Mheshimiwa Aweso mwenyewe akasema hii miradi kusema ukweli wanapeana kijomba kijomba, kishangazi shangazi, hakuna kusema ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kamwanda - Kirando nitakusomea, mradi huu umeingiwa mkataba wenyewe gharama ya shilingi bilioni 7.7 na mkandarasi Wimbe, mkandarasi ni *class five* ambao uwezo wake ni shilingi milioni 750 lakini akapewa kijomba kijomba mara kumi zaidi. Maelezo ya Bodi ya Usajili wa Wakandarasi tarehe 4 Julai, 2017 yalieleza kuwa mkandarasi huyu hana sifa za kutekeleza mradi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haikutosha, hata *guarantee* ya benki hakuweka, hana uwezo. Baraza la Madiwani Nkasi llimkatalia, lakini baada ya kusimamisha mradi alikwenda kukopa mabomba Kahama akaleta mabomba Kirando, yaani ni wizi wa hali ya juu. Tukazuia shilingi milioni 800 na

huyu mkandarasi nilizungumza hapa Awamu ya Nne, mkandarasi huyu ndiye alipewa shilingi milioni 210 kwa mradi wa maji Kamwanda, alikula hela hakuna chochote kilichofanyika, huyu mkandarasi. *Tenderyake haikutangazwa, siri, ni ujambazi wa hali ya juu. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu mkandarasi ni jambazi na miradi mingi ya Mkoa wa Rukwa huyu bwana kaingia haitoi maji. Nenda Matala mradi wa shilingi milioni 450 hakuna maji yaani miradi ya Nkasi utadhani ni Zaire kule Congo hawawezi kujua watu, lakini miradi yote ya Nkasi ni wizi, ni wizi, ni wizi hakuna hata mradi mmoja ambao unasema unatoa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana, Awamu ya Nne hapa imetoea shilingi bilioni 1 kwa ajili ya Bwawa la Mfili, alikwenda Naibu Waziri wa TAMISEMI, Ndugu yangu, shemeji yangu Kakunda kwenda kuangalia ule mradi thamani yake haifiki hata shilingi milioni 350 kwa ushahidi kabisa leo wanatoa shilingi milioni 300 kwenda kuweka mabomba, sijui kuweka mashine pale kwenye bwawa, bwawa lenyewe halina maji, amechimba kwa shilingi milioni 350, ni ujambazi wa hali ya juu. Hii Wizara kusema kweli inaibiwa hela zinatoka kule na zinarudi huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viongozi wakubwa ndiyo wenye miradi hii wanajulikana, kwa ushahidi wanana tafuta mimi tuzungumze nao na mimi nawakatalia. Eti Mbunge nyamaza ili waibe zaidi, haiwezekani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Isale - Kate, mikataba hii hapa wamefutafuta, wameongeza shilingi milioni 24 hajilikan za nini. Wanaweka shilingi milioni 300 eti kuzuia maji tu pale ili kuja huku, shilingi milioni 300. Ndugu zangu kodi za wananchi tuzioneeni uchungu, hii ni kodi ya wananchi. Serikali haifyatui noti ni kodi za wananchi, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walikwenda kujionea Mawaziri wenyewe, *Engineer Kamwelwe* alikwenda kuona kule Kabwe

wameweka *solar fake fake*, betri *fake fake* tu alikwenda kuona mwenyewe, tenki kidogo liue wanafunzi alikwenda kuona mwenyewe. Mheshimiwa Aweso alifika mpaka Kirando, wakandarasi kawaambia. Sasa nataka kujua Mradi wa Kirando umesimama leo miezi sita na Mkurugenzi kasimamishwa kazi, natakakuja mradi wa Kamwanda utaanza lini kutoa maji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumezuia wizi huu, ukipiga mahesabu zaidi ya shilingi bilioni tatu ilikuwa ziende mimi ndiyo nimezuia hii, nastahili sifa. Hata wakichunguza Mradi wa Isale - Kate kuna wizi. Miradi yote ya Rukwa ukichunguza ni wizi wa mabilioni ya hela. Ni kweli lazima Tume itumwe kila mradi wa maji uchunguzwe. Haiwezekani Rais anajitahidi kukusanya pesa Idara ya Maji ni kama mfereji, ndiyo maana ikaitwa Idara ya Maji, unatoa watu, unamwaga tu. Ndugu zangu tuwe na uchungu na nchi hii, hatuwezi kukubali kuibiwa namna hii. Maji ni uhai, Namanyere tunapata maji asilimia 16 leo mnasema maji vijijini sijui asilimia ngapi Namanyere maji yako wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilizungumza hapa mimi Mbunge nakaa siku tatu siogi, Namanyere kuna maji yako wapi? Asilimia 16 Namanyere maji hayatoki zaidi. Hakuna mradi umekamilika, hata kama mradi unatoa maji ukilinganisha na fedha mzee ni balaa tupu. Hata mimi sikusomea huo uinjinjia, sikuoma mahesabu lakini huwezi kunidanyanya bei ya bomba inajulikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilizungumza hapa miaka iliyopita kweli nina uchungu nimemwambia na alikuja mpaka Waziri pale aliyetoka tukawmwbilia usilipe hizi hela, usilipe shilingi milioni 300 hizi kwa hili bwawa maana thamani yake haifiki shilingi milioni 900 lakini cha ajabu alilipa hela. Ndiyo maana Rais akipita sehemu anasema wakamateni wakandarasi, msaidieni Rais Ndugu zangu yuko peke yake, hebu muoneeni huruma. Haiwezekani mtu anachimba bwawa la shilingi milioni 300 mnamlipa shilingi milioni 900 na tulizuia! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, alikuwa Zumba na Zumba siku hizi ndiyo Naibu Katibu Mkuu hapa TAMISEMI, alikuwa kwenye bwawa na akasema huyu Mhandisi ondoka naye na hizi hela msilipe lakini walilipa. Zumba shahidi leo ni Naibu Katibu Mkuu, TAMISEMI, tusemeje sasa sisi? Mbunge anazuia, *RAS* anazuia, *Mkurugenzi* anazuia, *DC* anazuia lakini analipwa kijanja kijanja. Ndiyo maana tunasema huko Wizarani kuna mtiririko, kuna wizi, kuna ujambazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sifichi, sili kwao, mimi nakula hela yangu ya halali hapa nawaambia ukweli kabisa anayechukia achukie, hizi kazi wanapeana kijamaa, kijomba kijomba. Mtu hana *guarantee* ya benki, hana chochote, anapata ile *15 percent* ndiyo anakwenda kununua magari na mabomba. Leo mradi wa Isale umesimama, kapewa shilingi bilioni 1.1 kaenda kununua magari mawili, kaenda kununua mabomba, kaishiwa hela anataka *certificate*, hakuna chochote. Ndugu zangu tuangalie hii miradi ni nani anaichunguza mpaka kupandishwa thamani, mradi wa shilingi bilioni tano, shilingi bilioni nne unakuwa wa shilingi bilioni saba? Nataka Mradi wa Kamwanda kuanzia sasa Mheshimiwa Waziri kaufanyie mahesabu uanze kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wananchi hawana makosa au mimi kosa langu kusema panatokea wizi ndiyo mmesimamisha mradi? Maana yake mimi ndiyo nimesema kuna wizi, baada ya kusema kuna wizi shilingi milioni 800 hakupewa na mradi umesimama, wananchi wanateseka hawana maji, kosa lao ni nini? Ningeachia mradi tungeibiwa zaidi ya shilingi bilioni 3.5. Hata mtu fanya hesabu kidogo tu, mradi wa kutoka Kate mpaka Isale ni shilingi bilioni 5.4 na unakwenda zaidi ya kilometa 30, Mradi wa Kirando unachukua maji Ziwa Tanganyika nusu kilomita shilingi bilioni 7.7 Ndugu zangu hebu na nyie wenyewe semeni ukweli. Hata mtu mpumbavu hakusoma darasa la pili atajua hesabu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mradi wa kutoka Kate kwenda Isale una-*supply* vijiji saba njiani, kilometa 35, shilingi bilioni 5.4 na hapo bado kuna wizi ndani yake...

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy nakuongeza dakika tano.  
(*Makofi/Kicheko*)

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Spika, ahsante

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Alie kidogo, alie kidogo  
Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, vijiji vya  
Nkasi karibuni vyote havina maji, Kata ya Mkwamba yote  
haina maji, vijiji vyote havina maji wala kisima hakuna. Visima  
wamechimba wakati wa Mzee Nyerere pia havitoi maji. Tuna  
matenki Kirando tangu enzi ya Nyerere bado Rukwa iko chini  
ya Mkoa wa Mbeya...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika,  
taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Haya toa taarifa.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Keissy. (*Makofi*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Kuna vijiji vya Itindi, Isale,  
Gele, Masolo, Katongoro, Kakoma, Ipanda havina maji wala  
kisima hata kimoja.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika,  
taarifa.

**SPIKA:** Sipokei taarifa muache aendeleee.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Wananchi wanafukua maji  
kwenye madwimbwi wakati wa masika kama panya, hela  
inakwenda wapi?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mzee mwenzangu...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, Serikali  
inatoa hela, lakini watendaji ndiyo wanaiba hela hizi. Kwa  
Nkasi mimi siilaumu Serikali hata kidogo, Serikali inatoa hela

lakini zinaliwa na wajanja wajanja wanapewa hela kijomba kijomba, kishangazi shangazi. Amesema Ester Bulaya hapa ni kweli yule mkandarasi hata kule Mtwara alikula hela, wala siyo uongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kusema kweli ni hatari, maji Ziwa Tanganyika yapo wananchi hawapati maji. Ni kitu cha ajabu kabisa, mradi wa shilingi bilioni 7.7 ulikuwa tayari kwenye *pipe* na anapewa hela hawa mapema kabisa, walitaka kumpa shilingi bilioni moja wakati hakuna kitu, Mradi wa Isale amepewa shilingi bilioni 1.1. Nataka TAKUKURU wakachunguze miradi yote Wilaya ya Nkasi na TAKUKURU wamekwenda kule wameshakaa mwezi mmoja na nusu. Niliwaomba TAKUKURU wakakae kule Mkoa wa Rukwa, nilimwambia Mkurugenzi wa TAKUKURU mimi kaangalie miradi ya mkoa mzima wa Rukwa, mkoa mzima ni wizi mtupu na inawezekana nchi nzima lakini kule kwetu mzee walfanya maficho. Namshukuru Mheshimiwa Aweso aliwaambia wakandarasi mbele ya uso wake kwamba nyie hapa mlitaka kula.

Mheshimiwa Spika, mwenyewe Waziri wa Maji alifika mpaka Kabwe akashuhudia tenki linawekwa maji baada ya maji kujaa limepasuka lote pwaaa! Mpaka leo Mheshimiwa Waziri hawajenga lile tenki. Tulikwenda na wewe mpaka leo hawajenga lile tenki. Yule mkandarasi akaja kukuambia ooh mimi tunajuana tunajuana kitu gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy inatosha, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Baada ya Mheshimiwa Keissy kuna watu wanataka kuchangia tena kweli?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Siyo tumuite Waziri ahitimishe hoja? (*Kicheko*)

Ahsante sana, nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Leah Komanya na atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu. Namshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kuniwezesha kusimama hapa jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuipokea hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Maji na naiunga mkono na natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa namna wanavyojituma katika shughuli za maji. Nitoe shukrani zangu za dhati kwa jinsi walivyounusuru Mradi wa Maji wa Bwawa la Mwanjoro kutoka Wilayani Meatu kwa sababu bwawa hili lilikuwa limetelekezwa toka mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, nikijielekeza upande wa hotuba, naomba kuongea kuhusu huduma ya maji vijijini. Katika kitabu cha hotuba ukurasa wa saba, Wizara imesema kwamba imejenga vituo vya kuchotea maji 123,000 na vituo 85,000 ndiyo vinavyofanya kazi tu. Kwa hiyo, ukiangalia pale ni vituo 38,000 ambavyo havifanyi kazi ambapo ni sawa na asilimia 30. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda zaidi Wizara imeona changamoto inayosababisha vituo visitoe maji ni usimamizi pamoja na uendeshaji wa miradi hii unaosababishwa na uendeshaji kwa kutumia dizeli. Naiomba Wizara iende zaidi kuangalia changamoto inayosababisha vituo visifanye kazi ikiwa ni pamoja na usanifu mbovu, usimamizi mbovu na utafiti mbaya. Kama Wizara itazichukua hizo sababu nyingine tatu kama changamoto, itaweza kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji kwa sababu tumeona usanifu umekuwa ukifanyika chini ya viwango, utafiti mwangi wa maji unafanyika wakati *water table* iko juu na kusababisha maji kupatikana wakati wa masika tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichangie kuhusu mradi wa maji wa kutoka Ziwa Victoria na kuyaleta katika Makao Makuu ya Wilaya ya Busega ambayo ni Nyashimo,

Bariadi pamoja na Itilima. Utekelezaji wa mradi huu imekuwa ni muda mrefu sasa. Toka Septemba, 2016 Waziri wa Mazingira alitujulisha kwamba fedha tayari zimeshaletwa lakini mpaka leo usanifu unafanyika. Naomba usanifu uishe haraka ili mradi utekelezwe kwa sababu maji yanahitajika kwa ajili ya hiyo miji mipya ya kiutawala iweze kujengeka. Nyashimo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Busega, Bariadi ni Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu na Itilima na Makao Makuu ya Wilaya ya Itilima yenyeewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maji haya pia ni muhimu kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na fedha hizi zililetwa kwa ajili ya kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa namna unavyochelewa kutekelezwa maana ya makusudio ya kuletwa hii fedha itakuwa haipo.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee Mradi wa Maji wa Kitaifa wa Wilaya ya Maswa. Katika kitabu cha bajeti wamesema kwamba utekelezaji wa ujenzi wa mtambo na kuchujia na kutibu maji unaendelea kukamilika na kwamba mradi utakamilika Mei, 2018 ambao ni mwezi huu. Ukiangalia muda wa mkandarasi wa kufanya kazi umekwisha lakini kazi haijakamilika. Mtambo huu utatumika kuchuja, kusafisha na kutibu maji lakini ukiangalia bwawa lile halina maji, limejaa tope. Kwa hiyo, hapa mimi naishauri Serikali itengete fedha kwa ajili ya kutoa tope hilo ili kuweza kuongeza kina cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee mradi wa skimu ya umwagiliaji iliyopo Wilaya Meatu ambapo mimi ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani pia ni mjumbe wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji. Ipo skimu ya umwagiliaji Kijiji cha Magwila na ilianza kutekelezwa 2012/2013 na ungekamilika 2013/2014 lakini mpaka leo mradi huu haujakamilika. Fedha iliyotumika ni shilingi 1,165,000,000 na kazi iliyofanyika ni kujenga chujio, kujenga mfereji wa kati wa mita 1,000 kati ya mita 7,000 pamoja na sehemu 12 za kusambazia maji. Shilingi bilioni 1 ikawa imetumika na imekwisha lakini mradi huo mpaka leo haujakamilika kwa ajili ya kunufaisha wananchi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka Mheshimiwa Waziri aieleze jamii ya Meatu kwa nini mradi huu haujakamilika? Kwa sababu fedha ilikuwa ya Mfuko wa Maendeleo ya Benki ya Afrika na usimamizi ulikuwa unafanywa na *DASIP* Kanda ya Mwanza. Halmashauri ya Wilaya haikuhusika na chochote katika usimamizi wa kiufundi. Mshauri wa mradi ilikuwa ni kampuni kutoka Jijini Nairobi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni lini mradi huu utatekelezwa? Naishauri Serikali ikamilishe sehemu iliyobaki ya mita 6,000 ya mfereji wa kati pamoja na kujenga mfereji mkuu ili sasa ule mradi uweze kufanya kazi. Pia naomba mradi huu ufuatiliwe ili kuona kama thamani ya fedha ipo. Maana mradi huu ungekamilika ungeweza kusaidia kaya 123 za kijiji hicho kati ya kaya 650 na ungeweza kusaidia upatikanaji wa mbogamboga na mazao mengine kwa Wilaya nzima ya Meatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ngombale hayupo?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili, moja linatoka kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Mabula kwamba kutokana na uhitaji mkubwa wa ununuzi wa viwanja kwenu ninyi Waheshimiwa Wabunge, Halmashauri ya Jiji la Dodoma, imeamua kwamba tena watakuwepo watalaam wake kesho kuanzia saa 7.00 mchana hadi saa 11.00 jioni kwa ajili ya zoezi la uuzaji wa viwanja.

Kwa hiyo, Wabunge ambao mngependa kununua viwanja katika maeneo ya Jiji la Dodoma mnakaribishwa kufanya hivyo kesho mchana, *Administration Block* pale chini.

### *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, niwaambie tu, walikuwepo wenzenu miaka iliyopita zilikuwa zinatolewa fursa kama hizi hizi za viwanja wakawa wanadharaudharau lakini leo hii wanajuta sana. Kwa hiyo, ni vizuri ukajipima ukaona kama unawea ukapata basi ni vyema ukafanya hivyo, maana ni fursa hiyo. Hilo ni la kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, la pili, asubuhi tulikubaliana kwamba saa 11.00 jioni au *around* hapo, Mheshimiwa Waziri Viwanda na Biashara angekuja na maelezo ya Serikali hapa kuhusu nini kinaendelea. Sasa nimuite *Chief Whip* ili alieleze Bunge alichonacho maana sasa ni saa kumi na mbili jioni. (*Makof*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, tulipokea maagizo yako na tulirudi Serikalini kuyafanyila kazi kama ulivyotuelekeza.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kikao cha kupokea matokeo ya uchunguzi wa kisayansi kutoka katika taasisi husika zote kinaendelea na kinaongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kikao hicho kukamilika, tunaliomba Bunge lako liridhie taarifa ya Serikali itolewe kesho jioni ili iwe taarifa kamilifu ya kutoa mwelekeo wa kutatua tatizo hilo kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makof*)

**SPIKA:** Hilo sitawahoji ni la utawala tu. Tunapokea maelezo haya na tunayakubali kwa jambo moja kwamba kesho saa 11.00 jioni tutaanza na hili. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kesho 11.00 jioni tunaanza na hili. Kama Serikali haitakuwa na maelezo kesho saa 11.00 jioni basi mimi nitalifunga kiaina tutawaachia Watanzania. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Vedasto Ngombale hayupo, tunaendelea na Mheshimiwa Augustino

Masele atafuatiwa na Mheshimiwa Azza Hillal. Tunaanza na Mheshimiwa Masele Mbunge wa Mbogwe.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili kusudi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu ya Maji na Umwagiliaji chini ya Mheshimiwa Waziri Kamwelwe.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai. Kwa hakika ndiyo maana Serikali yetu imekuja na mpango mzuri na miradi mingi mikubwa imeorodheshwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Mbogwe ni mionganini mwa Wilaya ambazo tulifanikiwa kunufaika na miradi ya *World Bank* tukapata maji katika eneo la Nyerere, Mji wa Masumbwe, Shenda, Bulugala Kata ya Nyasato na Lulembela, Kata ya Lulembela. Miradi hii inafanya kazi vizuri, naipongeza Serikali. Pia tumeleta makadirio ya maombi ya fedha kwa ajili ufungaji wa umeme katika hivi vyanzo vya maji vya visima virefu katika hii miradi minne *World Bank*.

Mheshimiwa Spika, nataka niiambie tu Serikali kwamba Wilaya yetu ya Mbogwe ilikuwa ni sehemu ya Wilaya ya Kahama ambayo kimsingi ilionekana dhahiri kwenye Serikali kwamba tuna upungufu wa maji ardhini na kwa maana hiyo Serikali ikaamua kuleta maji kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, nimpongeza Mheshimiwa Waziri Kamwelwe aliyahi kufika Mbogwe. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu ombi letu ulilikubali na ukafika na uliojionea hali halisi. Wilaya yetu ya Mbogwe tuna Makao Makuu yetu ambayo yako katika Mji wa Kasosobe na wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri ulifika na ukajionea hali halisi kwamba pale kumefanyika jitihada za kuchimba maji lakini kutokana na upungufu wa maji ardhini visima hivi vimekuwa vikitoa maji machache ambayo yanastahilli kwa ajili ya kuweka *pumpza* maji peke yake. Kwa hiyo, niiombe tu Serikali ifikirie uwezekano wa kutupatia maji kutoka Ziwa Victoria

kwa sababu Wilaya ya Kahama ipo jirani na kwetu pale, ikiwezekana basi pesa zipatikane za kuweza kutuletea maji hayo ili hatimaye tuwe na uhakika wa maji muda wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maji ni kitu muhimu sana kwa mambo yote, iwe uwekezaji wa viwanda ambaao sasa tunafikiria kwamba Tanzania itakwenda kuwa ni Tanzania ya viwanda, viwanda bila maji haiwezekani. Maji yanahitajika pia kwa mifugo na shughuli za kilimo cha umwagiliaji. Kwa maana hiyo, niiombe Serikali iendelee kuweka pesa katika Wizara hii na zitolewe kwa wakati. Pale tunapopitisha bajeti ni vizuri sasa Wizara ya Fedha ikazitoa pesa hizo kwa wakati na miradi ile ambayo imependekezwa itekelezwe kwa mujibu wa bajeti ya mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, tunayo pia miradi ambayo imetengewa pesa kwa ajili ya kuchimba visima katika Kata ya Ng'homolwa, Kijiji cha Chakabanga, pia katika Kijiji cha Lugunga Luhala. Vijiji hivi vimefanikiwa kupata maji wamechimba wakapata maji na kwa maana hiyo *certificates* zimepelekwa kwa Waziri ili kusudi tupatiwe pesa na utandazaji wa mabomba uweze kufanyika. Kwa maana hiyo, naomba Serikali utupatie hizo pesa kwa ajili ya uendelezaji wa visima hivi kwa maeneo ambayo tumefanikiwa kupata lita za ujazo ambazo zinaweza zikafaa kwa ajili ya uanzishaji wa visima vikubwa au visima virefu ili wananchi wetu waweze kupata hii huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya vyanzo vyta maji pia yanatakiwa yapewe utaratibu mzuri wa hifadhi ya mazingira. Kwa sababu bila kuwa na mazingira yaliyo safi hakika tunaweza kujikuta tunapata shida zaidi. Ni dhahiri kwamba vyanzo hivi vyta maji tunavyokuwa tunavianza na kuvisambaza kwa wananchi, vilevile tutarajie kwamba kutakuwa na maji machafu. Kwa maana hiyo, niombe tu kwamba wakati Serikali inakuja na mipango hii ya maji safi na salama basi tuwe na mipango mahsus kwa ajili ya *treatment* ya maji machafu ambayo yanazalishwa kutokana na matumizi mbalimbali. (*Makof*)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, najua wazi kwamba maji ndiyo chanzo kikubwa cha maradhi. Kwa maana hiyo, tukiwa na maji ambayo ni salama nina uhakika magonjwa mbalimbali ya kuambukiza ikiwemo kipindupindu na magonjwa mengine ya matumbo yanaweza yakadhibitiwa tukajikuta kwamba hata ile huduma ya dawa hospitalini bajeti yake inaweza ikapungua endapo watu hawaugui magonjwa maambukizi ya kuwadhuru wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, niombe tu Serikali iendelee pia na utaratibu huu wa kuhakikisha kwamba tunapanda miti kwenye vyanzo vya maji. Vyanzo vya maji vikiwa vimepandwa miti naamini kwamba kwa namna ya moja au nyingine tutakuwa tumesaidia kuhakikisha kwamba ukame unadhibitiwa na tutakuwa na uhakika wa kupata mvua za kuaminika. Wakati wote tutajikuta kwamba tumeondokana na ukame ambao unasababisha upungufu wa maji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ambazo tayari tumeshapeleka Wizarani, ninayo imani kwamba miradi yetu ambayo tumeiomba kwa Serikali itafanyiwa kazi. Kwa maana hiyo, niseme tu kwamba Wanambogwe tunaiunga mkono Serikali na niseme kwamba naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Augustino Masele, nilishakutaja Mheshimiwa Azza Hamad Hillal na atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Katani upande wa CUF.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyenijalia pumzi na uzima na hatimaye kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo inaifanya hususani katika usambazaji wa maji ingawa kuna kasoro ndogo ndogo ambazo zipo katika usambazaji wa maji. Naamini Waziri,

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Naibu Waziri na watendaji kwa sababu wako hapa watajipanga kuona wanatatuaje changamoto hizo zilizopo hususani katika Mkoa wa Shinyanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria ambao uliana Mkoa wa Shinyanga kwa mwaka 2014. Kulikuwa na utaratibu wa vijiji vilivyopo ndani ya kilometra 12 kupatiwa maji, hiyo ni toka mwaka 2014, lakini mpaka hivi tunavyoongea imekuja awamu nyingine ya usambazaji wa maji ya Ziwa Victoria kuna vijiji ambavyo havijapata maji. Naomba nitaje baadhi ya vijiji hivyo, vijiji vya Ntobo, Nyamigege, Kula, Buchambaga, Busangi na vingine vingi ambako bomba la Ziwa Victoria limepita kwa mara ya kwanza. Niiombe Wizara ya Maji waangalie wanakwendaje kumaliza vijiji hivi vilivyopo ndani ya kilometra 12 kwa mradi wa awamu ya kwanza ya Ziwa Victoria ambavyo mpaka leo hii hawajapata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa katika Mkoa wangu wa Shinyanga, naomba niizungumzie Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu. Mkoa wa Shinyanga mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria ndiyo unakwenda kupeleka maji Mkoa wa Tabora. Nasikitika kusema kwamba Halmashauri ya Ushetu haina kijiji hata kimoja ambacho kinapata maji ya mradi wa Ziwa Victoria. Ukiangalia Kahama Mji na Ushetu ni jirani sana na Ushetu imetokana na Kahama Mji inanipa taabu ni kwa nini...

**SPIKA:** Mheshimiwa Elias Kwandikwa uwe unasiliza! (*Kicheko/Makof*)

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, inanipa taabu sana ni kwa nini Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu hamjaiweka kwenye mpango wa mradi wa maji ya Ziwa Victoria na ukiangalia Ushetu imezaliwa kutoka Kahama. Niiombe Wizara mijipange muangalie Halmashauri ya Ushetu wanawezaje kupata maji ya Mradi wa Ziwa Victoria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niingie katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ina mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria ambao mpaka sasa hivi

unatekelezwa na baadhi ya maeneo yanapata maji. Vijiji vinavyopata maji ni Kolandoto, Maganzo, Mwadui na Munze ambapo ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nimesema katika utekelezaji wa mradi huu, kuna matatizo ambayo yanajitokeza. Ukiangalia pia katika Halmashauri Wilaya ya Kishapu sehemu ambapo bomba kuu linapita kuna vijiji ambavyo viko ndani ya kilometra tatu mpaka tano yaani wanatizama bomba lakini hawana maji, haipendezi. Anawezaje mwananchi wa kawaida kuangalia yeye anahangaikia ndoo moja ya maji lakini bomba analitizima linapita kilometra tatu kutoka hapo yeye alipo? (*Makofii*)

Wizara ya Maji kaeni mijipange, haipendezi na kutakuwa na uharibifu tusipokuwa makini, mtu hawezi kupata shida ya maji wakati bomba analiona linapita kwenye eneo lake. Vijiji hivyo vilivyopo katika Halmashauri ya Kishapu ni Kijiji cha Songwa, Seseke, Nyenze, Kakola, Igaga, Lubaga, Uchunga na Mwadui Luhombo. Naomba Wizara ya Maji mijipange muone vijiji hivyo vinakwendaje kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niingie katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ambayo mimi ndiyo naihudumu na ninakoishi. Nianze moja kwa moja na sehemu ninayotoka, msahau kwao ni mtumwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati wa bajeti nilisimama ndani ya ukumbi huu nikaipongeza Serikali na nikaishukuru Wizara ya maji kwa mradi mkubwa wa maji ambao kwa kitabu cha bajeti cha mwaka jana, ninacho hapa, ukiangalia ukurasa wa 70 kitabu cha mwaka jana mradi mkubwa wa Ziwa Victoria ulikuwa unasomeka kwa ajina la Solwa, Tinde, Nzega, Igunga, Uyui na Tabora. Nilisimama hapa na kuishukuru Serikali, lakini naomna kusema sijui Wizara wameepitiwa, Mheshimiwa Waziri na Naibu wako na watendaji wenu mpo hapa. Mimi naomba mnijibu, kitabu chenu cha mwaka huu cha bajeti jina la mradi limebadilika,

mradi huu umeenda kuondoa jina la Tinde, Mheshimiwa Waziri naomba nipate majibu. Ni kwa nini jina la mradi limebadilika? Katika hotuba yako ya mwaka huu ukurasa wa 46 mradi unasomeka Solwa, Nzega, Uyui, Igunga na Tabora; Tinde tena haimo, kama mmepeitiwa naomba muangalie.

Mheshimiwa Spika, ukizingatia Mheshimiwa Rais alisimama Tinde na akasema, mradi mkubwa wa maji unatoka Solwa, Tinde, Nzega na kwenda mpaka Tabora. Lakini nashangaa hotuba ya mwaka huu labda bajeti ya mwaka huu mmekwenda mradi wa maji wa Tinde. Ninaomba nipate majibu, Mheshimiwa Waziri tumeshasema sana na wewe, nimekufata mara nyingi, lakini kunyamaza si majibu, watendaji wako hapa naomba nipate majibu, wananchi wa Tinde wapate majibu, mradi wa maji wa Ziwa Victoria ni kwa nlini mwaka huu wa fedha haupo katika mradi wenu ambao unasomeka? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa hapo hapo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga naomba nisemee mradi wa maji tena mwingine wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ambaeo ni mradi wa Ziwa Victoria wa Kijiji cha Masengwa.

Mheshimiwa Spika, kuna fedha ambazo mradi huu ilikuwa imesha pata, lakini mradi huu unatoka Manipsaa ya Shinyanga na mradi huu ukifika katika kijiji cha Masengwa unaweza ukahudumia Kata zingine ambazo hazina maji. Ikiwemo Kata ya Samuye, Kata ya Usanda pamoja na Kata ya Mwamala. Kata hizi zinaweza kupata maji kuitia kijiji cha Masengwa.

Mheshimiwa Spika, na niseme mradi huu halmashauri yangu imesha andika barua nyingi Wizara ya Maji, kuanzia mwezi wa tatu mpaka hivi ninavyoongea Wizara ya Maji haijajibu. Kuna matatizo matatu ambayo yanaonekana yapo, Halmashauri imeomba Kibali cha kutumia maji ya SHUWASA kutokana na kwamba, Masengwa ipo nje na Manispaa ya Shinyanga, hivyo hawarushuswi kutumia maji kwa sababu wao wapo vijijini. Halmashauri imeomba kibali

Wizara ya Maji lakini mpaka hivi leo ninavyoongea kibali hakijapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kikwazo kingine cha pili, wizara hajatoa maelekezo ya namna ya usimamizi kutoka Wizara ya Maji kwenye Halmashauri husika, Halmashauri imeandika barua wameshapiga simu wamekuja wenyewe mpaka ofisini kwenu lakini majibu hayajapatikana mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kikwazo cha tatu katika mradi huu, *vetting* kutoka katika Mwanasheria Mkuu wa Serikali haijapata majibu Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Kwahiylo naiomba Wizara mtuambie, mradi huu wa Masengwa mna mpango nao gani? Kwa sababu mna utaratibu wenu wa matumizi ya fedha hizi za maji mna siku 21 sijui siku 35 siku hizi zikiisha manakwenda kuwanyang'anya Halmashauri fedha. Naomba majibu kwa nini wizara haitekelezi wala haijibu maandiko yanayoletwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niingie katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala... (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Bahati mbaya sana Mheshimiwa Azza.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** ...dakika tano! Nakushukuru naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Azza amesema Ushetu hakuna kijiji hata kimoja dah! Hebu mwangalie kwa huruma ndugu yangu huko, angekuwa na nafasi ya kusema leo angepasuka.

Mheshimiwa Katani Katani atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige.

**MHE. KATANI A. KATANI.** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na niombe tu kwa namna unavyoendesha mjadala kwa siku ya leo ingewezekana ungekalia kitisiku zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji linalozungumzwa ni tatizo la kitaifa, na kaka yangu Mheshimiwa Chikota wakati anachangia amejaribu kuzungumzia Mradi wa Maji wa Makonde, mradi ambao uliasisiwa mwaka 1953 katika Wilaya ya Newala, mwaka 1953 ilikuwa bado haijawa Wilaya maana Wilaya ya Newala imepatikana mwaka 1954 Mzee unajua. Mradi huu wakati unasisiwa ulikuwa unahudumia wakazi 82,000 tu; leo tunapozungumza Newala kuna watu zaidi ya 205,000, Tandahimba kuna watu zaidi ya 227,000. Nanyamaba ambako mradi unatakiwa uende kunazaidi ya watu zaidi ya 60,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukiangalia mradi huu kwa sasa, unahudumia watu zaidi ya laki saba. Hata hivyo mradi huu ukiuangalia kwenye bajeti, kuanzia mwaka 2016/17, 2017/2018 na mbaya zaidi tarehe 10 Septemba, 2016, mimi nilikuwa na Makamu wa Rais Tandahimba pale, amewaambia watu wa Mtwara kwa maana ya Newala, Tandahimba na Nanyamba kwamba Serikali imetenga shilingi bilioni 170 kwa ajili ya Mradi wa Maji wa Makonde.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo hii tunapozungumza ukiangalia kwenye makabrasha fedha iliyotengwa mwaka huu 2018/2019 ni shilingi bilioni moja. Sasa kuna majibu gani kwa wapiga kura wale wa maeneo ya Mtwara? Kuna maelezo gani ambayo yatawafanya watu wale waiaminini Serikali ya CCM? Na tatizo la maji ni tatizo kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, nimewahi kumwandikia barua, *message* zaidi ya tatu au nne Mheshimiwa Waziri, lakini mara ya mwisho hata Naibu Waziri nimewahi kumwambia, kwangu Tandhimba kuna Mradi wa Maji ya Mkwiti ambo unatekelezwa kwenye *lot* nne; *lot* ya kwanza mwaka 2016/2017 mkandarasi ameshasaini mkataba

na tayari ameshapeleka bomba zenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 1.4, *advance payment* hajapata, ameandika *certificate* ya pili ya kuomba shilingi bilioni 1.1 hajapata,

Mheshimiwa Spika, tunaingia kwenye bajeti nyengine wakati mkandarasi ameshapeleka vifaa tayari lakini yeye hajalipwa hata *advance payment* na ukiusoma mkataba baina ya Mkandarasi na Halmashauri, *advance payment* inapaswa ndani ya siku 28, leo tunaozungumza toka mwezi Februari fedha hii haijatoka.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui Waziri wa Fedha, maana niliuliza watu wa Wizara ya Maji wanasema taratibu zote zishakwenda Wizara ya Fedha, sasa sijui Wizara ya Fedha inauwezo ya kupata fedha ya kujenga viwanja vyta ndege bila ya kutoka kwenye bajeti, ya kununua ndege bila ya kuwepo kwenye bajeti lakini hawana uwezo wa kulipwa fedha ya maji ambayo ipo kwenye bajeti, sijui. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na hii sijui watu tunawaonea aibu Wizara ya Fedha, lakini kuna mambo mengi wanakwamisha ambayo hayana msingi kabisa. Wana uwezo wa kutafuta fedha za *maneuver* kwa kutengeneza vitu ambavyo haviko kwenye bajeti vyta kwenye bajeti hakuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeona mwaka jana Wizara ya Maji asilimia 22 tu ya fedha za maendeleo ndizo zimeenda; lakini ipo miradi zilitengwa pesa shilingi bilioni 35 zilmelipwa pesa zaidi ya shilingi bilioni 42. Kumbe mijitu hii ina pesa za kutosha kwa nini kwenye miradi ya maendeleo kama ya maji ambayo ndio uhai wa Tanzania zisiende fedha hizo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana, dada yangu Ashatu Mheshimiwa Waziri sijui ametukimbia hapa, alitakiwa hapa alitakiwa awepo mwenyewe, kwa sababu yeye ndio mshauri wa mambo ya fedha kwa Rais na kwa Baraza la Mawaziri. Atuambie kama mna fedha za kufanya mambo mengine, lakini hamna fedha za kutatua tatizo la maji ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna mtu alikuwa anachangia kwa kujipendekeza, mimi sjui kama Wabunge tuko *Serious* na Taifa letu, mtu anazungumza suala la bomba la maji mita 400? Mheshimiwa Waziri umefika Tandahimba, ukitoka Mkwiti kwenda Tandahimba kilometra 61 niambie wapi uliliona bomba? Halafu uniambie mita 400?

Mheshimiwa Spika, kilometra 61 mpaka unafika Wilayani hakuna bomba, anakuja mtu wa CCM anasema maji mita 400; mita 1000 hakuna bomba utazungumza mita 400? Tuwaonee huruma akina mama hawa, tuwaonee huruma Watanzania hawa kila anayesimama anazungumza wazi kabisa kwamba bila ya maji hakuna kinachowenza kuendelea, hivyo viwanda tunayoyasema kama bila ya maji hakuna viwanda, hili Bunge tunalolisema kama hatukuoga maji hatuwezi kuingia Bungeni, mbuzi tunaofunga, ng'ombe tunaofuga kama hawakunywa maji watakufa tu.

Mheshimiwa Spika, niombe sana nyie watu wa fedha mnakwamisha mambo mengi sana. Huyu mkandrasi wa kwangu sasa tunataingia mwaka 2018/2019 fedha ya mwaka 2017/2018 hajapata mpaka leo. Sasa hatimaye tutamlalamikia nani? kama fedha hajapewa na amepeleka bomba za shilingi bilioni 1.4 ziko *site*. Maana si wakandarasi wababaishaji yeye bomba ameshapeleka *site, advance payment* hajapata, hizo fedha za *certificate* ya shilingi bilioni 1.1 hajapewa. Kwa hiyo tatizo liko kwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, Sasa kwa sababu jambo la maji umeliona ni jambo la msingi sana, moja mimi siwezi kuunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara hii na ninaamini Wabunge wote kwenye shughuri pevu itatokea kwenye Wizara ya Maji, mimi ninaamini hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ipo miradi ambayo nataka Mheshimiwa Waziri ikiwezekana mtusaidie, ipo miradi mnaapeleka fedha mnakwenda kuzindua, mfano Mahuta pale, tulienda na Mheshimiwa Selemani Jafo akiwa Naibu Waziri, akaenda kuzindua Mradi wa Maji wa Mkupete ambao fedha zake zimeshalipwa. Ule mradi umezinduliwa mwaka

2016 mpaka leo tone la maji hakuna na mradi umezinduliwa, hizi fedha mnazopeleka mnapeleka kwa ajili gani? Kama mradi umekamilika na umezinduliwa na maji hakuna huu mradi unakwenda kwa nini?

Mheshimiwa Spika, hebu mtuambie miradi inaenda kwa nini? Mnasema imekalimika lakini maji watu hawapati huduma nini maana ya kukamilika? Tuambieni maana ya kukamilika kwa mradi, umeleta mradi unasema mradi umekamilika. Mradi huo hauna tofauti ukienda Mahea kuna mradi mwengine, kuna miradi wa Mahuta mmepeleka zaidi ya shilingi milioni 86, lakini miradi hii yote imekamilika lakini watu hawapati maji.

Sasa mtuambie mnaposema mradi umekamilika maana yake ni kukamilika tu kuona aidha mmejenga mabomba mmeweka mabwawa au kukamilika Watanzania wapate amaji? Tunaomba sana mtupe ufanuzi wa jambo hili kwa uzuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini bahati mbaya ukilisoma *book* lenu hili Mtwara tuna bahati mbaya sana. Katika mikoa ambayo bajeti ya maji ni ndogo, ni mkoa wa Mtwara. Tatizo la Mtwara ni nini? Miradi mnayotupa hewa, tunaozungumza wamakonde fedha hakuna, Kaka yangu Chikota amezungumzia mradi wa Ruvuma fedha mpaka sasa hakuna. Tuna tatizo gani watu wa Mtwara?

Mheshimiwa Spika, mimi nilidhani Mheshimiwa Rais alivyokuwa amezungumza watu wa Kusini, alijua kwamba Kusini tumeachwa nyuma kwa muda mrefu na tutapewa priority sasa kwa kuona kwamba vitu vya msingi vinavyokuja basi Kusini lazima tuwapelekee na wao waone wananzaika na matunda ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na mnajua wakati anatoa taarifa Mheshimiwa wa Liwale amezungumza, zipo fedha za wakulima haohao wa korosho zaidi ya shilingi bilioni 250 na kitu zimekwenda kwenye matumizi yasiyoleweka, lakini watu wake hawana maji. Watu wa Mtwara wanachangia pato

kubwa kwenye Taifa hili. Kwa miaka hii miwili/mitatu mfululizo ukiangalia *trends* ya Mtwara kutoka kwenye zao la Korosho hawakuwa watu wa kulilia maji leo, hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana, tumekuwa na ngnjera, mimi tangu nakua nimemkuta Mbunge wa kwanza ninayemjua, Mzee Nandonde, kila niliposikiliza hotuba yake alizungumzia suala ya maji, akaja Mzee Lutavi alizungumzia suala la maji, amekuja ndugu yangu Njwayo akazungumzia suala la maji, napita mimi nazungumzia suala la maji. (*Makofi*)

Mheshemiwa Spika, ebu nyie ndugu zetu wa CCM, mnisaidie jambo kubwa sana; kwenye mazingira yetu ya taifa letu kitu gani tutaweka kipaumbele kama si maji? Katika vitu vyote tulivyokuwa navyo maji nadhani ni jambo la msingi kuliko kitu kingine chochote. Kwa hiyo tuweke priority kwenye maji kwanza halafu tufanye mambo mengine; na tunauwezo kuamua tukasema kwamba mwaka huu baadhi ya bajeti fulani zisinde tuitekeleze bajeti ya maji... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Katani tunakushukuru, muda wako umeisha ahsante sana. (*Makofi*)

Jamani Mheshimiwa Kamwelwe tumpitishie tu bajeti hapo kesho, maana sasa mtamtwhisa, hii mizigo yote mnayosema ni ya huko nyuma. Sasa tukiwaonea Mheshimiwa Kamwelwe na Mheshimiwa Aweso nawaonea huruma ndugu zangu. Hii miradi hewa hata Kongwa ipo, yaani kila Mbunge hapa yaani lakini ndugu zetu wameikuta hiyo shughuli pevu, *at least* nao wanapata picha ya kujua mzigio walioubeba ni mzito kiasi gani, kwa hiyo tuwape ushirikiano kwa kweli. (*Makofi*)

Nilimtaja Mheshimiwa Ezekiel Maige, atafatiwa na Mheshimiwa Alex Gashaza baada ya ye ye tutaenda CHAADEMA.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukura sana na mimi kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagilaji.

Kwanza naomba nipongeze sana juhudzi zinazofanywa na Serikali hii Awamu Tano na kwa kiasi kikubwa kama ambavyo umesema kwamba kazi inayofanyika wa awamu hii inaonekana dhahiri. Yawezekana katika maeneo mengine yanaweza ikawa haijadhihirika sana lakini wanasesma unapotapa ni vizuri ukasema ukweli. Miradi ambayo imeanzishwa na inatekelezwa kwenye Jimbo langu la Msalala kwa sasa hivi ni mingi na mikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka mwaka 2014, tulikataa bajeti ya Wizara ya Maji hapa tukitaka fedha zitengwe kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na hasa vijiji viliiviyokuwa kandokando ya bomba kuu la Ziwa Victoria hadi Kahama na Shinyanga. Tuilipitishiwa fedha kwa ajili ya kuanza kutekelezwa mradi wa Kagongwa Isaka, shilingi bilioni nane, wakati ule Naibu Waziri akiwa Mheshimiwa Amos Makala Waziri wa Maji akiwa Mheshimiwa Profesa Maghembe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpaka mwaka 2015 mradi ule ulikuwa haujatekelezwa, mwaka 2015 Mheshimiwa Riasi John Pombe Magufuli amechukua nchi, akafika Isaka akasesma ndani ya miezi sita mradi huo utakuwa umeanza kutekelezwa. Tumesikia hapa kwamba sasa hivi wakandarasi wako karibu 40 wakitekeleza mradi huu. Naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, lakini nimpongezea pia Mheshimiwa Wazri na Naibu wake. Kwa kiasi kikubwa wanajitahidi sana kusimamia miradi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nisemee mawili tu ya ujumla ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wameyazungumzia; kwanza usimamizi wa miradi hii. Ni kweli ukisikia fedha zilizotengwa karibu katika kila mradi ni hela nyingi sana. Mradi wa Isaka zaidi ya shilingi bilioni ishirini, mradi wa Bulyanhulu bilioni karibia kumi na saba. Miradi yoote hii ukiangalia fedha zinaengwa na utekelezaji wake mara nyingi unakuwa

hauwiani. Mimi nishauri sana, Mheshimiwa Waziri umesikia jitahidi sana kuwa na mfumo mzuri wa usimamizi wa utekelezaj wa hii miradi, fedha ni nyngi lakini utekelezaji unakuwa haukidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, suala la pili nilitaka kumshauri Mheshimiwa Waziri na hasa Serikali kwa ujumla wake kwamba tukubali hili wazo la kuanzisha mfuko maalum wa maji utakaokuwa na wakala wake unaojitegemea. Tumeona mifumo ya namna hii ambavyo inafanya kazi vizuri kwenye maeneo mengine. Tumeona kwa mfano *REA* wanafanyakazi vizuri kwa sababu kwa kiasi kikubwa fedha zinatengwa na zinakwenda kwenye eneo maalum ambalo limelengwa kwa ajili hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunaona kwenye barabara *TANROADS* wanavyofanya kazi vizuri kwa sababu wana Mfuko wa Barabara. Pamoja na changamoto zinazokuwepo za kibajeti kiujumla, lakini angalau miradi inakwenda vizuri. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana, Waheshimiwa wengi wamesema na mimi nirudie ombi hilo kwamba ni vizuri sasa Serikali likakubali hili wazo la kuanzisha wakala maalum na mfuko maalum wa maji na hasa utakaokuwa unalenga vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vyando vimepekezwa, kwenye mafuta na maeneo mengine lakini kubwa ni kuwa na wakala maalum unajitegmea ili kutoka kwenye haya makucha ya kumtegemea Dkt. Mpango kila wakati ambaye mwisho wa siku anawapa asilimia 22.

Mheshimiwa Spika, wakiwa na mfuko unaojitegemea hawatapeleka kwa Dkt. Mpango au wakipeleka wanajua kabisa mfuko wa maji zimekusanya kiasi fulani lazima zitapelekwa bila kusumbuliwa kama inavyotokea sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu la ujumla nilitaka kushauri pia juhudzi ziongezwe katika *schemes* za umwagilaiji, ziwe nyngi zaidi. Tumeona mvua zilivyo nyngi lakini mwisho wa mwaka utajikuta tena kuna maeneo mengine

tunalalamika kuna tatizo njaa kwa sababu maji yanatiririka mikoa ya Dodoma, Mikoa ya Shinyanga, hii yenye ukame, yanatiririka lakini hakuna namna ya kuyatunza kwa kilimo cha umwagilaji.

Mheshimiwa Spika, niombe sana Mikoa hii ya Shinyanga na Dodoma iwe na *schemes* maalum kwa ajili ya kufanya kilimo cha umwagilaji ili tuweze kuondokana na tatizo hili. Kwetu pale Msalala tulikuwa tumeshaanzisha tangu mwaka 2014 ulikuwepo mradi wa *scheme* za umwagiliaji, Mradi wa Kahanga ulikuwepo sasa hivi kwa Halmashauri ya mji pamoja na mradi wa Chela. Miradi hii ilitengewa fedha hazikutoka zote na haukutekelezwa. Nikuombe Mheshimiwa Waziri utakapopata nafasi ukija Kahama tukumbushane ili uweze kutembelea mradi wa umwagilaji *scheme* ya Chela. Utasikitika kwa sababu umeachwa asilimia 40 ya utekelezaji wake, fedha zimepotea, umwagiliaji haufanyiki na hakuna chochote kilichofanyika na ilikuwa ahadi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda alikuja Chela wakati huo na akasema mradi huo ungefanyika. Kwa hiyo, haya matatu nilitaka niombe sana Wizara izingatie.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwemye miradi ya Msalala, kama ambavyo nimesema miradi ipo mingi, wasiwasi wangu ni utekelezaji wake kwa ukamilifu. Tuna mradi huu isaka kama ambavyo nimegusia, una awamu mbili, awamu ya kwanza inakwenda vizuri, lakini kuna hofu awamu ambayo inahusu usambazaji kwenye vijiji vilivyo kandokando ya bomba kuu, ukachelewa kutekelezwa kwa sababu ya huu mwenendo ambao tunao katika upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa mradi wenywewe.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuomba sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yako na Katibu Mkuu yupo hapa na rafiki yangu Mhandisi Karobero - Naibu Katibu Mkuu, wote kwa ujumla sasa muanze utekelezaji wa awamu ya pili kama tulivyokuwa tumekubaliana. Awamu ya kwanza ikifika asilimia 40; awamu ya pili iweze kuanza ili wananchi wa Kata za Mwalugulu, Isakajana waweze kupata maji kwa sababu kwa sasa hivi maji yanapita kwenye kata hizo lakini watapata

wananchi wa Isaka Mjini na wananchi wa Kagonga Mjini, lakini Kata ya Isagehe, Mwalugulu, Isakajana hazitapata maji na ziko ndani ya kilometra nane/sita; chini ya kilometra 12. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni huu niliyougusia wa Bulyanhulu kutoka Manghu kwenda Bulyanhulu. Mradi huu nao tulikubaliana utekelezwe kwa ushirikiano baina ya Serikali na mwekezaji wa ACACIA. Nkuombe Mheshimiwa Waziri, ACACIA mimi nawafahamu, nimefanya nao kazi miaka yote, *commitment* yao ilikuwa kutoa dola milioni mbili, nadhani mnafahamu; mpaka hivi tunavyozungumza tumesaini mkataba na mkandarasi toka mwezi Desemba, mpaka sasa hivi hata *advance* haijatoka lakini ACACIA alishatenga dola milioni mbili, zaidi ya bilioni tano ambazo ziko lakini hazijatoka.

Kwa hiyo, nilitaka kuomba tu kwamba muwe macho na huyu mwekezaji, hakikisheni hizi fedha kweli zimetoka, ziko kwenye mfuko amba Serikali inaweza ikazi-access na ikatumia kulipa wakandarasi, vinginevyo tutapigwa changa la macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulishaahidiwa mambo mengi kule, mimi nawajua na nimekuwa nikiwalalamikia hapa kila wakati. Kwa hiyo, tutauita mradi wa amoja kati ya ACACIA na Serikali lakini mwisho wa siku utakuwa ni mradi wa Serikali peke yake. Kwa hiyo, nataka kuhimiza hilo, Serikali mlione na mzingatie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia awamu ya pili ya mradi huu, kama nilivyosema ule wa Isaka nao una sura hii hii, kwamba unapita kwenye vijiji, lakini tulikubaliana *phase* ya kwanza angalau bomba kuu liweze kufika llogi, vijiji vya pembezoni havipati maji. Itakuwa ni tatizo kubwa pale mradi utakapokuwa umefika, bomba kuu lipo, vijiji viko pembezoni havipati. Utekelezaji wa awamu ya pili unaosambaza maji pembezoni mwa hilo bomba kuu na kusogeza mradi huo hadi Lunguya kama tulivyokuwa tumekubaliana nao uweze kuanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, hatua za utekelezaji awamu ya pili ya miradi wa Isaka na Bulyanhulu ianze sasa hivi kwa sababu *commitment* tulioiweka kwa wananchi ni kwamba ifikapo mwaka 2020 wananchi wa Kata za Bulyanhulu, Bugarama, Lunguya, Busangi, Kashishi, Isaka, Mwalugulu na Isakajana wawe wamepata maji. Leo ni mwaka 2018 bado mwaka mmoja na nusu au miwili muda huu umefika wa kuja kuulizwa tumefikia wapi. Sipendi ifike wakati huo tuanze kuulizwa maswali ambayo tungeweza kuyaepuka kwa sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nakubaliana, naunga mkono...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE: EZEKIEL M. MAIGE:** Nashukuru sana, kama nilivyosema naunga mkono bajeti, niombe tu Waziri asimamie awamu hizi zitekelezwe kwa ukamilifu. Nashukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Magolyo. Mheshimiwa Alex Gashaza. Atafuatiwa na Wabunge wa dakika tano tano upande wa CHADEMA Mheshimiwa Marwa Ryoba na Mhesimiwa Anna Gidary.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi hii na kunijaalia uzima na afya, lakini pia nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu Wizara hii, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi kwa kazi kubwa wanayoifanya na nzuri. Tunajua zipo changamoto kadha wa kadha ambazo huwezi kuzikwepa.

Nichukue nafasi hii pia kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano kwa kazi ambayo inafanyika chini ya Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikianza na miradi ya maji, Wabunge wengi wamelalamika kuona jinsi ambavyo miradi mingi ya maji ambayo imeanza kwa muda mrefu hasa miradi ile ya vijiji kumi, imechukua muda mrefu kukamilika. Niombe kwa sababu hili limejitokeza pia hata kwenye Jimbo langu la Ngara, miradi ile ya vijiji kumi bado mpaka sasa hivi haijakamilika. Niombe kwamba sasa tuweke nguvu kubwa katika miradi hii ambayo tumewekeza fedha nyngi takribani shilingi bilioni 5.1 kwenye Wilaya yangu ya Ngara iweze kukamilika ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, sambamba na miradi hiyo ya vijiji kumi, kuna vijiji villiongezwa kufikia 13 ambavyo ni vijiji vya Kabalenzi, Murugarama na Kumbuga Kata ya Nyamagoma. Vijiji viwili kati ya hivyo vipo kwenye programu inayoendelea na miradi inakaribia kukamilika. Kipo kijiji cha Kumbuga, Kata ya Nyamagoma, vilichimbwa visima vitatu tangu mwaka 2014 wakamaliza kuchimba lakini pampu hazikufungwa wala *DP* hazikujengwa ili kuwafikia watumiaji. Kwa hiyo mradi ukatelekezwa. Niombe sasa kwamba mradi huu wa kijiji hiki cha Kumbuga ambapo wananchi wanahangaika, wanatembea zaidi ya kilometra 16 kwa maana ya kilometra nane kwenda na kurudi kufuata maji, mradi huu ukamillike, zinunuliwe pampu zifungwe na *DP* zijengwe ili wananchi waweze kupata huduma za maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba hili litafanyika kwa sababu mmeniongezea pia miradi ya vijiji vitatu; Kijiji cha Mrugina, Mkariza Kata ya Mabawe na Kijiji na Kanyinya Kata ya Mbuba. Kwa maelekezo yaliyotolewa ni kwamba mradi huu wa Kumbuga utaunganishwa kwenye vijiji hivyo, niombi basi kwa sababu tayari wataalam wako *site* kwa ajili ya kufanya *survey* kwenye vijiji hivi vitatu na baada ya hapa watatengeneza *BOQ* kwa ajili ya kutangaza *tender*, niombi kijiji hiki cha Kumbuga kisisahaulike, kiunganishwe ili iweze kufanyishwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka jana aipotembelea Ngara tuliomba *pump* akatupatia shilingi milioni 13, tukaomba shilingi milioni 24 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji mjini, tukapewa. Vile vile akatupatia shilingi milioni 75 kwa ajili ya eneo la K9 ambapo kuna kiteule cha Jeshi pamoja na shule mbili za sekondari. Mradi huu unaendelea vizuri, wameshafunga *pump*, umeme umeshafika kwa hiyo tunaamini kwamba wananchi wataanza kunufaika muda si mrefu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kuna mradi mkubwa ambao niliomba wa kutumia chanzo cha Mto Ruvuvu na kutumia kilele cha mlima Shunga ambao ndio mlima mrefu kuliko milima yote Mkoa wa Kagera ambapo yakijengwa matenki makubwa pale yanaweza yakapeleka maji kwa mtiririko na kwa gharama nafuu Wilaya nzima ya Ngara, Biharamulo, Karagwe kuendelea mpaka hata Mkoa wa Geita kwa maana ya Mbogwe, Bukombe mpaka Chato. Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikifuatilia juu ya hili, nishukuru kwa ushirikiano ambao umenipa na Katibu Mkuu na niliahidiwa kwamba zitatengwa shilingi milioni 200 kwa ajii ya kuanza usanifu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nimejaribu kuangalia kitabu cha bajeti nimeona fedha za jumla, kwamba kwenye Jimbo langu la Ngara wamenitengea shilingi bilioni 1.7, kati ya hizo shilingi bilioni 1.05 ikiwa ni fedha za ndani. Hakuna mchanganuo lakini nitaomba Waziri atakapokuja kuhitimisha basi unipe ufanuzi kama hizi shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuanza usanifu wa mradi huu zitakuwa ziko kwenye fungu hili ili angalau niweze kupata amani na wananchi wa Jimbo la Ngara waweze kuamini kwamba sasa tatizo la maji likuwa historia katika Wilaya yetu ya Ngara na Wilaya jirani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimeona katika ukurasa wa 195 katika miradi ile itakayotekelezwa katiak mikoa 17 ukiwemo Mkoa wa Kagera ni Mradi wa Rusumo ambao umeelezwa hapa. Mradi huu najua kwamba utatekelezwa katika vijiji vitano; vijiji vitatu vya Kata ya Rusumo ambavyo ni

Nyakahanga, Mshikamano na Kasharazi na vijiji viwili Kata ya Kasulu ambavyo ni Rwakalemela na Nyakariba na hapa imeonesha kwamba fedha hizi zilizotengwa, takriban shilingi bilioni moja ni kwa ajili ya mikoa hii 17.

Mheshimiwa Spika, nitaomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho basi niweze kuelezwu kwamba kwenye mradi huu wa Rusumo ambao utatekelezwa kwa ubia wa Serikali na *NELSA* ni kiasi gani ambacho tumekuwa tumetengewa kwa ajili ya kuanza kufanya *feasibility study, detailed design* na kutangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye umwagiliaji, nchi ya Misri wanatajirika na uchumi unakua kwa kasi kutokana na kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia Bonde la Mto Nile. Mto Nile asili yake inatokewa kwetu huku Ngara, mto Kagera na Ruvuvu ambayo inapoungana ikaingia kwenye Ziwa Victoria, ndio inaenda kutengeneza mto Nile kule, sisi huku mito hii hatujaitendea haki. Sasa naomba kwamba kwenye upande wa umwagiliaji tuwekeze hapo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *scheme* ya umwagiliaji nchi nzima tumeshatumia tu asilimia 1.6 kwa hekta zaidi ya milioni 29 ambazo zinaweza zikafanya kilimo hiki. Niombe kwamba tuweze kutumia fursa hizi ili kuweza kuinua uchumi kwa kutumia *scheme* za umwagiliaji. Ipo *scheme* ya umwagiliaji ya Bhigomba ambayo ilishaanza tangu mwaka 1913, ilitakiwa ikamilike 2014, ilianza mwaka 2013 ikamilike 2014. Ilitumia gharama ya shilingi milioni 715 ambayo ilitakiwa kukamilisha mradi, lakini mpaka sasa hivi huo mradi haujakamilika, umetekelizwa. Ukienda kufanya tathmini sasa hivi, kwa tathmini iliyofanyika mwaka juzi inaonekana inahitajika karibuni shilingi milioni 185 ili kukamilisha mradi huo. Niombe kwamba sasa Wizara ya Maji kuukamilisha mradi huu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba mwezi uliopita tumepokea *delegation* kutoka *Kuwait Fund* kwa ajili ya kuangalia bonde la Mhongo, ili kuanza usanifu wa *scheme*

ya umwagiliaji katika bonde hili. Niombe kwa sababu tunazo fursa, tuna zaidi ya hekta 5,000 katika Wilaya yetu ya Ngara ambapo tukiweza tuzitumie kwa *scheme* hii ya umwagiliaji. Kuna *scheme* tano ambazo tayari Serikali tulishaziingiza kwenye mpango.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 tulitengewa bilioni mbili kwa ajili ya *scheme* ya umwagiliaji ya Mgozi, Kata ya Mbuba na Mhongo, Kata ya Bukirio lakini fedha hizo hazikutoka. *Scheme* ya umwagiliaji kwenye bonde hili la Mgozi hata kwenye bajeti hii ya mwaka huu haikuwekwa. Kwa hiyo niombe, kwa sababu ni fursa ambazo zinaweza zikainua uchumi wa wananchi wa Jimbo la Ngara ambao zaidi ya asilimia 80 ni wakulima basi tuwekeze hapo ili kusudi tuanze *scheme* hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba yapo mazao ambayo unaweza kulima katika maeneo ya kawaida, lakini yapo mazao ambayo huwezi kulima kwenye *highlands*, inatakiwa yalimwe kwenye maeneo ya mabonde ambapo unaweza ukafanya umwagiliaji na Ngara tumejipanga kwa sababu yapo mazao ambayo tunaendelea kufanya utafiti ambayo tunaamini tukipata kilimo hiki cha umwagiliaji unaweza ukatumia hekta moja ukawa tajiri kama mazao haya ni kama vile *stevia* na *chia seeds*, Waheshimiwa wanajua kwamba tunaweza tukainua uchumi wa wananchi wetu, vile vile tukaboresha hali ya lishe na tukachangia Pato la Taifa. Kwa hiyo, niombe tuwekeze kwenye *scheme* za umwagiliaji ili kusudi tuweze kuinua kipato cha wananchi wetu na pia tuinue uchumi wa Watanzania, ikiwa ni pamoa na kupata malighafi za kulisha viwanda vyetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niunge mkono uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijijini, hii itakuwa ni suluhishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja bajeti hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana nashukuru. Waheshimiwa Wabunge mnaoendelea kuchangia, ni vizuri mnapotaja vijiji

vyenu mkavitaja vizuri maana watu wangu wa *Hansard* wamelalamika kidogo hasa haya majina ya baadhi ya vijiji vya Usukmani huko, Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Magolyo kule, Mheshimiwa Masele, dada yao Azza, *Hansard* haijashika maana majina ya Kisukuma sijui yakoje yakoje, mtamke sawa sawa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Marwa Ryoba atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Gidarya.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kama kuna wakati Serikali ya CCM imewahi kupigwa upofu na Mungu basi ni wakati huu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, maji ni siasa, maji ndiyo kila kitu nchi hili; na kama ukitaka uendelee kuwepo madarakani, hakikisha ya kwamba umewapelekea Watanzania maji. Ukienda vijijini wananchi wanalia, wanalalamika maji, ukienda mijini wananchi wanalia wanalalamika maji. Lakini unashangaa watu hawa hawaoni, hawasikii, hawaelewi! Fedha nydingi wamepeleka sijui wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitamani Waziri wa Fedha awepo hapa, naona hayupo, maana huyu ndiye tatizo. Nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Kilimo na Maji, kilio kilikuwa ni hiki hiki tangu niingie Bungeni mpaka leo, fedhahaziendi.

Mheshimiwa Spika, walitenga zaidi ya shilingi bilioni mia sita haziendi, leo wanaleta tena. Shida si hawa Mawaziri waliokaa hapo, shida ni huyu Waziri wa Fedha na Naibu wake, hawa ndio tunatakiwa tuwasulubu kweli kweli. Kwa hiyo, mimi niwashukuru sana Waziri wa Maji na Naibu wake, wanajitahidi, wanafanya kazi nzuri ila wanaangushwa na huyu mtu huwa anakaa hapa. Sasa amekimbia ngoja nimuache. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alikuja Serengeti, akauna ule mradi wa maji pale Mugumu, una zaidi ya miaka mitano. Kama asingekuja kwenye mradi ule

maana yake hakuna chochote ambacho kingekuwa kinaendelea pale, lakini ujio wake umesababisha mambo sasa yaende vizuri. Ni ushauri tu kwamba jitahidini, kwa sababu ninyi ndiyo mnatoa fedha, jitahidini iwezekanavyo, nendeni kwenye miradi yote nchi nzima. Ni bahati mbaya sana hamna chombo kinachosimamia kwa niaba yenu. Ulikuja Serengeti, ulienda kwenye ule Mradi wa Mugumu. Kuna Mradi wa Maji Nyagasense, ultumia zaidi ya shilingi bilioni 500 mpaka ninavyoongea hakuna maji! Imetulazimu kama Halmashauri tuutangaze upya, lakini fedha za wananchi zilishatumika pale.

Mheshimiwa Spika, kuna Mradi wa Maji Kata ya Kibanchebanche, Kijiji cha Kibanchebanche, mradi ule umetumia shilingi milioni 557 na kampuni iliyokuwa inajenga mradi ule inaitwa *Gross Investment Company*, wamejenga DP, wamejenga tank, power house lakini chanzo cha maji hakuna, na mkandarasi alishatokomea na ndiyo maana nilikuwa nalia Mheshimiwa Waziri ungefika pale Serengeti nikakupeleka mwenyewe ukaona pesa zimechukuliwa, lakini chanzo cha kuleta maji kwenye tenki hakipo mpaka leo na hakuna chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuombe wa hili Mheshimiwa Waziri, ama wewe ama naibu wako, naomba aje twende Serengeti akajionee mwenyewe, lakini wakati anakuja aje na wataalam wake na hatua ya nini kifanyike kwa ajili ya ku-rescue hizi shilingi milioni 557 ambazo zimetumika lakini hakuna maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, pia niombe wakati unapokuja kujibu, kuna zile fedha ambazo ni mkopo kutoka Serikali ya India, nataka kujua zimekwamia wapi? Maana tangu bajeti ya kwanza tulianza kuzungumzia fedha za mkopo kutoka Serikali ya India, imepita miaka hiyo mpaka leo hazijulikani. Kwa hiyo naomba unapokuja ku-wind up ueleze wananchi wa Mugumu ni lini watasambaziwa maji maana Mradi wa Maji Mugumu ni moja ya miradi ambayo ilikuwa inapata hizi fedha za kutoka India.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja pia aje na ufanuzi. Mradi wa maji Mugumu uko *class* gani. Najua uko *class C*, je, unastahili kupewa ruzuku kwa ajili ya kulipia umeme? Na kama unastahili kupewa ruzuku, nani yuko *responsible* na kulipa hiyo fedha maana wananchi wanapata shida, kila siku tunachangishana tu kwa ajili ya kulipia maji lakini ni mradi ambao unastahili kupewa ruzuku na Serikali kwa ajili ya kulipia *bill*.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, mimi niwashukuru mnafanya kaz nzuri lakini mnatakiwa kwenda mradi mmoja baada ya mwingine. Ahsante sana nashukuru. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Marwa Ryoba, Mbunge wa Serengeti. Mheshimiwa Anna Gidarya atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Badwel na Mheshimiwa Hassan Masala.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi naomba nichangie katika Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji katika maeneo mawili.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai wa kila kiumbe chenye uhai katika uso wa dunia, lakini nchi yetu imekuwa ni kinyume na matarajio, maji yamegeuka kuwa mtego wa umaskini kwa uchumi wa Mtanzania wa kawaida. Maskini analipia maji *bill* kubwa kuliko mtu mwenye uwezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja kutokana na muda naomba niende kwenye mpango wa maji vijiji. Tuna vijiji vingi katika nchi hii ambavyo havina maji tofauti na sisi tunaokaa katika maeneo ya mjini. Naomba nitolee mifano miwili tu katika Mkoa wangu wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia pato la kawaida la Mtanzania kwa mwaka ni shilingi 2,131,299; hii ni kutokana na takwimu ya Juni, 2017 ili uone ni jinsi gani tuna hali mbaya katika sekta hii ya maji, tuna vijiji katika Wilaya ya Hanang, tuna vijiji vinaitwa Gehandu na Laganga, vijiji hivi umbali

wa kupata maji ni kuanzia kilometra mbili mpaka kilometra nne watu wanatafuta maji. Hata hivyo pale unapopata hayo maji pipa la lita 200 ni shilingi 7,000. Sasa ndio ujulize ukiwa na familia ya watu sita utakuwa unagharmia katika uchumi wako shilingi ngapi? Halikadhalika vijiji nya Endakiso na Nkaiti maji yanauzwa kwa gharama hizo hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pato la huyu mkulima na mwananchi wa kawaida badala ya kufanya masuala ya kiuchumi pato lake linaishia katika manunuzi ya maji. Hapa tunasifiana, lakini hata Biblia inasema kusifu kunawapasa wanyoofu wa moyo, hivi mnasifu nini katika hili? Wanaokufa ni akina nani? Tuna watoto tuna ndugu zetu, hata kama sisi tunaishi mjini, tumewaacha babu zetu na mama zetu huko nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, familia moja inahitaji angalao pipa moja kwa kubana matumizi, lakini mwananchi huyu anahitaji takribani shilingi milioni 2.5 kwa mwaka ili watoto wake wale, waoge, wapige mswaki na matumizi mengine, lakini pia familia ya watu sita wastani wa hicho kipato ni asilimia 16 ya kipato cha kila mwanafamilia. Kwa muktadha huu hata mtoto aliyezaliwa leo wa siku moja anahuksika katika manunuzi ya maji. Hebu tujiulize kwa Tanzania nzima na vijiji vyote hali hii ya adha ya maji uchumi wa Watanzania tumeukuba kiasi gani na tumewarudisha kiasi gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba Waziri utakapokuja utuambie umeongea vipi na watu hao wa Wizara ya Fedha? Tunajua tatizo haliko kwenu, tatizo liko Hazina. Kwenye Kamati za kisekta watu wa Hazina wanakuwepo, mara waje kwanza na ukomo wa bajeti, mmeweka ukomo wa bajeti kile kidogo mllichokiweka hamkitoi. Kwa nini mnatuchosha kukaa kwenye Kamati tunachambua nini? Unawezaje kuwa na akili nzuri hujaoga, hujala, wewe utapata wapi hiyo afya? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Gidarya.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Omary Badwel kama nilivyosema atafuatiwa Mheshimiwa Hassan Masala. Mheshimiwa Badwel tafadhalii.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana mheshimia Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri ambaao kwa kweli, wametoa ushirikiano mzuri sana kwangu katika kipindi chote ambacho wamekuwa Mawaziri. Wamefika kwangu Bahi kwa nyakati tofauti na Mheshimiwa Waziri hivi ameniahidi Jumamosi ijayo tena anakuja Bahi. Kwa hiyo, kwa kweli nina kila sababu ya kuwashukuru na matokeo ya ujio wao pia yameonekana kwa sababu pale Mji wa Bahi tumekuwa na shida ya maji kwa muda mrefu sana, lakini Mheshimiwa Waziri aliruhusu pesa shilingi milioni 400 katika bajeti hii ambayo tunakwendanayo na kwa kweli, watu wa Bahi wameanza kupata maji angalau kwa kiwango kidogo, lakini maji yameanza kutoka na kwa mara ya kwanza watu wa Bahi wameyaona maji ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika bajeti hii nimeona wametuungezea shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Maji wa Bahi, ingawaje fedha hizo hazitoshii, na Mheshimiwa Waziri kwa kuwa unakuja basi utaona namna ambavyo tutakuomba kule Bahi. Ninaamini utashirikiana na sisi kama ambavyo umeshirikiana kukamilisha kabisa ule Mradi wa Maji wa Bahi, mji ambaao unakua kwa kasi ili watu waweze kuyatumia maji kwa shughuli mbalimbali za maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini Wizara ilitupa fedha ya kuchimba visima vitano katika mwaka huu wa fedha ambaao tunakwendanao na tayari tumechimba visima vitatu katika vijiji vya Ilindi, Bahi Makulu na Mpamata. Sasa tunakwenda kuchimba katika Kijiji cha Ikungulu na Lamaiti. Katika bajeti ambayo tunakuja sasa kwa kuwa mlitupa fedha za kuchimba visima katika vijiji vitano bila *pump*, lakini naona

mmetuwekea sasa katika hivi vijiji vitano, safari hii mmetuwekea fedha shilingi milioni 100 kwa kijiji kimoja cha llindi. Sasa nilikuwa nataka njue Mheshimiwa Waziri umetupa mwaka jana fedha za kuchimba visima vitano, tumeshachimba vitatu na tunakwenda kuchimba viwili vingine na vitakuwa vitano ambavyo havina *pump*, lakini kwenye bajeti hii unatoa tu kisima kimoja kama tukafunge *pump* kwa maana ya kisima cha Kijiji cha llindi. Nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Waziri kama umesahau vijiji viko vitano, basi niongezee hivyo vijiji vinne pia navyo tupate fedha kwa ajili ya kufunga *pump* ili wananchi wameona visima vimechimbwa wawee kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Iakini pia, viko vijiji kadhaa ambavyo navyo vina shida kubwa katika Wilaya ya Bahi na hususan kwa sababu Wilaya ya Bahi ile ni Wilaya ya ukame, ningeomba pia katika vijiji baadaye utakaapopanga bajeti zako vijiji vya Chikola, Chonde, Ikumbulu, Chifutuka, Chaliigongo, Chikopelo, Chalisanga na Mkola navyo kwa kweli uweze kuvipata fedha kwa ajili ya uchimbaji wa visima.

Mheshimiwa Spika, Iakini kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri cha hotuba yake katika ukurasa wa 273 ziko taarifa ambazo mimi nataka nimwambie taarifa zile si sahihi. Nimeona kwamba katika mradi ule wa visima vilivyo chimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*)imeonesha pale kwenye ukurasa wa 273 kwamba kwenye Wilaya yangu ya Bahi viko vijiji vya Mzogole ambapo kuna kisima namba 278 kwa kupitia Mkandarasi Godwin Mwasombwa na kijiji cha Zejele namba 279 kupitia Mkandarasi Emmanuel Nyaumba kwamba vijiji hivyo vimkechimbiwa visima na kwa bahati mbaya visima vimekutwa havina maji.

Mheshimiwa Spika, jambo hili sio kweli Mheshimiwa Waziri. Kama nkuna watu walikupa taarifa hizi wamekudanganya kwa sababu mimi binafsi nimeshituka kuona hapa kwenye kitabu chako kwamba mmetuchimbia hivyo visima katika Vijiji vya Mzogole na Zejele lakini hakuna maji. Nikafanya utafiti, nimewasiliana na uongozi wa kijiji,

nimewasiliana na Mheshimiwa Diwani, Mhandisi wa Maji wa Wilaya na Mkurugenzi, wote wamenijibu kuwa jambo hili halikufanyika. Kwa hiyo, nilikuwa naomba jambo hili wakati unajibu hoja mbalimbali za Wabunge na mimi unijibu kumetokea kitu gani zimeletwa taarifa hapa ambazo si sahihi. Kama ahawajachimba na fedha hizi zipo waende wakachimbe visima hivi na nina uhakika maeneo haya watapata maji.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati tunaendelea na miradi hii ya maji ni vizuri pia tukaiangalia kwa jicho lingine miradi ya umwagiliaji. Kwa mfano sisi watu wa Dodoma kila mtu anajua namna ya ukame wa Dodoma, hata watu mwaka huu wameshangaa kuona mvua kubwa namna hii, ni baraka tu za Mwenyezi Mungu. Lakini kwa kweli tuna shida kubwa ya ukame na mkombozi pekee kwenye Wilaya hizi za Dodoma, hususan Wilaya yangu ya Bahi ni kuwa na killimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, tunazo skimu kumi pale katika Wilaya yetu ya Bahi, lakini skimu hizi miongoni mwao zimechakaa, ni za muda mrefu, hazikutengenezwa kwa kiwango kizuri na skimu hizi zinazhitaji matengenezo makubwa. Katika bajeti iliyopita nilipata nafasi hapa ya kuchangia, nikaomba Wizara ije itume wataalam wake kuja kufanya tathmini ya kina kujua hii miradi ya umwagiliaji Bahi hasa mahitaji yake ni nini maana imepitwa na wakati. Miradi hiyo ni Bahi Sokoni, Nguvumali, Matajira, Mtazamo, Mtitaa, Uhelela, Chikopelo, Kongogo, Lubala na Uhelela. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri safari ile hukutuma hiyo timu, lakini safari hii naomba utume timu Bahi ije ione miradi hii inahitaji mahitaji gani ili iweze kuendelezwa na sisi wananchi ambaao wilaya yetu ni ya ukame tuweze kuitumia kikamilifu kupata chakula na tuepukane na omboomba ya chakula kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, uko Mradi wa Kongogo ambaao umeniahidi Jumamosi ijayo unakuja kuutembelea. Huu ni mradi wa muda mrefu wa bwawa na sehemu nyingine

inataka kwenda kumwagilia. Ni mradi ambao umekuwa ukilalamikiwa na wananchi muda mrefu, umetumia fedha nylingi na umeniahidhi kwamba utafika siku ya Jumamosi. Mimi mwenzio nilipokwenda mara ya mwisho nilipokelewa na mabango juu ya namna ambavyo watu hawakuridhika na utengenezaji wa Mradi huu wa Kongogo. Sasa siwatumi hapa waje na mabango siku ya Jumamosi utakapokuja, lakini watakuwa ujumbe wa namna ambayo wamesikitishwa na kuchelewa kukamilika na kutokuridhika kwa kiwango cha mradi huu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lakini gharama za miradi ya maji zimeelezwa na Waheshimiwa Wabunge hapa na mimi mwaka jana niliwahi kusema jambo hili kwa kweli gharama za miradi ya maji ni gharama kubwa mno. Wako baadhi ya wataalam wetu si waaminifu, wamekuwa wakishirikiana na wakandarasi kuhakikisha kuongeza kiasi cha fedha cha miradi hii na imekuwa ni vigumu sana. Mimi naamini kama miradi hii ingetafutiwa njia bora ya utekelezaji kwa miaka yote hii leo tusingekuwa na kilio hiki tunacholia hapa. Kilio hiki tunacholia kimesababishwa na sehemu ya wataalam wetu na wakandarasi ambao sio waaminifu, lakini pia na usimamizi hafifu na Wizara kutokujituma kutaka kubadilika na wakati kwamba, hivi kwa nini kila siku tunalia kilio hicho hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vizuri na mimi nakubaliana, na umezungumza vizuri asubuhi kwamba miradi ya shilingi milioni 600, shilingi milioni 700 ni miradi ambayo imeumiza wananchi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, umekuwa ukiunda tume hizi na zimekuwa zikifanya kazi nzuri sana, hebu tubadilike na kwenda kwenye tume ambayo itachunguza utekelezaji wa miradi ya maji. Uunde Tume hapa ya Kibunge iende ikaangalie namna ya kutengeneza miradi inavyotengenezwa, ifanye tathmini ya muda, gharama, kwa nini miradi ya umeme tunaambiwa ukienda kilometra kadhaa ni shilingi kadhaa, lakini miradi ya maji huwezi kukuta hiyo habari, kila mtu anajipangia vile anavyoona ye ye inafaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima jambo hili kwa kweli liangaliwe kwa kina, kiki fedha zitumike chache, lakini zenye tija, vifaa bora na wananchi waweze kupata huduma hii ya maji kama ambavyo inasisitizwa na Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi nakuomba sana hebu uunda tume itakayochunguza miradi ya maji tuisaidie Serikali. Tume ile ya Wabunge itakuja na mapendekezo na hapa tunapofikiria kuunda huu Wakala wa Maji Vijijiini uwe na kitu cha kuanzia kwamba inakwenda kusimamia kitu gani ambacho kimechunguzwa kikamilifu na kimetolewa maelekezo na kinaweza kutoa tija na ufanisi, ili wananchi wetu hawa wasiendelee kulia kilio cha kukosa maji.

Mheshimiwa Spika, tunayo Tume ya Umwagiliaji, kwa kweli imekuwa na watumishi wachache na yule bosi wao anakaimu leo mwaka wa tatu, sijui ni mwaka wa nne, inakuwaje mtu anaweza kukaimu miaka yote hiyo na mtu anafanya kazi vizuri, anachapa kazi vizuri, tunashirikiana na Ye vizuri? Mpeni nafasi ya kuwa Mkurugenzi kamili, ili aweze kujiamini na kufanya kazi ile kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono tozo ya shilingi 50 iongezwe kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameshauri, ili iweze kuongeza kiwango cha fedha ambacho kitatusaidia sana katika utekelezaji wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. asante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hassan Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Maji. Naomba niungane na waliotangulia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na msaidizi wake, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo amekuwa anaifanya katika

kuhakikisha Watanzania wanapata huduma hii muhimu ya maji.

Mheshimiwa Spika, kipindi chote ambacho nimekuwa nasimama hapa nimekuwa ni mtu wa kuomba tu juu ya mahitaji ya jimbo ambalo ninaliongoza, lakini katika Wizara hii nitakuwa mtovu wa fadhila kama sitatoa neno la shukrani kwa Mheshimiwa Waziri, Mzee wangu Mheshimiwa Kamwelwe, kwa kweli, ametitendea haki watu wa Wilaya ya Nachingwea, mara zote ambazo tumemuomba mahitaji yetu amekuwa ni msikivu, lakini pia amekuwa ni mtu ambaye amejali sana kwa kufanya ziara si chini ya mara tatu katika Wilaya yangu ya Nachingwea kuja kuona hali ya upatikanaji wa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika hili nilikuwa naomba kabisa nimpongeze na nintakie kila la heri mzee wangu kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na tunaendelea kumuombea mambo mazuri zaidi ya hapo alipo ili ikiwezekana basi mambo yakae sawa.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo ambayo kimsingi tuliomba, moja ni eneo la utanuzi wa mtandao wa maji ya Mbwinji. Kwa mwaka jana alitutengea shilingi bilioni moja na katika fedha ile tulipata zaidi ya shilingi milioni 870 na hii imetuwezesha kutanua maji. Katika Wilaya yangu mimi viko vijiji takribani nane ambavyo toka uhuru wa nchi hii upatikane hawakuwahi kupata maji safi na salama, lakini sasahivi tunavyozungumza wananchi wa Kata za Naipanga, Rahaleo, Chiwindi, Nkotokuyana, Stesheni, Mtepeche, pamoja na maeneo yote yanayozunguka mradi huu sasa hivi wanapata maji safi na maji salama. Kwa hiyo, katika hili Mheshimiwa Waziri naomba upokee pongezi na salamu kutoka kwa wale wananchi ambao uliwatembelea mwaka jana na ukaenda kupanda kwenye yale matenki ya pale Chiumbati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nilitaka pia nione na nipongeze ni eneo la upatikanaji wa fedha abayo sasa hivi nafikiri wametutengea. Nimesoma katika kitabu hiki

cha bajeti nimeona kuna shilingi bilioni mbili zimetengwa kwa ajili ya kuuendeleza mradi huu kwa ajili ya kuweka chujio ambalo litasaidia kupata maji mazuri zaidi. Kwa hiyo, sio fedha ndogo hii ni fedha kubwa na kwa uchapakazi ambao Mheshimiwa Mzee Kamwelwe ameendelea nao nina hakika fedha hii tutaipata kwa wakati, ili wananchi wa Masasi, Nachingwea, pamoja na Ruangwa ambao wananaufaika na Mradi wa Mbwinji waweze kupata maji ambayo kimsingi ni mahitaji makubwa sana ambayo tumekuwa tunayahitaji.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo pia, nilitaka nilizungumzie, nimeangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeangalia kwenye kitabu ukurasa namba 120, nimeona fedha ambayo Wilaya ya Nachingwea tumetengewa, shilingi bilioni moja karibu na milioni mia mbili kwa ajili ya maji vijiji. Tunavyo Viji vya Mtua ambavyo kwa muda mrefu vimekuwa vinakosa maji, lakiini pia tunacho kijiji cha Ndomoni, tunacho Kijiji cha Marambo pamoja na maeneo mengine, yote hayo yatapata maji. Ila wito wangu Mheshimiwa Waziri, Mzee wangu Mheshimiwa Kamwelwe naomba nikuombe, mpaka sasa hivi wakandarasi ambao wamepewa kufanya kazi katika maeneo haya tayari *tender* zilishatangazwa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba msukumo wako, ili kazi ya kupeleka maji kwa sababu fedha tayari mmeshatutengea, naomba kwa heshima na taadhima ifanyike, ili wananchi hawa waweze sasa kwenda kupata maji ambayo fedha yake kimsingi tayari hata mkurugenzi wangu mlishtamuita na mmeshampa maelekezo juu ya kwenda kusimamia zoezi la kuanza kazi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, mradi huu au miradi hii ni muhimu sana na itawasaidia wananchi wa maeneo haya kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo nikuombe Mheshimiwa Waziri pale Nachingwea kuna eneo moja linaitwa Mnero Miembeni, kuna mradi mkubwa ambao mwaka jana ulikuwa unatengenezwa na mkandarasi mmoja ambaye kimsingi kazi yake mpaka sasa hivi bado haijaka

sawa. Yapo maeneo ambayo amefunga *solar* ambazo haziwezi kusukuma maji na ule mradi ni mkubwa zaidi umetumia zaidi ya shilingi milioni 150, lakini mpaka sasahivi ninavyozungumza Mheshimiwa Waziri na ofisini kwako nilikuja, bado maji katika maeneo yale ya Mnero Miembeni ambayo yanahudumia vijiji karibu sita mpaka sasa hivi ninavyozungumza bado maji hayajaanza kutoka na yule mkandarasi ni kama tayari alishamaliza kazi.

Sasa tunaomba msukumo wako, tunaomba wataalam waje wachunguze ni sababu gani ambazo zimesababisha kufunga *solar* ambazo zinashindwa kufanya kazi tofauti na malengo ambayo yamkusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni njema, nia ya wizara yako ni njema ndio maana ulitoa fedha. Mradi ule ullikuwa umeenda pia na maendeo ya Nditi kule ambako kimsingi Nditi maji yanapatikana, lakini katika eneo la Mnero Miembeni bado kumekuwa na changamoto ambayo nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri wakati unahitimisha hotuba yako basi utuahidi namna bora ambayo unaweza ukatusaidia, ili maeneo yale wananchi waweze kupata maji ambayo wewe mwenyewe umeyasimamia na mimi nashukuru sana umenipa ushirikiano katika kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka pia, niombe ni eneo la visima. Nilikuomba Mheshimiwa Kamwelwe visima na uliniahidi kwamba utatusadia tupate visima kwa baadhi ya vijiji ambavyo kwa muda mrefu tumekosa maji na uwezekano wa kupeleka maji haya Mbwinji utatuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tunacho Kijiji cha Namanga, hali ni mbaya, wananchi wanatembea umbali wa kilometra karibu 40 kwenda kufuata maji. Hali ile kwa wale mama zetu kidogo imekuwa ni ya kukatisha tamaa. Nia yako ni njema na ulishaniahidi tangu mwaka jana kwamba utatusaidia. Nikuombe sana na ninaleta hili ombi tena, kwamba vile vijiji ambavyo uliniahidi kunipa visima angalao vinne, basi

tutumie nafasi hii ili wale wananchi tuweze kuwasaidia na tuwatue mama zetu ndoo kichwani, ili waweze kufanya shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ambalo nilitaka nichangie ni eneo la mradi wa umwagiliaji. Ndani ya Wilaya ya Nachingwea tunayo miradi mikubwa miwili ya umwagiliaji, eneo mojawapo ni eneo la Matekwe. Mradi huu ni wa muda mrefu kwa kipindi cha nyuma tulishawahi kupata shilingi milioni 500, lakini mradi ulikoishia mpaka sasa hivi ni kama fedha imepotea. Pia pia Mheshimiwa Kamwelwe unakumbuka tulikupeleka eneo moja la Mitumbati pale ukatuahidi utatupa shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuukarabati na kuurejesha ule mradi katika hali yake ya kawaida, lakini mpaka sasa tunavyozungumza nimeangalia katika makabrasha yako sijaona kama umetukumbuka.

Mheshimiwa Spika, wale wananchi wamesimamisha shughuli zao za kilimo, lakini pia, tulikuwa tunatamani tuwarejeshe kwa sababu kipato chao kwa sehemu kubwa wanakipata kuititia maeneo yale. Mimi nikuombe sana mzee wangu na watu wa wizara muweze kuona namna ambavyo zile fedha ambazo tumeziomba zitakavyoweza kwenda kupatikana tuweze kurudisha ile miradi ya umwagiliaji ikae katika utaratibu ambao wananchi wetu wanaweza wakafanya shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi naomba niunge mkono hoja na niwatakie kila la heri watu wa Wizara katika utekelezaji wa bajetio yao. Asante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hassan Masala Mbunge wa Nachingwe.

Mheshimiwa Lucy Magereli kwa dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta. Mheshimiwa Lucy hayupo? Kama Mheshimiwa Lucy hayupo, tuendelee na Mheshimiwa Susanne Maselle atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mwanza umezungukwa na Ziwa Victoria lakini maeneo mengi ya mkoa huu hayana maji. Maeneo kama ya Misungwi, Magu na Buchosa; maeneo haya yako karibu sana na Ziwa Victoria lakini hayana maji. Ni aibu sana kwa Taifa kama hili ambalo lina miaka 57 toka limepata uhuru halafu bado wananchi wana-share maji na viumbe.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Waziri anapokuja ku-*wind up* atueleze wananchi wa Mwanza ni lini tutafaidika na hili ziwa kwa sababu haya maeneo sioni sababu kwanini mama zangu wa kule ninakotoka Misungwi wahangaike kuchota maji na ku-share na wanyama maji machafu wakati wako karibu kabisa na ziwa.

Mheshimiwa Spika, ziwa hili limewasaidia watu wa Misri ambao wanatumia Mto Nile lakini wameweza kupata maji ambayo yanawasaidia hata katika viwanda kwa sababu wameweza ku-utilize hili ziwa vizuri. Sasa kwa nini sisi tunashindwa hata kupata maji ya kunywa tu ambapo ziwa kwa kiwango kikubwa liko katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, nizungumzie miradi ambayo haijakamilika, Mradi wa Lumea Kalebezo. Mradi huu ulianza mwaka 2012 katika Halmashauri ya Buchosa na ultakiwa kutumia miezi sita tu, lakini mpaka sasa hivi miaka sita mradi huu haujakamilika. Mradi huu ulikuwa wa kiwango cha shilingi bilioni 1.69 na mkandarasi ameshapewa shilingi bilioni 1.3 na maji hayajatoka. (*Makofii*)

Sasa Waziri nataka uje utuambie hii hela imeenda wapi, huu ni ubadirifu wa hali ya juu sana. Hela za walipa kodi zinaliwa tu na tunaangalia tu. Nataka uje utuambie hawa watendaji waliyofanya haya mambo, walipolipa hela nyingi kwa mkandarasi wakati hajamaliza kazi watachukuliwa hatua gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu Taasisi za Serikali ambazo hazilipi *bili*. Kwa nini Serikali hawalipi *bili* katika taasisi zao matokeo yake wanakatiwa maji, wanakatiwa na umeme? Hii inasumbua watu wetu, mnawapa adhabu watu wetu ambao wanalipa *bili* kwa wakati. Tunaomba hili tatizo liishe; ni aibu sana kwa Serikali kukatiwa maji au umeme kwa sababu ya kutokulipa *bili* wakati ninyi mmekuwa mbele sana kuwakatia watu. Sasa tunaomba muoneshe mfano katika taasisi zenu.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa hospitali kukatiwa maji, yaani mnategemea sasa watu wetu wafanye nini, kama sisi wenyewe tunashindwa kujisimamia? Ninaomba unapokuja ku-*wind up* utuambie kwamba ni lini sasa mama zetu wataacha kubeba ndoo? Kwa sababu hili limezungumzwa sana na wabunge tumekuwa tukilisemea sana na tunaenda kuitisha bajeti kama kawaida. Tunaomba hii bajeti iende, pesa hizo ambazo tunazitenga naomba ziende kwenye hiyo miradi na miradi ikamilike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika,...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Susanne Maselle, nakushukuru sana. Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mezani, lakini pia namshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii na wakati huo huo nawashukuru wapiga kura wa Urambo ambao wamekuwa wakinipa ushirikiano kila siku, ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, inanibidi nimshukuru Mheshimiwa Waziri Kamwelwe pamoja na Naibu Waziri Aweso pamoja na Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo, Wakurugenzi wote wa Wizara hii kwa jinsi ambavyo wanajitahidi kutatua tatizo

hili kubwa tulilonalo nchini mwetu. Mheshimiwa Waziri ulikuja Urambo na ninakushukuru ulikuja kwa kituo, tukazunguka tukaona shida ya maji tullyonayo Urambo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwetu sisi Urambo changamoto ya kwanza ni maji na wewe mwenyewe ulishuhudia. Tulikwenda Usoke Mheshimiwa Waziri, ukaona jinsi ambavyo wanaume na wanawake wamezunguka kisima kimoja, wote wanasubiri maji yajae kwenye kisima na kisha wanatumia neno ambalo wewe mpaka leo Mheshimiwa Waziri unalijua, wakisema amsha popo, wote kwa pamoja wanashusha ndoo ndani ya kisima, Mheshimiwa Waziri uliona. Ni jambo lilikuhuzunisha wewe mwenyewe binafsi na mimi mwenyewe, hatukuaga kwa jinsi ya uchungu tuliuopata. Tukaanza kuhangai na wewe Mheshimiwa Waziri je, tupate maji kwenye Mto Ugala ikashindikana.

Mheshimiwa Spika, niko mbele yenu ninyi viongozi wa Wizara hii kwa uchungu uliouona Mheshimiwa Waziri nakusihu, nakuomba kwa niaba ya wapiga kura wa Urambo mtupati maji ya kutoka *Lake Victoria*. Wewe mwenyewe umeona hakuna mbadala, visima tunavyochimba vitoe maji kama walivyoongea wenzangu kutoka Mkoa wa Tabora maji yako chini sana. Kwa hiyo, tunapokuomba visima ni ufumbuzi wa muda tu, lakini kwa ufumbuzi wa kudumu Mheshimiwa Waziri nakusihu kwa niaba ya wananchi wa Urambo tupate maji kutoka *Lake Victoria*. Naomba Mwenyezi Mungu akuongoze Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unahitimisha angalau utamke neno la kuwapa matumaini watu wa Urambo, shida ya maji ni kubwa mno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika jitihada ya kupata suluhisho la muda tuliomba kuchimbiwa visima, tukapata Mkandarasi akatuchezea akili, tukarudi kwako wewe Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara yako wakatusaidia katuunganisha na Wakala wa Uchimbaji Maji inayoitwa *DDCA*. Tunaomba Mheshimiwa Waziri utusaidie, kwa kuititia wizara yako ili huu wakala unaochimba maji uje uchimbe maji angalau kwenye vijiji 17 ambavyo vina shida sana ya maji.

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Waziri utaisukuma hii *DDCA* ili angalau ilete vyombo vyake tuone tuanze kupata matumaini, kwa sababu mpaka sasa hivi hawajafika na sisi tuna shida sana ya maji na hatuombi kwamba ishindikane fedha zirudi, zishindwe kutumika katika mwaka huu wa fedha. Tunakusih i sana Mheshimiwa Waziri utuangalie Urambo kwa jicho la huruma kutokana na shida ya maji tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, la pili Mheshimiwa Waziri tunaona kwamba katika kupata suluhisho la muda tukisubiri mradi huo mkubwa ambaonaamini Mwenyezi Mungu atakusaidia tupate kutoka *Lake Victoria*, tunaomba tuchimbiwe bwawa. Kuna eneo zuri sana wataalam wetu walishaleta udongo Wizara ya Maji ili upimwe udongo ule kuona aina ya udongo ambayo unaweza kufaa kwa *ku-retain* maji yaani kwa kutunza maji. Eneo hilo zuri sana, bonde zuri sana ukija tena tutakupeleka Mheshimiwa ukaone, lakini tutafurahi kama wakija wataalam waone eneo ambao linaweza kuchimbwa bwawa zuri sana eneo la Kalemela.

Mheshimiwa Spika, nimeona, mimi nina wivu wa maendeleo, nimeangalia kwa wenzangu wanachimbiwa mabwawa, naamini kwa jicho lako la huruma pia na sisi Urambo tutachimbiwa bwawa la maji katika eneo la Kalemela ili na sisi tuwe na chanzo kimojawapo cha kupata maji ya kutusaidia wakati tukisubiri maji kutoka kwenye mradi mkubwa ambao naamini kwa jicho la huruma utatuingiza na sisi katika huo mradi ambao unahusisha milioni kama 500 hivi za fedha za kigeni kutoka India.

Mheshimiwa Spika, mimi nachukua nafasi hii kuwaunga mkono Wabunge wenzangu wote waliotangulia kuzungumzia umuhimu wa kuwa na Mfuko wa Maji Vijijini. Tumeona jinsi ambavyo *REA* inafanya kazi vizuri, tunaamini tukianzisha Mfuko Maalum wa Maji Vijijini, hili suala la maji linaweza kupata ufumbuzi. Kwa hiyo, naunga mkono wenzangu waliotangulia walioongea kusema tupate angalau ushuru au jina lolote mtakalotumia wa shilingi 50

kutoka kwenye dizeli na petroli ili isaidie kuunda mfuko huo ambao tunaamini utasaidia upatikanaji wa maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa siku ya leo ni tatizo hili ambalo nadhani linahitaji si wizara moja tu, nadhani linahitaji Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wakati huo huo TAMISEMI na Wizara yako mkae pamoja muone jinsi gani ambavyo mtahakikisha kwamba tunathamini kuvuna maji ya mvua. Kwa kweli ukiangalia maji ya mvua yanavyopotea na shulenii watoto wa kike, wa kiume wote wanashindwa kupata hata maji ya kunawa mikono baada ya kwenda sehemu zile wanazokwenda. Kwa hiyo, mimi ningeomba kuwe na sheria fulani ya uvunaji wa maji ya mvua ili tuondokane na shida ya maji hasa katika maeneo ya taasisi zetu za shule na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pengine Wizara ya Elimu inaweza ikaamua kwamba shule isifunguliwe mpaka kuwe na utaratibu wa kuvuna maji ya mvua. Kwa sababu ni jambo la kusikitisha mvua inavyonyesha hasa kwa mfano kama sasa hivi mvua inanyesha Dar es Salaam na wapi, lakini maji yanapotea, na wakati huo huo unakuta watoto hawana maji mashulenii na kwenye taasisi kama hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa nafikiri kuwe na kautaratibu fulani ka kulazimisha, wenzetu kwa mfano, kwa taarifa nilyonayo na nimeshuhudia nilikwenda Bamuda. Kwenye Kisiza cha Bamuda wameweka utaratibu kwamba hujengi nyumba yako wewe ya kuishi kabla hujaonesha jinsi utakavyovuna maji ya mvua. Sasa na mimi nilikuwa nafikiri na sisi tungekuwa na utaratibu huo hasa hizi taasisi zetu isifunguliwe mpaka utaratibu wa kuvuna maji uwekwe. Wakati huo huo nichomekee na hapa hapo, maji na choo yaani kuwe na maji uvunaji wa maji na choo ndio taasisi iandikishwe. Nimechomekea hilo kwa sababu naona vinaenda karibu pamoja tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba kumalizia kwa kurudia tena kilio chetu sisi watu wa Urambo. Pamoja na shukrani zetu kwako wewe Mheshimiwa Waziri, Naibu

Waziri ambaye pia alikuja akitokea Kigoma nawasihi mtuweke. Hata kama hamkututaja kwenye kitabu hiki muone jinsi ya kutuingiza sisi kama Urambo kwenye mradi wa kupata maji kutoka *Lake Victoria* kama ukombozi wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru nawapongeza kwa kazi ngumu mnayoifanya lakini niko mbele yenu kuwaomba mtukumbuke Urambo, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Margaret Sitta. Sasa Mheshimiwa Seif Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii nami kuchangia jioni hii ya leo. Kwanza nipongeze Wizara kwa juhudini mbalimbali ambazo inazifanya katika kuhakikisha kwamba inatatu changamoto za maji ambazo zipo katika maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengi wamezungumza juu ya tatizo la maji katika maeneo yetu na mimi nilipata bahati kuwa katika Kamati hii ya *LAAC*, tulibahatika kwenda kule Mbeya tukaenda kujiona hii miradi ya maji inavyotekelizwa. Tulienda pale maeneo fulani yanaitwa Kyela na sehemu moja panaitwa Tukuyu. Kuna fedha zilitengwa kule, katika usanifu zikahitajika kama shilingi bilioni moja mradi utekelezwe. Mradi ule umeenda ukakwama katikati, wakafanya tena wakataka kama shilingi bilioni nne hivi. Mradi ule wakagawa kwa wakandarasi wengi sana lakini *at the end of the day* hakuna ambacho kimefanyika mpaka siku tunakwenda kama Kamati kwenda kushuhudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukatoka pale tukaenda Tukuyu, tulivyofika tukakuta *story* ni ile ile iliyoko Kyela iko Tukuyu, shilingi bilioni moja imeenda shilingi bilioni nne, shilingi bilioni nne ikaenda shilingi bilioni saba. Wamegawanyishwa wakandarasi; mkandarasi huyu kafanya kwa hatua fulani , mwingine ameingia mitini, yaani ni kama vile mchezo fulani ambao ndiyo yale yaliyokuwa yanazungumzwa hapa na waheshimiwa wenzangu hapa kwamba ni kama kuna ka-

*chain ambako kuna fedha zinatiririka zinaliwa na kama kuna-hang yaani hakuna ile kunakuwa kama sintofahamu na miradi hii imekuwepo ndani ya nchi yetu yote.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani hata juzi walikuja Kamati ya LAAC pia kukagua mradi wa maji Wilaya ya Igunga. Walienda kijiji kimoja kinaitwa Blangamilwa tulipata fedha lakini ni zaidi ya shilingi milioni 700. Katika hii juzi iliyokuja shilingi milioni 900. Wameenda kuangalia utekelezaji mabomba yaliyowekwa ilitakiwa wajenge matenki ya kuhifadhi maji, wameenda kununua matenki ya shilingi laki tatu/tatu kaweka matenki mawili. Ni jambo la aibu kwenye miradi hii ya maji ni janga lingine la kitaifa kwenye hii miradi ya maji ni janga la kitaifa.

Mheshimiwa Spika, tumeona tunaunda tume mbalimbali kufuatilia, Tume ya Makinikia, sjui Tume ya Madini ya Almasi; hebu sasa nikuombe, na juzi tumemsikia Rais alipiga simu pale kila mmoja akamwagiza Katibu Mkuu aende kwenye kile kijiji kutatua tatizo la maji kwa mkandarasi yule. Nikuombe tuisaidie Serikali tuunde tume ifuatilie miradi ya maji nchi nzima iletu taarifa na tutoe *way forward* ambayo itaweza kusaidia hii Serikali wapi twende. Nimekusikia ulipokuwa unasema hawa watu ni wapya. Ni kweli Mheshimiwa Waziri ni mpya, Naibu Waziri mpya hata Katibu Mkuu ni mpya. Sasa kwa sababu ya upya wao tuwasaidie kuhakikisha kwamba wapi tulikosea, wapi tupo, wapi tunatakiwa twende kupitia miradi hii ya maji na itatatura tatizo ambalo tunalo katika miradi yetu ambayo tunayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunazungumza kwamba Wizara ya Maji haina fedha, lakini hata fedha zilizokuwepo zinazopelekwa ndivyo zinavyoliwa. Leo mimi binafsi naunga mkono tuongeze fedha shilingi 50 iwe shilingi 100 katika kodi ya mafuta, lakini kwa utaratibu huu ambao uliokuwa unaendelea na ukaendelea maana yake tutaweza kuongeza fedha nyangi zaidi, lakini...

*(Hapa umeme ulikatika)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, naona sijui utaratibu tuendelee hivyo hivyo? Kwa hiyo, hapo nimetumia kama dakika mbili kwa hiyo bado dakika zangu unilinde tu.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huo huo ambao tunaushuhudia katika maeneo mbalimbali ya ubadhirifu wa fedha hizi za umma unavyojitokeza iko haja ya Bunge kuchukua hatua na kuisaidia Serikali katika utatuzi wa miradi hii ya maji ambayo... (*Makofii*)

*(Hapa umeme ulirudi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, inabidi askari wawe imara, maana yake dhahabu hii kuna Wasukuma hapo. (*Kicheko*)

Endelea Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kuchangia, Mheshimiwa Waziri alikuja jimboni kipindi ambacho akiwa Naibu Waziri wa Maji. Alikuja akatembelea Choma cha Nkola akaona mbuga kubwa ya ulimaji wa mpunga ambayo ilivyokuwa ikistawi mpunga na aliona maeneo ambako bwawa kubwa lilikuwa limekuwa *designed* kwa ajili ya kuchimbwa na akaahidi kulifuatilia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilibeba *documents* zote za *feasibility study* ambazo zilifanyika kwa ajili ya uchimbaji ule wa bwawa. Bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja kama Naibu Waziri. Leo amekuwa Waziri kamili, kwenye kitabu hiki nilikuwa nataka kuangalia angalau nione labda ametenga sasa fedha za kuanzia uchimbaji wa bwawa lile, sijaona sehemu yoyote ambako ameweka na ukizingatia tunapata mvua na mvua ni nydingi. Sasa tunapoziacha zinapotea na mbuga tunayo kubwa maana yake uzalishaji unapungua badala ya kuongezeka na kama tuna mbuga tungeitumia vizuri tukazalisha mpunga kwa wingi tukaweza kuuza ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Waziri alichukulie hili suala la bwawa kwa uzito wake wa hali ya juu sana. Hili suala la bwawa, tuna maeneo mengi ya uchimbaji wa bwawa, tunaweza tukachimba bwawa kubwa pale Choma ambapo tayari *documents* zote anazo mpaka na Mwenyekiti wa Umwagiliaji Taifa alimwita hapa Dodoma kwa ajili ya kulifanya uchambuzi wa kina tupate fedha, lakini sijona. Hata ukienda Ziba pale tuna maeneo makubwa sana ya uchimbaji wa mabwawa na maji ni mengi yanapotea pale, tungechimba sisi bwawa lingine pale Ziba, lakini tungechimba bwawa lingine pale Simbo ambako lingeweza kusaidia kilimo cha umwagiliaji ambacho kingeondoa tatizo la njaa. Katika nchi yetu kuwa na njaa ni aibu.

Mheshimiwa Spika, sehemu nydingine ambayo nilitaka kuchangia ni kuhusu wakandarasi, sasa hivi wako *site wanafanya* kazi ya usambazaji maji katika mijji midogo midogo. Kwa mfano kuna mkandarasi anafanya kazi ya usambazaji maji katika Kijiji cha Isenegeja Kata ya Mwisi amesha-*raise* zile *certificate* Wizarani shilingi milioni 180 hajatolewa leo ni muda mrefu. Sasa huyu mkandarasi atasimama na akisimama maana yake atachelewa ataacha kufanya kazi halafu vile vifaa vilivyopo vitaibiwa na vikiibiwa maana yake mradi utaanza kupoteza mwelekeo.

Mheshimiwa Spika, niombe sasa wizara zile *certificate* ambazo zimekuwa *raised* pale Kata ya Mwisi na katika Vijiji vile vya Mwamala, Mwakabuta na Mangungu *certificate* zake ambazo zipo wizarani nimuombe Waziri atoe *go ahead* ili hawa wakandarasi waendelee. Kwa sababu tunapochelewesa inaweza kusababisha upotevu wa vifaa ambavyo tayari viko katika maeneo yetu. Nimuombe Mheshimiwa Waziri alichukue hili na alifanyie kazi. (*Makofii*)

*(Hapa umeme ulikatika na kurejea)*

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Gulamali ili umalizie.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa napenda kuchangia kwa usiku wa leo,

katika maeneo yetu yako maeneo ambayo visima vinachimbwa na maji tunapata kwa kiwango fulani. Tafiti zimefanyika katika baadhi ya maeneo imebahatika kuna sehemu kuna maji, tunaweza tukapata, na wao pia wame-raise certificate ambazo ziko wizarani. Nilikuwa nimuombe tu Waziri kwamba aweze kutoa *go ahead* ili hizi kazi ziweze kufanyika na wananchi waweweza kupata maji katika yale maeneo ambako utafiti umefanyika na maji yamepatikana. Tunaishukuru Serikali mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria unatoka sasa Nzega unakwenda Igunga na baadhi ya vijiji vyetu vitapata maji.

Kwa hiyo ni shukrani pekee ziende kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli; lakini pili na watu ambao wako wizarani pale kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Timu yao nzima kuhakikisha kwamba wanasimamia kwa ukaribu mradi huu uweze kutekelezwa kwa umakini sana.

Napenda kuunga mkono hoja ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Seif Gulamali, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, uchangiaji wetu unaendelea vizuri, kwa kweli wengi sana wamepata nafasi na wale ambao bado kidogo basi kesho tutapata namna ya kumalizia na pia Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kujibu hoja zetu kwa wakati muafaka, maana ni nydingi.

Liko tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho Jumatano tarehe 9 Mei, 2018 kutakuwa na warsha ya Wabunge Wanachama wa Chama cha Kuhamasisha Afya Bora na Jinsi ya Kujikinga na Magonjwa Yasiyoambukiza (*Non Communicable Diseases Forum*). Wabunge wanachama wa chama hicho na wabunge wengine ambao mko *interested* na kujunga na *forum* hiyo mnaombwa kuhudhuria warsha hiyo itakayofanyika saa saba mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Spika, lakini wale wa *forum* kama mtakuwa na mawazo ni vizuri kama mtakutana mapema, tuandikieni ili kesho saa nne tuambiane pia mnaweza mkakutana mapema kidogo maana huenda mchana pakawa na vikao vingine tena vikaingilia zoezi lenu muhimu. Kwa hiyo, mtatujulisha kesho tuweze ku-*confirm* lakini otherwise wale *Non Communicable Diseases Forum* mtakuwa na warsha hiyo kesho.

Nina funguo hapa huenda ni ya Mheshimiwa Mbunge au nini ya mlango, usije ukalala nje Mheshimiwa ambaye umepoteza funguo wako. Nitaacha kwa Makatibu wangu mezani hapa, kwa hiyo, yejote ambaye amepotelewa na ufunguo upo hapa.

Waheshimiwa Wabunge niwashukuru sana kwa kazi nzuri sana iliyofanyika siku ya leo na michango mizuri sana ambayo kwa kweli imewajenga wenzenzu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na wameona kwa kweli uzito uliopo katika jambo hili la maji katika nchi yetu. Kama walivyosema Wabunge wengi basi Wizara ya Fedha jamani mjue kilio cha Wabunge hawa ni maji. Maji kwanza, mambo mengine nayo pia ni muhimu pia, kwa hiyo tunatarajia kama wanavyosema waheshimiwa wabunge paongezeke hapa na pale basi ni vizuri muanze kuliangalia hilo mapema, maana mwaka jana lilikuja lakini likananii... (*Makofi*)

Tunatumaini mwaka huu hakutakuwa na haja ya mivutano tena katika eneo hilo, kwa sababu lengo ni wananchi wetu wapate huduma ya maji kwa uhakika. (*Makofi*)

Basi baada ya hayo kwa kuwa muda wetu wa kuahirisha Bunge umeshafika, basi nichukue fursa hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 1.45 Usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 9 Mei, 2018 Saa Tatu Asubuhi*)

